# Nipashe

Ijumaa Desemba 6, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580094

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710

Albinism Hotline

- Jifunze kuhusu Ualbino
- Toa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino

0800 75 00 50

Piga simu bure



## Tahadhari mvua ya kimbunga mikoa 17

UKURASA 3

# Ma-RC MTEGONI

**WATAKIWA** kujenga madarasa 1,500 ndani ya siku 86...*Endelea ukurasa wa 2*



Selemani Jafo



## ZITTO AJITOSA KUMKABILI MAGUFULI 2020

UKURASA 2

## YALIYOMO

**UKURASA WA 2**

**KARIAKOO NYINGINE SASA KUANZISHWA**
SHIRIKA la Masoko Kariakoo, limesema liko mbioni kuanzisha soko lingine nje ya Jiji la Dar es Salaam, eneo la Makonde Mbezi Beach...

**UKURASA WA 4**

**MASHINJI AANIKA BARUA YA MSIMAMIZI UCHAGUZI**
KATIBU Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Dk. Vincent Mashinji, anayekabiliwa na wenzake wanane...

**UKURASA WA 25**

**MAHARI YAONDOLEWA BAADA YA WANAUME KUSUSA KUOA**
MAMLAKA nchini Nigeria imesitisha uamuzi wa kuwakata kodi wananchi wanaoishi Kaskazini...

## BABU APIGWA MSIBA MJUKUU

UKURASA 3




**MICHEZO** KASEJA ATEMWA KILIMANJARO STARS UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Kariakoo nyingine kuanzishwa

Na Mwandishi Wetu

SHIRIKA la Masoko Kariakoo, limesema liko mbioni kuanzisha soko lingine nje ya Jiji la Dar es Salaam, eneo la Makonde Mbezi Beach.

Akizungumza na Nipashe jijini wiki hii, Meneja Mkuu wa shirika hilo, Hetson Msalale, alisema mradi huo ni sehemu ya mageuzi yanayoendelea tangu kupata bodi na menejimenti mpya miaka minne iliyopita, baada ya kuikosa kwa miaka 16.

Msalale alisema mradi wa soko hilo jipya unatarajiwa kugharimu zaidi ya Sh. milioni 500 na hadi sasa uko katika hatua za upembuzi, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mpango mkakati unaoendelea.

Kwa mujibu wa meneja huyo, miradi mingine inayotarajiwa kwenda sambamba na huo wa Mbezi, ni kufanya mageuzi ya kuboresha jengo la soko lake dogo, kuligeuza katika mhimili mkubwa na wa kisasa, likikadiria kutumia zaidi ya Sh. bilioni 23.

Alitaja mpango mkakati wa miradi mingine unaohusu uwekezaji katika viwanja vyake viliyoko eneo la Tabata Bima katika Manispaa ya Ilala, ambako kuna baadhi ya majengo yake.

*Soma zaidi ukurasa wa 14.

# Ma-RC mtegoni wanafunzi 58,000 wakikosa sekondari

**Na Paul Mabeja**, DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amewaweka mtegoni wakuu wa mikoa, baada ya kuwataka kujenga vyumba vya madarasa 1,467 ndani ya siku 86 kuanzia jana.

Lengo ni kupata madarasa yatakayotumiwa na wanafunzi 58,699 (asilimia 7.73) waliofaulu mtihani wa darasa la saba mwaka huu, lakini wamekosa nafasi za kujiunga na kidato cha kwanza mwakani, kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa.

Katika taarifa yake ya uchaguzi wa wanafunzi wa kujiunga na kidato cha kwanza mwakani aliyoitoa kwa waandishi wa habari jana, Jafo alibainisha kuwa kati yao, wavulana ni 28,567 (asilimia 48.53) na wasichana 30,132 (asilimia 51).

Jafo alisema kutokana na hali hiyo, anaagiza wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya zilizobakiza wanafunzi, kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa ifikapo Februari 29 mwakani.

Ingawa waziri huyo hakutaja idadi ya vyumba vya madarasa vinavyohitajika, wanafunzi 58,699 ni sawa na madarasa 1,467 kwa uwiano wa wanafunzi wa 40 kwa kila chumba cha darasa.

Jafo pia aliagiza makatibu tawala wa mikoa na wakurugenzi wa halmashauri husika, wasimamie utekelezaji wa agizo hilo ili kuhakikisha wanafunzi wote waliobaki wanajiunga na kidato cha kwanza ifikapo Machi 2 mwakani.

Aliitaja mikoa yenye uhaba wa vyumba vya madarasa na idadi ya wanafunzi waliobaki kwenye mabano kuwa ni Arusha (4,739), Dar es Saalam (5,808), Iringa (3,480), Kigoma (12,092), Lindi (1695), Manyara (728), Mara (9,493), Mbeya (2,716), Pwani (2,918), Rukwa (686), Simiyu (6,616), Songwe (4,684) na Tanga (3,044).

"Wanafunzi wote hao watajiunga na masomo yao baada ya vyumba vya madarasa kukamilika," waziri huyo alisema.

Jafo alibainisha kuwa mikoa ya Dodoma, Geita, Kagera, Katavi, Kilimanjaro, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Njombe, Ruvuma, Shinyanga, Singida na Tabora imewachagua wanafunzi wote waliofaulu kujiunga na kidato cha kwanza katika shule za sekondari za serikali.

Alisema baada ya uchaguzi kukamilika, wanafunzi 701,038, sawa na asilimia 92.27, wakiwamo wavulana 335,513 (asilimia 47.86) na wasichana 365,525 (asilimia 52.14), wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwezi ujao.

Jafo alifafanua kuwa kati ya waliofaulu, wamo wanafunzi wenye ulemavu 1,461, sawa na asilimia 0.19 (wavulana 777 na wasichana 684).

Jafo pia aliwataka walimu wote na watumishi katika idara ya elimu, kuacha kuweka vikwazo vyovyote kwa wanafunzi waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza, ikiwamo kuwatoza michango ili kutekeleza kwa vitendo dhana ya elimu bila malipo.



Kiongozi wa ngoma ya asili Bugimbagu kutoka Kata ya Mwawaza, Manispaa ya Shinyanga, Mahona Mtoba (kulia), akichezea joka aina ya chatu katika maadhimisho ya siku ya kupinga ukatili wa kijinsia, yaliyoandaliwa na Shirika la Agape, mjini Shinyanga jana. Katikati ni Mkuu wa kikosi cha usalama barabarani Wilaya ya Shinyanga, Emmanuel Palangyo. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Zitto ajitosa kumkabili Magufuli uchaguzi ujao

**Na Mwandishi Wetu**

KIONGOZI Mkuu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, amesema anatamani kuwa Rais wa Tanzania na yuko tayari kuchuana na Rais John Magufuli kusaka kiti hicho katika uchaguzi ujao.

Hata hivyo, kiongozi huyo wa zamani wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), amesema ndoto yake hiyo itatimia ikiwa atapewa ridhaa na vyama vingine vya upinzani nchini.

Akihojiwa kwenye kipindi cha 'Konani' kinachorushwa na ITV, Zitto alisema ili upinzani uongoze nchi, ni lazima waungane na kuwa na mgombea mmoja, na kama atapata ridhaa ya chama chake na vyama vingine, angependa awe mwakilishi wao.

"Ningependa siku moja niwe Rais wa Tanzania, nina agenda kwanini ninapenda, lakini huwezi kuwa Rais kwa kutaka kwa kuwa kuna michakato ikiwamo uamuzi wa chama na vyama," alisema.

Kwa mujibu wa Zitto, kwa mazingira yoyote yale, uchaguzi wa mwakani ni lazima vyama vya upinznai kushirikiana na kuwa na mgombea mmoja wa kupambana na Chama Cha Mapinduzi (CCM), kinachotarajiwa kuwakilishwa na Dk. Magufuli katika kuwania nafasi ya urais.

"Iwapo vyama vikiona kwamba mimi (Zitto) ndiyo mgombea ninayestahili kupeperusha bendera ya umoja wa vyama... lakini iwapo vyama vikiona kuna Mtanzania mwingine wa chama kingine ambaye ataweza kutupatia faida akiwa mgombea, mimi nitamuunga mkono huyo.

"Suala la kugombea au kutokugombea limetoka nje ya matakwa yangu binafsi, limekwenda kwenye matakwa ya chama ambacho mimi ni kiongozi, na vyama vingine rafiki tunavyofanya kazi kwa pamoja, suala si kuwa kwenye karatasi ya kura, bali kuwa kwenye karatasi ya kura na kushinda, na ukishashinda utafanya nini," alisema. Aliongeza kuwa iwapo atapata ridhaa hiyo, atahakikisha anabadili maisha ya Watanzania milioni 14.7 wanaoishi katika lindi la umaskini licha ya nchi kuwa na rasilimali nyingi.

Zitto alisema kati ya mwaka 2007 hadi 2012, Watanzania milioni moja waliondoka kwenye dimbwi la umaskini lakini kati ya 2016 na 2019, Watanzania milioni 2.7 wametumbukia kwenye umaskini.

**DEMOKRASIA**

Alisema kila mtu ana mchango wa kuihami demokrasia kwa namna yoyote isianguke na kurudi kwenye mfumo wa chama kimoja ambao alidai unaelekea kujitokeza nchini.

Zitto alidai alifukuzwa Chadema kutokana na kupishana kimtazamo kuhusu itikadi na mikakati ya uendeshaji wa chama na kwamba tofauti hizo hazikutatuliwa na ilikuwa lazima atoke kwenda kuanzisha chama kipya.

Alisema kufukuzwa kwake hakukuwa na uhusiano wowote na nafasi ya Mwenyekiti wa Chadema kwa kuwa wakati huo hakukuwa na uchaguzi ndani ya chama.

**UCHAGUZI S/MITAA**

Zitto pia alizungumzia uchaguzi wa serikali za mitaa uliofanyika Novemba 24, mwaka huu, akidai ulivurugwa kwa kuhakikisha wagombea wa upinzani wananyimwa fomu ili CCM ipite bila kupingwa.

Alidai viongozi wa upinzani wanashauriana kuhakikisha wanadhibiti yaliyotokea kwenye uchaguzi huo hayajitokezi kwenye uchaguzi mkuu.

"Tutahakikisha nguvu zetu katika mambo 10 tunayoyafanya kama vyama vya siasa, la kwanza hadi saba ni tume huru ya uchaguzi, ili kuwa na uchaguzi wa kweli ambao ni huru na haki," alisema.

**KUMPOKEA SUMAYE**

Kuhusu kumpokea Waziri Mkuu mstaafu, Frederick Sumaye, Zitto alisema wako tayari kupokea ushauri wake na pale watakavyohitaji watakwenda kumuona kwa kuwa moja ya sifa ya chama chake ni kuthamini wastaafu waliotumikia nchi.

"Tunawathamini bila kujali itikadi za vyama, wakati wowote tutakapohitaji ushauri wa aina yoyote, tutamuona na tunaamini atatufungulia mikono, ni Waziri Mkuu, amehudumu kwa miaka 10 toka akiwa na umri wa miaka 43 hadi miaka 53," alisema.

Aliongeza kuwa Sumaye alikuwa Waziri Mkuu wa kwanza wa Bunge la mfumo wa vyama vingi na uzoefu wake ni muhimu na utahitajika.

## HABARI KITAIFA



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mbezi, wakipata maelezo kutoka kwa Mwandishi wa Habari Mwandamizi wa Gazeti la Nipashe, Salome Kitomari, walipofanya ziara ya mafunzo katika ofisi ya kampuni ya The Guardian Ltd, Mikocheni Viwandani, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# TPA yajipanga kuteka biashara A. Mashariki

**Na Elizabeth Zaya,** MWANZA

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari (TPA) kupitia bandari zake za Ziwa Victoria imeanza kujipanga kukamata soko la biashara katika nchi za Afrika Mashariki.

Meneja wa bandari hizo, Morris Mchindiuza, akizungumza na waandishi wa habari waliotembelea bandarini jana, alisema tayari mikakati ya kufikia lengo hilo imeanza. Alisema tayari timu ya wataalamu kutoka taasisi mbalimbali wanazoshirikiana nazo, imeundwa na wameshaanza kutembelea na kufanya mazungumzo na baadhi ya nchi kwa ajili ya kufanikisha mkakati huo.

"Tumeshirikisha taasisi mbalimbali ambazo zinashiriki katika shughuli za bandari pamoja na jumuiya za wafanyabiashara na tumeenda katika baadhi ya nchi.

"Lengo letu ni kuboresha na kupanua zaidi huduma zetu na tunataka tuongeze kiwango cha mizigo katika kila nchi inayopita katika bandari zetu.

"Na tunataka kutumia pia ujio wa reli ya kisasa katika kufanikisha hili, tuko kwenye mchakamchaka wa kuongeza hata maeneo ya bandari kavu kwa maana mizigo itakuwa mingi.

"Tumeanza kulipa fidia kwa wananchi ili watupishe na tulianza kwa kuwaelimisha umuhimu wa jambo hili na wametuelewa," alisema.

Mchindiuza alibainisha mkakati mwingine kuwa ni kuangalia upya mifumo ya kufanikisha hilo ikiwa ni pamoja na kufanyia kazi upungufu uliopo katika baadhi ya maeneo, kuboresha miundombinu na kuwa na vifaa vya kisasa vya kuhudumia abiria na mizigo kwa uharaka na ufanisi.

Alisema lengo lao la sasa ni kuhakikisha kufikia mwaka 2025, wanakusanya mapato kuanzia yanayoanzia Sh. bilioni nne hadi tano kwa mwaka.

Alisema mkakati mwingine ni kuhakikisha wanadhibiti bandari bubu kwa kurasimisha zitakazokuwa na sifa na kuziondoa zitakazokosa sifa.

"Nia ya kurasimisha hizi bandari bubu, kwanza serikali itaongeza mapato, lakini pia itasaidia kurahisisha kudhibiti mambo mengi ikiwamo wahamiaji haramu, biashara za magendo na hata mlipuko wa magonjwa kwa sababu mamlaka zote zitawekwa katika bandari hizo," alisema.

# Tahadhari mvua ya kimbunga mikoa 17

**Na Faustine Feliciane**

MVUA kubwa zinatarajia kunyesha ndani ya siku tano kuanzia jana katika mikoa 17 ukiwamo mkoa wa Dar es Salaam na Pwani, huku Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) ikitoa tahadhari.

Kwa mujibu wa utabiri wa siku tano uliotolewa jana na TMA, mvua hizo zilianza jana kwa baadhi ha maeneo ya mikoa ya Dar es Salaam na Pwani na zitaendelea katika mikoa ya Katavi, Kigoma, Tabora, Kagera, Geita, Mwanza, Mara, Simiyu na Shinyanga.

Meneja wa Huduma za Utabiri wa TMA, Samuel Mbuya, alisema kwa leo mvua kubwa zinatarajiwa katika mikoa ya Rukwa, Mbeya, Ruvuma, Songwe, Iringa na Njombe.

"Athari zinazoweza kutokea ni kubwa husasani kwa baadhi ya maeneo ya mkoa wa Dar es Salaam ambapo kunaweza kutokea kwa uharibifu wa miundombinu, maeneo ha makazi kuzungukwa na maji na hali mbaya zaidi kwa wakazi wa maeneo ya mabondeni," alisema Mbuya.

INAENDELEA UK. 8

# Babu apata kipigo msiba wa mjukuu

**Na Gurian Adolf,** MPANDA

MKAZI wa Mtaa wa Makanyagio, Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi, Otonatus Sokoni, amepokea kipigo kutoka kwa mtoto wake wa kike na waombolezaji wa msiba wa mjukuu wake.

Babu huyo alipokea kipigo hicho baada ya kuwafukuza waombolezaji msibani muda mfupi baada ya mazishi.

Tukio hilo la aina yake lilitokea juzi majira ya saa 11:00 jioni katika mtaa huo kwenye msiba wa Catherin Hilary (11) ambaye alikuwa mwanafunzi wa darasa la sita Shule ya Nsingi Kashato, Manispaa ya Mpanda. Siku ya tukio, waombolezaji na ndugu wa marehemu, walishiriki kwa wingi maziko ya mtoto huyo katika makaburi ya Mwangaza ikiwa ni siku nne tangu alipofariki dunia baada ya kuugua ghafla.

Kwa mujibu wa mashuhuda wa tukio hilo, baada ya kumaliza shughuli za maziko, ndugu wa marehemu na waombolezaji walirudi nyumbani, ambako ni nyumbani kwa Mzee Sokoni ambako msiba ulikuwako ili kupata taratibu zingine za msiba huo.

Wakati waombolezaji na ndugu wakiwa wanasubiri kupata taratibu, babu huyo alianza kuwafukuza waombolezaji akidai kuwa waondoke kwenye nyumba yake kwa kuwa shughuli za mazishi zimeisha, hivyo haoni sababu ya wao kuendelea kuwapo hapo na hataki kuweka matanga nyumbani kwake. Ndugu wa marehemu kutoka upande wa baba, ambao walitoka Tarafa ya Mpimbwe Wilaya ya Mlele, baada ya kuambiwa kauli hiyo waliamua kuondoka na kwenda kutafuta usafiri wa kurudi kwao.

Kutokana na kauli hiyo, waombolezaji wengine na ndugu wa marehemu kutoka upande wa mama, walishikwa na butwaa hali ambayo ilimfanya mama wa marehemu, ambaye ni mtoto wa Mzee Sokoni, apandwe na hasira na kuamua kumpa kichapo baba yake mazazi.

Baada ya kuona mtoto wake ameanza kumpiga baba yake, waombolezaji wengine na wanandugu waliungana na mama wa marehemu kumpa kipigo babu huyo.

Kipigo hicho kilipozidi, alianza kupiga mayowe ya kuomba msaada, lakini watu hao waliendelea kumshushia kichapo.

Kutokana na kipigo hicho kuzidi, Mzee Sokoni aliamua kukimbia na kuchukua pikipiki yake na kisha kuondoka na kuelekea kwenye nyumba yake nyingine iliyoko katika kijiji cha Itenka, Halmashauri ya Nsimbo mkoani humo.


## HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

## MNADA WA UUZAJI WA VIWANJA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma anawatangazia Wananchi wote kuwa zoezi la uuzaji wa Viwanja kwa njia ya Mnada litafanyika tarehe **14 Disemba, 2019** siku ya Jumamosi. Mnada utafanyika katika eneo la wazi la Manispaa ya zamani (karibu na Sabasaba) kuanzia saa 4:00 Asubuhi.

Viwanja vinavyouzwa ni Maeneo ya:

| ENEO | MATUMIZI NA BEI TSHS KWA (SQM1) |
|---|---|
| IYUMBU (New Town Centre) | • Viwanja vya Nyumba za kupangisha (Apartments)<br>• Viwanja vya Biashara<br>• Viwanja vya Viwanda Vidogo |
| NALA (Industrial Area) | • Viwanja vya Viwanda vya aina mbalimbali |
| NJEDENGWA (Investment Centre) | • Viwanja vya Nyumba za kupangisha (Apartments)<br>• Viwanja vya Biashara |
| NZUGUNI (Jirani na Uwanja wa Mpira, Soko Kuu na Stendi kuu mpya ya mabasi) | • Viwanja vya Hoteli<br>• Viwanja vya Biashara<br>• Viwanja vya Maduka makubwa (Shopping Malls) |

**NB**:

- Asilimia 50 ya Malipo italipwa siku ya Mnada
- Asilimia 50 inayobaki italipwa ndani ya siku 14 baada ya Mnada.

Tangazo hili limetolewa na:
**Mkurugenzi wa Jiji,**
**DODOMA**

# EAC yasaidiwa zaidi ya bil. 30/-

**Na Daniel Sabuni,** ARUSHA

SHIRIKA la Maendeleo la Ujerumani (giz), limetoa msaada wa Dola za Kimarekani milioni 16 (zaidi ya Sh. bilioni 30) kuendelea kuwezesha Jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia mpango wa kuwezesha biashara, masoko na mambo ya mtangamano wa EAC 'SEAMPEC' na mipango ya kupambana na magonjwa ya kuambukiza.

Akizungumza kabla wa kutiliana saini na Katibu Mkuu wa EAC, Liberat Mfumukeko, Ofisa Balozi anayeshughulikia Mambo ya Nje, Joerg Herrera, alisema misaada na ushirikiano wa giz na EAC kuwezesha sekta mbalimbali kumewezesha kukua katika nyanja za biashara, afya na maendeleo ya viwanda.

Mkataba huo wa makubaliano ya msaada yalisainiwa kwenye makao makuu ya Jumuiya ya EAC jana.

"Tumetekeleza miradi mingi kwenye kilimo cha biashara, utalii, dawa kwa kweli tunajivunia maendeleo makubwa kwenye sekta ya binafsi ambayo ndiyo uti wa mgongo wa jumuiya na nchi wanachama, tutaendelea mpaka hali za maisha za wananchi kwa ujumla iwe ya uchumi wa kuridhisha," alisema ofisa huyo.

Dola milioni tatu zimeelekezwa kwenye kudhibiti magonjwa ya milipuko, mradi ambao ulianza Machi, 2017 kama awamu ya kwanza na awamu ya pili Septemba 2019.

Alisema fedha hizo zinafanya kazi ya kujiandaa kitaalamu kwa magonjwa ya mlipuko ambayo kama yatatokea nchi zote wanachama ziwe tayari kuchukua hatua na pia kudhibiti ili kuepuka madhara ambayo mara nyingi hugharimu maisha ya wananchi.

Magonjwa haya lazima tuweke mkazo kwa kushirikiana na Wizara za Afya maana yanaondoa nguvu kazi inayohitajika kuzijenga nchi wanachama na Jumuiya kwa ujumla wake kichumi na maendeleo ya kila familia na taifa.

Naye Irene Lukassowitz, Meneja Mradi wa giz, alisema shirika lake zaidi ya kushirikiana na EAC kwenye sekta ya afya pia limeshawezesha kwenye ujasiriamali kwa nchi zote wanachama na hivyo kukuza vipato na

kupunguza changamoto za maisha zinazosababishwa na changamoto mbalimbali.

Alisema mpaka sasa wajasiriamali, wafanyabiashara na wenye viwanda wamefanikiwa kupata soko kubwa kwa maana ya nchi sita na kuuza bidhaa zao kwa urahisi, lakini kuongeza ajira kwa wananchi wa Jumuiya wanachama wa EAC.

Shirika la Maendeleo ya Ujerumani kwa niaba ya Wizara ya Maendeleo ya Kuichumi (BMZ) na Umoja wa Ulaya (AU) wamefanya mchango mkubwa kwenye jumuiya wanachama katika mipango mbalimbali kama kuongeza ubora wa biashara, maendeleo ya viwanda, uwekezaji, kujenga uwezo na elimu.

# Mashinji aanika barua ya msimamizi uchaguzi

**Na Hellen Mwango**

KATIBU Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Dk. Vincent Mashinji, anayekabiliwa na wenzake wanane na kesi ya uchochezi, amedai mahakamani kuwa barua ya msimamizi wa uchaguzi ilielekeza viapo na barua zitatolewa kwa wawakilishi wa mawakala.

Kadhalika, amedai kuwa kwa mujibu wa barua hiyo, wawakilishi wote baada ya kupokea nakala za viapo na barua watoe kwa mawakala.

Dk. Mashinji ambaye ni mshtakiwa wa sita alitoa madai hayo jana wakati akihojiwa na Jamhuri dhidi ya ushahidi wake mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba, anayesikiliza kesi hiyo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam. Akihojiwa na Wakili wa Serikali, Jacqueline Nyantori, mshtakiwa huyo alidai kuwa alianza kazi akiwa Katibu Mkuu Chadema Machi 12, 2016.

"Barua ya msimamizi wa uchaguzi Kinondoni, ilielekeza wawakilishi wa mawakala kuchukua nakala za viapo na barua kwa ajili ya kuwapatia mawakala," alidai Dk. Mashinji.

Alidai kuwa katika barua hiyo ya msimamizi, hakuona maelekezo ya kufuata nakala za barua kwa maandamano na kwamba aliekeleza mawakala watapewa.

Naye shahidi wa saba, Halima Mdee, alidai mahakamani kuwa Februari 16, 2018 alisafiri kutoka Dodoma mpaka jijini Dar es Salaam na kwamba alikwenda kwenye viunga vya kufungia kampeni Kinondoni.

Alidai kuwa kutokana na hali ya afya yake haikuwa nzuri, alipanda jukwaani akasalimia na kumtakia heri ya uchaguzi mgombea Salum Mwalimu.

Alidai kuwa aliondoka saa 11:15 kwenda nyumbani kwake Mbweni jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kujiandaa kwenda kwenye matibabu nchini Afrika ya Kusini.

"Nilisafiri kwenye matibabu lakini siku niliporudi niliwakuta maafande wananisubiri Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere katika ukumbi wa VIP, walinikamata wakanipeleka Kituo Kikuu cha Polisi," alidai Mdee. Alidai kuwa kuhusu kauli ya vichinjio, ilikuwa ina maana ya kwenda kupiga kura kuichagua Chadema na kumgalagaza Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais John Magufuli na wafuasi wake.

"Watu wa mjini tunafahamu kama kichinjio ni kadi ya kupigia kura kwa hiyo haina maana nyingine," alidai Mbunge huyo wa Kawe.

Mbali na Dk. Mashinji na Mdee washtakiwa wengine ni Mwenyekiti wa Chadema Freeman Mbowe, Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Salum Mwalimu; Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche; Mbunge wa Kibamba, John Mnyika; na Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya. Pia wamo Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa; na Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko.

Washtakiwa hao kwa pamoja wanakabiliwa na mashtaka 13, ikiwamo kula njama, kufanya mkusanyiko wenye ghasia, kuhamasisha hisia za chuki, kushawishi hali ya kutoridhika, uchochezi na kushawishi utendaji jinai kati ya Februari Mosi na 16, 2018, Dar es Salaam.

Kesi inaendelea leo kusikiliza ushahidi wa utetezi.




Mkuu wa Mauzo na Masoko wa GSM Group, Allan Chonjo (kulia), akihojiwa na Mtangazaji Samson Charles, kupitia kampeni ya Kibiashara Zaidi ya East Africa Television na East Africa Radio, ambapo mbali na bidhaa mbalimbali, ameeleza nafasi wanazotoa kwa wananchi kuwa mawakala wa kuuza jezi za Yanga. **PICHA: EATV**

# Mahakama yataka taarifa Magereza ofisa NIDA kutofika

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imeuagiza upande wa utetezi kufuatilia taarifa za ugonjwa wa mshtakiwa wa tatu ambaye ni Ofisa Usafirishaji wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), George Ntalima, kwa maofisa Magereza kutokanana na kutofika mahakamani mara ya pili.

Kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kusomwa maelezo ya awali mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Salum Ally.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Ladslaus Komanya, alidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya washtakiwa kusomewa maelezo ya awali.

Komanya alidai kwa kuwa mshtakiwa wa tatu hajafika mahakamani, Jamhuri inaomba wakili wa utetezi kuieleza mahakama mahali alipo mteja wake. Wakili wa utetezi, Tuli Kaundime, alidai mshtakiwa huyo ni mgonjwa anasumbuliwa na majipu yaliyosababisha homa kali ndiyo sababu ya kushindwa kufika mahakamani.

Alidai afya ya mshtakiwa huyo imedhorota na kuiomba mahakama kupanga tarehe nyingine ya kutajwa. Wakili Komanya alidai wakili wa mshtakiwa alitakiwa kutoa taarifa hiyo ikiambatanishwa na taarifa rasmi kutoka Magereza ili ijulikane kama anapatiwa matibabu au amepumzishwa.

Alidai kwa ajili ya kutenda haki kwa washtakiwa wengine, wakili huyo alete uthibitisho wa ugonjwa na sababu za kutompeleka mahakamani.

Akijibu hoja hiyo, Kaundime alidai mteja wake yupo mahabusu chini ya uangalizi wa Magereza hivyo, si sahihi kupeleka taarifa za ugonjwa au kueleza alipo mshtakiwa wakati wanafahamu yupo kwenye mikono salama ya Magereza.

Alidai wanaopaswa kutoa taarifa hiyo ni Magereza.

Hakimu Ally alisema ni wajibu wa upande wa mashtaka kupata taarifa za mshtakiwa huyo kutoka Magereza.

Hata hivyo, aliutaka upande wa mashtaka kuwasiliana na Magereza ili kupata taarifa za mshtakiwa huyo na kuieleza mahakama maendeleo yake.

Hakimu Ally aliahirisha kesi hiyo hadi Desemba 19, mwaka huu, kwa ajili ya kuwasomea washtakiwa maelezo ya awali.

Wengine kwenye kesi hiyo ya uhujumu uchumi ni aliyekuwa Mkurugenzi wa NIDA, Dickson Maimu, Meneja Biashara wa NIDA, Avelin Momburi; Ofisa Usafirishaji, George Ntalima; Xavery Silverius maarufu kama Silverius Kayombo na Mkurugenzi wa Sheria NIDA, Sabina Raymond.

Maimu na wenzake wanakabiliwa na mashtaka 55 yakiwamo ya kutakatisha fedha na kuisababishia serikali hasara ya Sh. bilioni 1.175.

Kati ya mashtaka mapya 55 waliyosomewa washtakiwa hao, yapo ya kuisababishia serikali hasara ya Sh. bilioni 1.175 ; utakatishaji fedha; kughushi; kuwasilisha nyaraka za uongo ili kumdanganya mwajiri wao; kujipatia fedha kwa njia za udanganyifu; matumizi mabaya ya madaraka na kuongoza genge la uhalifu.

Hata hivyo, Maimu, Ntalima na Silverius wamerudishwa rumande kutokana na mashtaka yao kutokuwa na dhamana huku Momburi na Raymond wakiwa nje kwa dhamana.



Mkazi wa Jiji la Dar es Salaam akiokota tiketi kwenye droo ya maji ya Kilimanjaro iliyofanyika jijini humo jana, ambapo walipatikana washindi wa bodaboda, televisheni na katoni za maji. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Serikali yarekebisha kanuni uwekezaji, gharama zafyekwa

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Sima, amesema serikali imefanya mapitio ya Kanuni ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira ili kurahisha uwekezaji nchi.

Akizungumza na wafanyabiashara na wawekezaji katika mkutano wa kushauriana baina yao na serikali mkoani Morogoro juzi, Sima alisema gharama za kulipia vibali zimepungua na idadi ya siku pia imepungua kutoka siku 145 za awali hadi siku 95.

"Ndugu zangu, marekebisho haya yote yanayofanywa na serikali, yanalenga kurahisisha mchakato wa tathmini ya athari kwa mazingira na kurahisisha uwekezaji nchini.

"Mfano, awali gharama kwa vituo vya mafuta zilikuwa zaidi ya Sh. milioni 10 lakini kwa sasa gharama hizi zimepungua hadi kufikia Sh. milioni nne na nyingine Sh. milioni mbili," alifafanua.

Naibu Waziri huyo alisema ofisi yake pia inaandaa kanuni za wataalamu elekezi wa mazingira ili kurahisisha uwekezaji kwa kuwa miradi yote kwa kuwa ni lazima ipate cheti kutoka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

"Tangu tumefanya mapitio ya kanuni zetu, malalamiko kutoka kwa wawekezaji yamepungua kwa kiasi kikubwa sana," alisema. Sima alitumia nafasi hiyo kuwakumbusha washiriki wa mkutano huo kuwa mabadiliko ya tabianchi ni tatizo kubwa duniani.

Alitoa rai kwa umma wa Watanzania kupanda miti kwa wingi kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi.

Aliwaagiza wawekezaji, hasa wenye viwanda kuhakikisha wanaanzisha vitalu vya miche katika maeneo yao na kusisitiza kuwa ukaguzi wa masuala ya mazingira katika maeneo yao utaanzia hapo.

Mkutano huu ulilenga kusikiliza na kutatua matatizo ya uwekezaji na utaendelea katika mikoa ya Pwani na Dar es Salaam. Mawaziri 13 na manaibu wao wanashiriki mkutano huu.

# Jela maisha kunajisi mtoto

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

MAHAKAMA ya Wilaya Mkoa wa Kigoma, imemhukumu mkazi wa Kijiji cha Kalenge Wilaya ya Uvinza, Dastan Elia (40), kutumikia kifungo cha maisha jela kwa kumnajisi mtoto mwenye umri wa mwaka mmoja na miezi saba.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu wa Mahakama hiyo, Eva Mushi, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo pasipokuacha shaka.

Hakimu Mushi alisema mahakama inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na kwa watu wengine wenye tabia ya kikatili kwa watoto kama yake.

Alisema upande wa mashtaka ulipeleka mashahidi wanane pamoja na vielelezo viwili ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo.

Aidha, alisema Julai 5 mwaka huu majira ya asubuhi katika kijiji cha Kalenge Wilaya ya Uvinza Mkoa wa Kigoma, mshtakiwa alimbaka mtoto huyo na kumsababishia maumivu sehemu zake za siri.

Alisema siku ya tukio hilo watoto walikuwa wakicheza mshtakiwa huyo aliwafuata na kuwafukuza, na baada ya kuwafukuza walitawanyika na baada ya kutawanyika mshtakiwa aliingia ndani ya nyumba na kumfanyia kutendo hicho cha kikatili mtoto huyo msichana.

Hakimu huyo alisema wakati mshtakiwa

INAENDELEA UK. 8

# Mbinga wahimizwa kuanzisha viwanda

**Na Felix Andrew**

SERIKALI wilayani Mbinga Mkoa wa Ruvuma, imeeleza kwa sasa itatoa kipaumbele kwa waombaji wa mikopo wenye mwelekeo wa kuanzisha viwanda ili kujenga uchumi wa viwanda na kuongeza ajira .

Kauli hiyo ilitolewa na Mkuu wa wilaya hiyo, Cosmas Nshenye, wakati wa ufunguzi wa semina ya wazalishaji, wasindikaji na wauzaji wa bidhaa za chakula na vipodozi. Nshenye alisema mikopo hiyo inayotolewa na Halmashauri ya Wilaya kwa makundi ya vijana na wanawake haina riba, na kwa sasa watakaopewa kipaumbele ni wale ambao wameitikia wito wa kuanzisha viwanda vya kusaga kahawa, watengenezaji wa batiki, wazalishaji wa sembe na bidhaa nyingine mbalimbali.

"Walioitikia wito wa kujenga uchumi wa viwanda kwa kuanzisha viwanda tunawapongeza kwani tuna imani ajira zitaongezeka na Kauli ya 'Mbinga Mbingun' itazidi kujidhihirisha kutokana na mafaniko yatakayotokana na viwanda," alisisitiza. Alisema pamoja na jitihada hizo za wazalishaji za kuanzisha viwanda, pia wazalishaji wanapaswa kuzalisha bidhaa kwa kuzingatia viwango ili kuwa na uhakika wa ubora na bidhaa wanazozizalisha pamoja na uhakika wa soko ndani na nje ya wilaya hiyo.

Alisema fursa ya elimu inayotolewa na Shirika la Viwango la Taifa (TBS) ni muhimu kwa wazalishaji kuizingatia kwani mbali na elimu hiyo inayotolewa bure, pia wajasiriamali hupatiwa huduma ya uthibitishaji wa ubora wa bidhaa bure kwa miaka mitatu ya mwanzo.

Akizungumzia kundi maalumu la wasindikaji wa pombe za kienyeji, ameiomba TBS kuangalia namna ya kuwawezesha wasindikaji pombe za kienyeji wanafikia viwango vinavyokubalika ili bidhaa zao zikidhi matakwa ya viwango na kukubalika katika masoko ya ndani na nje ya nchi hususan katika soko la Afrika Mashariki.

Awali Kaimu Mkurugenzi wa Udhibiti Ubora na Meneja wa Utafiti na Mafunzo, Hamisi Sudi, akimkaribisha Mkuu wa Wilaya kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Athuman Ngenya, alisema, Shirika litaendelea kutoa elimu ya viwango kwa Watanzania wote lengo kuu likiwa ni kuwa na uelewa wa pamoja wa masuala ya viwango na ubora wa bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi na zile zinaingizwa kutoka nje nchi.

Naye mkuu wa Wilaya ya Songea, Palolet Mgema, akifungua semina, Songea alisema imefanyika katika kipindi muafaka kwani wafanyabiashara na wazalishaji walikuwa wakiisubiri kwa hamu ili kujua ni taratibu zipi za kufuatwa baada ya mabadiliko ya Sheria ya fedha ya Mwaka 2019.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# WB, serikali zina nafasi kuondoa umaskini huu

**LICHA** ya jitihada nyingi kufanyika kuondoa umaskini, wadau wa maendeleo wakiwamo Benki ya Dunia (WB) wanaeleza kuwa umaskini ni changamoto nchini na kwamba idadi ya watu hao inaongezeka.

Ripoti ya chombo hicho cha fedha duniani inayotolewa wiki hii jijini Dar es Salaam, inasema kuwa maskini wameongezeka kutoka milioni 12.3 mwaka 2012 hadi kufikia milioni 14 mwaka jana.

Si habari njema lakini ni jambo linalolipa taifa changamoto ya kujitahidi zaidi kuondoa umaskini ambao kwa miaka mingi ni maradhi yanayolitesa taifa tangu uhuru mwaka 1961 hadi leo takribani miaka 58.

Pamoja na taarifa hiyo , ukweli ni kwamba serikali imeweka mipango na mikakati kadhaa ya kuondoa umaskini ili kila Mtanzania aweze kumudu maisha yake ikiwa ni pamoja na kuweka mikopo ya kinamama, vijana na watu wenye ulemavu.

Kwa mfano, inawasomesha watoto wote bure kuanzia elimumsingi inayojumuisha pia sekondari.

Aidha, imeanzisha mfumo wa kutumia mfuko maalumu kuzisaidia kaya masikini kwa kuzipatia ruzuku na huduma nyingine kazi inayofanywa kupitia Mfuko wa Taifa wa Maeneleo ya Jamii (Tasaf). Lakini, si hivyo tu, kuna mpango wa kuwasaidia watu wenye ulemavu na mahitaji maalumu kusoma. Katika mchakato huo wa kusoma hadi kufika chuo kikuu serikali imeeleza kuwa wapo watakaosamehewa kulipa mikopo waliyopewa ili kuwapunguzia mzigo wa kulipa madeni. Nia ni kuendelea kuwawezesha kwa kila namna ili wamudu maisha yao.

Mambo mengi yanayofanywa hayamaanishi kuwa umaskini utaondoka kwa siku moja. Ni mchakato unaohitaji ushirikishwaji na ushirikiano baina ya wadau hao wa maendeleo na serikali.

Mikakati ya kuondoa umaskini inahusisha kujenga uchumi ikiwamo miundombinu, viwanda na miradi mingine mingi kama kuendeleza kilimo na ufugaji , uchimbaji madini na kuongezea thamani bidhaa zinazozalishwa nchini.

Pamoja na kusikia ripoti ya Benki ya Dunia ni wakati pia wa wadau hao wa maendeleo kuongeza mchango wao kusaidia kupunguza umaskini kwa kufanikisha juhudi za kuanzisha viwanda vya kusindika mazao na kuzalisha bidhaa zilizoongezewa thamani vijijini waliko Watanzania wengi.

Kwa kuliona hilo tunaoimba WB kusaidia utafiti unaowezesha kupatikana teknolojia rahisi na za gharama nafuu ili kutumiwa kuondoa umaskini vijijini.

Teknolojia hizo tunaamini zitafanikisha uzalishaji, usindikaji na uhifadhi wa mazao vijijini ambako suala la kujenga vihenge vya kutunza chakula kwa utaalamu ni tatizo linalozikabili jamii nyingi.

Ni wazi kuwa WB ina mchango kwenye maendeleo ya nchi, tunajua kuwa ina nafasi ya kushirikiana zaidi na serikali kwenye kuwatambua watu maskini zaidi walioko sehemu mbalimbali na kushirikiana na serikali kufanya utafiti wa kuibua mikakati ili waondokane na umaskini huo.

Tunaona kuwa ni wakati wa kuibua mikakati ya kuwekeza zaidi vijijini na kuboresha maisha ya sehemu hizo ili kupunguza idadi ya watu wanaokimbilia mijini kwa kuwa vijijini au mashambani kuna maisha duni. Hapo ndipo tunapoishauri WB na serikali kuona uwezekano wa kuwa na vyuo vya ufundi maalumu kwa ajili ya kusaidia makundi mbalimbali ya watu wanaoishi vijijini ili waweze kumudu maisha yao na kupunguza umaskini.

Vyuo hivyo vinaweza kuanzishwa baada ya kutambua mahitaji watu wa maeneo hayo pamoja na rasilimali zao ili kuwafunza waweze kuzitumia kujenga uchumi na kuboresha maisha yao.

Kwa muktadha huo kuwasaidia kielimu na kiteknolojia kutakuwa na manufaa zaidi kutokana na uanzishwaji wa viwanda vitakavyoajiri watu wanaoishi vijijini na kuzalisha bidhaa kwa ajili ya matumizi yao na kuinua uchumi wao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# RC Malima 'komaa nao' tu hadi waziteme

Na Sabato Kasika

**MKUU** wa Mkoa wa Mara, Adam Malima amewapa siku saba viongozi wa vyama zaidi ya 85 vya ushirika, wanaotuhumiwa kufuja fedha zaidi ya Sh. milioni 105 kuzirejesha mara moja.

Alitoa agizo hilo baada ya kupokea ripoti kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) kuhusu kuwapo ufujaji wa fedha zaidi ya Sh 105 milioni katika Amcos, zaidi ya 85 mkoani mwake na kumfanya acharuke na kuagiza wahusika wazirejeshe.

Malima anasema, vitendo hivyo vya ubadhirifu na ufujaji wa fedha za ushirika vinavyofanywa na viongozi vinarudisha nyuma juhudi za serikali, katika kumkomboa kiuchumi mwananchi wa kawaida.

Anasema, ushirika ukitumika vizuri utakuwa ni mkombozi mkubwa wa wakulima, na kwamba serikali haiwezi kuwavumilia viongozi wa aina hiyo, ambao wanatumia jasho la wananchi kwa manufaa yao.

"Lengo kuu la ushirika ni kuwasaidia na kuwainua wanachama kupitia kwenye ushirika baada ya mauzo ya mazao na bidhaa zao na michango mbalimbali kwa mujibu wa makubaliano yao," anasema Malima.

Mkuu huyo anasema, anafanya jitihada za kuimarisha sekta ya ushirika, ili iwe mojawapo ya zile zitakazosaidia kuleta mapinduzi ya kiuchumi, akianzia kuimarisha kilimo cha pamba na kahawa, kisha uvuvi na madini.

Hivyo, anasema hawezi kukubali kuona kuna watu wanamkwamisha wakiwamo hao wanaotuhumiwa kufuja kiasi hicho cha fedha, amewapa siku saba kuhakikisha kwamba wanakirejesha mara moja.

Mkuu huyo wa mkoa amechukua hatua hiyo huku tayari kukiwa na wito wa kuimarisha udhibiti wa ndani katika vyama vya ushirika, ili kuondoa wizi unaofanywa na baadhi ya viongozi na watendaji wa vyama hivyo.

Wito huo ulitolewa Oktoba mwaka huu na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO), alipowasilisha ripoti ya ukaguzi wa vyama hivyo kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Ripoti hiyo ilikabidhiwa kwa Mwenyekiti wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dk. Titus Kamani, jijini Dodoma na kisha Makamishna wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania wakaijadili.

Katika mjadala wao, nao wakashauri COASCO na TCDC kuboresha ushirikiano uliopo kwa ajili ya udhibiti katika vyama vya ushirika ili kuondoa tatizo la wizi na ufujaji wa fedha kwenye vyama hivyo.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Brigedia Jenerali John Mbungo, baada ya kupokea ripoti hiyo, alitangaza vita kwa wanaotafuna fedha hizo.

Alizitaka taasisi na mashirika yote yaliyotafuna fedha za vyama vya msingi vya ushirika kuzirudisha haraka iwezekanavyo na kwamba wasipofanya hivyo, watafikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Baadaye aliujulisha umma wa Watanzania kupitia vyombo vya habari, kuwa viongozi 52 wa vyama vya ushirika mkoani Lindi walinaswa kwa kushindwa kuwalipa wakulima wa korosho Sh. milioni 436.

Hatua zinazochukuliwa na viongozi mbalimbali akiwamo Mkuu wa Mkoa wa Mara, kwa ajili ya kukabiliana na tatizo la ufujaji wa fedha za Amcos ni za kuungwa mkono na wapenda maendeleo.

Ninasema hivyo, sababu moja ya vyanzo vya migogoro katika vyama vya ushirika kwenye maeneo mbalimbali hapa nchini, ni ufujaji wa fedha unaofanywa na baadhi ya viongozi wasio waaminifu.

Hivyo, RC Malima aendelee kuwakomalia hao viongozi wanaotuhumiwa kufuja fedha zaidi ya Sh. milioni 105 za vyama vya ushirika, ili hatimaye wazirejeshe mara moja kama alivyoagiza.

Ushirika hauwezi kuwa na maana kama wanachama wataendelea kuibiwa na viongozi wao, ambao kwa namna moja au nyingine wanaweza kuharibu dhana ya ushirika ambayo inalenga kumkomboa mkulima. Kimsingi ni kwamba wanaotuhumiwa kufanya ufujaji wa fedha za vyama watambue kuwa wanavuruga umoja na mshikamano wa wanachama kwa maslahi yao binafsi, hivyo ni muhimu wakaepukwa.

Ushirika hauwezi kuwa na maana kama wanachama wataendelea kuibiwa na viongozi wao, ambao kwa namna moja au nyingine wanaweza kuharibu dhana ya ushirika, ambayo lengo lake ni kumkomboa mkulima.

Ikumbukwe kuwa ushirika ni kwa maendeleo ya wanachama, chama na hata taifa kwa ujumla, hivyo wanaouvuruga kwa njia yoyote ile, hawana budi kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

# Wazee kimila waungana kutokomeza mila potofu

**Na Waandishi Wetu,** MWANZA

WAZEE wa kimila 225 kutoka mikoa tisa nchini wameazimia kuunda mtandao wa pamoja utakaowawezesha kutokomeza mila potofu zinazochochea ongezeko la vitendo vya ukatili.

Walitoa azimio hilo katika mkutano uliowakutanisha wazee kutoka mikoa ya Mwanza, Tabora, Shinyanga, Geita, Kagera, Mara na Simiyu, kujadiliana namna watakavyoweza kuondoa matukio ya ukatili, ndoa na mimba za utotoni katika jamii.

Akizungumza na waandishi wa habari, jijini Mwanza ambako mkutano huo ulifanyika, Chifu Mifungo Charles, kutoka mkoani Geita alisema, ndoa za utotoni ni tatizo na haliendani na karne ya 21 hivyo wameungana ili kutoa elimu itakayosaidia kuachana na mila potofu.

Alisema, changamoto watakazozifanyia kazi ni kumaliza ndoa za utotoni, wanawake kupewa haki ya kumiliki mirathi pamoja na kuondokana na mila ya utakasaji kwa wanawake, kitendo kinachoaminiwa kuwa ni kuondoa mikosi mke au mume anapofariki dunia jambo lililokuwa likisababisha magonjwa mbalimbali hasa yasiyokuwa na tiba.

Naye Kineno Maporu kutoka Tabora alisema, vijana wanapaswa kubadilika na kuachana na utamaduni wa nje bali waendelee kuishi kwa kufuata mila zao nzuri na zenye kuleta tija japokuwa umaskini ndiyo chanzo kikubwa cha vijana kubadilika, lakini ushirikiano wao na serikali unahitajika ili kulijenga suala hilo na kuondokana na vitendo vyote vya ukatili.

"Malezi ni jambo la muhimu kuliko yote hasa kwa mtoto wa kike wakati mwingine sisi wazazi ndio tunachangia..." alisema Maporu.

Naye Lucy Tesha, kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa UN Women, kitengo cha kutokomeza ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake hususani watoto wa kike, akibainisha maazimio hayo yaliyowekwa na wazee wa kimila alisema, moja ya mkakati waliopanga ni kuunda mtandao wa pamoja kwa mikoa tisa na badala ya kuitwa wazee wa mila waitwe wazee mashuhuri wakiwashirikisha pia na vijana katika mapambano hayo.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT), Elirehema Kaaya, alisema jumuiya yao inafanya kazi halmashauri 185 nchini, hivyo viongozi wa mila wapo ngazi ya chini kutunza maadili yenye mchango kwa jamii na taifa.

Alisema japo kuwa sheria zipo kumaliza tatizo la ndoa za utotoni na ukeketaji itakuwa jambo gumu endapo wazee hao hawatashirikishwa, jambo la msingi ni kutoa elimu kwa jamii ili watambue athari zitokanazo na matendo ya kikatili.

■**Imeandikwa na Elizabeth Faustine na Neema Emmanuel, MWANZA**

# Hatima ya Malinzi kujulikana Desemba 11

**Na Hellen Mwango**

HATIMA ya kurudi uraiani au la kwa Rais wa zamani wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Jamal Malinzi na wenzake watatu wanaokabiliwa mashtaka 20 yakiwamo ya kula njama, kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na utakatishaji wa fedha wa USD 173,335 itajulikana Desemba 11, mwaka huu itakaposomwa hukumu yao.

Kesi hiyo imepigwa kalenda jana na Hakimu Mkazi Mwandamizi, Janeth Mtega, baada ya hakimu aliyesikiliza kesi hiyo kuhamishiwa kituo kingine cha kazi.

Kesi hiyo ilipangwa kusomwa hukumu jana lakini, Hakimu Mtega alisema kwamba bado haijawa tayari mpaka wiki ijayo Desemba 11, mwaka huu.

Awali, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kusikilizwa hukumu na upande wa Jamhuri ulikuwa tayari.

Hakimu Mtega alisema hukumu hiyo itasomwa wiki ijayo washtakiwa wataendelea kukaa mahabusu na mshtakiwa aliye nje, dhamana yake inaendelea.

Mapema mahakamani hapo upande wa Jamhuri ukiongozwa na Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Leonard Swai, uliita mashahidi 15 na vielelezo tisa kuthibitisha kesi hiyo na utetezi wa nne kupangua tuhuma hizo.

Mbali na Malinzi, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni, aliyekuwa Katibu wa TFF, Selestine Mwesigwa, Mhasibu wa TFF, Nsiande Mwanga na Karani Flora Rauya

Katika kesi hiyo mashahidi 15 wa upande wa mashtaka walitoa ushahidi na tayari Malinzi ameanza kujitetea.

Malinzi, Mwesigwa na Nsiande wapo rumande kwa kukabiliwa na mashtaka ya utakatishaji wa fedha kuwa miongoni mwa mashtaka ambayo kwa mujibu wa sheria hayana dhamana huku Flora akiwa nje kwa dhamana.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya rangi ya Goldstar, K Srinivasan (kushoto), akipongezana na Mkurugenzi wa Kampuni JK Cement Ltd, Amit Kothari baada ya kusaini makubaliano ya kuungana katika bidhaa zao wakati wa mkutano uliofanyika jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkuu wa Mauzo na Masoko wa Goldstar, Pushpendra Singh Khamis. **PICHA:MPIGAPICHA WETU**

# Wawekezaji wahakikishiwa kuwahishiwa vibali mazingira

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

Serikali imesema kwamba Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira(NEMC) litakuwa taasisi muhimu katika kuchochea uwekezaji nchini kwa kutoa vibali kwa wakati na kuwa mshauri elekezi kwa wawekezaji.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Musa Sima, wakati akijibu hoja za wawekezaji, wafanyabiashara na watendaji wa serikali katika mkutano uliofanyika hapa kujadili uboreshaji wa mazingiria ya uwekezaji na ufanyaji biashara nchini,

Waziri Sima alisifu kazi kubwa inayofanywa na NEMC katika kulinda na kuhifadhi mazingira ili yasiathiriwe na shughuli za uwekezaji, lakini alilitaka baraza kuwa mshauri elekezi na kutoa vibali vya kulinda mazingira kwa wakati ili wawekezaji wasihangaike na waamini na msimamo wa serikali juu ya uwekezaji na kufanya biashara nchini.

Aliwakumbusha wajumbe kwamba usimamizi na uhifadhi wa mazingira vinafanywa kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya 2004 na Kanuni zake, na kwamba uwekezaji na biashara vikifanywa kwa utaratibu mzuri vinaibua na kuongeza ajira na mapato ya serikali kupitia kodi mbalimbali.

Aliwashukuru wawekezaji na wafanyabiashara kwa kuelewa dhamira ya serikali na akawataka wazingatie sheria ili kufanyakazi zao kwa amani na salama na kuwaomba wapande na kuwa na vitalu vya miti katika maeneo yao.

"Jukumu la Ofisi ya Makamu wa Rais ni kuhakikisha sheria za nchi juu ya mazingira zinatekelezeka kwa usimamizi wa NEMC. Baraza ndilo linalohakikisha shughuli za uwekezaji na biashara nchini zinafanyika pasipo kuathiri mazingira," aliwaambia wajumbe na kuongeza kwamba katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, serikali imeliruhusu baraza kutoa vibali vya muda mfupi vya kulinda mazingira vinavyompa mwekezaji fursa kuanza shughuli za uwekezaji wakati taratibu nyingine zikiendelea kufanyiwa kazi.

Alilitaka baraza litoe vibali hivyo kati ya siku 7 hadi 14 kutegemea kutegemea ukamilika kwa nyaraka zinazohitaji.

Awali nyaraka hizo zilikuwa zinatolewa na Waziri mwenye dhamana ya mazingira. "Tunaamini maboresho yanayofanywa yatachochea kasi ya uwekezaji nchini na kufanya azma ya Serikali ya awamu ya tano ya kujenga uchumi wa kati na viwanda itekelezeke kwa vitendo kutokana na wepesi katika uwekezaji na kufanya biashara."

Alikumbusha kwamba wakati mwingine wawekezaji wanahangaika kutoka na matumizi tofauti ya kisheria ya ardhi na kuitaka NEMC ifanye mawasiliano ya ndani na taasisi husika ili kumpunguzia adha mwekezaji.

"Maombi mengi ya wawekezaji wakati mwingine yanakwama kutokana na sababu za matumizi ya ardhi kuwa tofauti na anachoomba mwekezaji. Suala hili linahusu sekta ya umma hivyo ni lazima kufanya mawasiliano ya ndani ili matumizi yabadilishwe pasipo kumhangaisha mwekezaji."

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare, amesema mkoa huo una ardhi nzuri ya kilimo, madini na vivutio vya utalii na kuwaalika wawekezaji na wafanyabiashara kutumia fursa zilizo katika mkoa huo.

# Mikataba kukaribisha uwekezaji yasainiwa

**Na Romana Mallya**

MIKATABA miwili mikubwa iliyolenga kuvutia uwekezaji, ufanyaji biashara na kukaribisha teknolojia mpya Tanzania kupitia kampuni 9,100 za India, imesainiwa jijini Dar es Salaam.

Mikataba hiyo ilisainiwa jana kati ya Jumuiya ya Wafanyabiashara wa India na Tanzania mbele ya Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa.

Mkataba wa kwanza wa makubaliano uliosainiwa ulikuwa ni kati ya Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) na Jumuiya hiyo ya wafanyabiashara wa India.

Mwingine ulikuwa ni kati ya jumuiya hiyo ya Wafanyabiashara wa India yenye kampuni 9100 na Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) kupitia Baraza la Biashara.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Waziri Bashungwa alisema kwa sababu Rais John Magufuli ndiye mwenyekiti wa SADC, aliomba ujumbe wa jumuiya hiyo ya wafanyabiashara wa India uje Tanzania kwa ajili ya shughuli hiyo.

"Leo, mikataba ya makubaliano ya kufanya biashara kati ya India na Tanzania imesaidiwa, hivyo tumeweka mazingira ya kuwekezaji na ufanyaji biashara na kukaribisha teknolojia kutoka kwenye nchi ambayo imeshapiga hatua," alisema.

Alisema Tanzania imewekeza kwenye miundombinu, umeme, barabara, reli na sekta ya anga ambapo kwa sasa ndege za Shirika la Ndege la Tanzania zinakwenda nchini India.

Alisema kwa sasa wanachotafuta ni kuongeza mnyororo wa thamani kwenye bidhaa na kuvutia uwekezaji kwenye viwanda vya pamba, korosho na viungo ambapo India ndilo soko kubwa.

Kaimu Mwenyekiti wa TPSF na Kaimu Mwenyekiti wa Baraza la Biashara la SADC, Angelina Ngalula, alisema kwenye makubaliano hayo kikubwa walicholenga ni kubadilishana taarifa za kibiashara, kiuchumi na kimasoko kwa wafanyabiashara wa nchi hizo.

Pia alisema makubaliano hayo yamelenga kufungua milango ambapo kampuni za pande zote mbili zitaweza kufikiana na kufanya biashara au uwekezaji wa pamoja.

"Tunapozungumzia uwekezaji wenzetu wanaangalia soko la SADC ambalo Rais Magufuli ndiye mwenyekiti wake, ukiangalia kijiografia yeyote anayetaka kuingia kwenye soko hili nchi ya kwanza atakayofikiria ni Tanzania.

"Ataifikiria Tanzania kwa sababu ni nchi pekee Afrika Mashariki iliyopo SADC, na soko la jumuiya hii lina zaidi ya watu milioni 500 na zaidi ya watu milioni 100 Afrika Mashariki, tumewaeleza wakitaka kufika SADC kituo ni Tanzania ili waweze kunufaika," alisema.

Naye Balozi wa India nchini, Sanjiv Kohli, alisema serikali yao itaendelea kuboresha ushirikiano uliopo kati ya nchi hizo mbili ikiwamo biashara, elimu na afya.

Mjumbe wa jumuiya ya wafanyabiashara wa India, Manikantan Rajendran, alisema raia wa India 50,000 waishio Tanzania ni ushahidi tosha wa ushirikiano mzuri uliopo baina ya nchi hizo.

"Kwa mwaka 2018/19 biashara kati ya India na Tanzania ilifikia kiasi cha Dola za Marekani bilioni 2.6," alisema.



Meneja Uhusiano wa Idara ya Biashara ya Kadi ya Benki ya NMB, Yusuph Achayo (kulia), akimkabidhi zawadi ya fedha taslimu Sh. 50,000/- dereva wa bodaboda wa kituo cha Ubungo Plaza, Abubakar Mohamed, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kuibuka mshindi kwa kufanya miamala mingi kwa kulipwa na wateja wake kupitia huduma mpya ya MastaBoda QR Code. Kushoto ni Mwenyekiti wa Chama cha Waendesha Bodaboda Mkoa wa Dar es Salaam, Michael Massawe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wataja mbinu kuteka soko

**Na Mwandishi Wetu**

MENEJA Viwango wa Wakala wa Vipimo nchini (WMA), Jared Mushi, amewataka wazalishaji wa bidhaa mbalimbali kuutumia wakala huo ili kujihakikishia soko na kukuza biashara zao.

Aliyasema hayo jana kwenye Viwanja vya Maonyesho ya Biashara vya Mwalimu Nyerere jijini Dar es Salaam, akieleza kuwa faida mojawapo ya kutumia wakala huo ni kupata bidhaa kwa usahihi kulingana na thamani inayotolewa.

Alisema wakala huyo una jukumu la kumlinda mlaji na umma kwa ujumla kupitia uhakiki na udhibiti wa vipimo vinavyotumika katika biashara na huduma nyingine zikiwamo za afya, usalama na mazingira.

"Kazi kubwa ya WMA ni kusimamia ufungashaji, ushauri wa kitaalamu kwa wanaojihusisha na utengenezaji, uundaji, uagizaji wa vipimo mbalimbali katika sekta ya biashara, afya, usalama na mazingira na kuwa kiungo kati ya taifa letu na taasisi za kikanda na kimataifa katika masuala ya vipimo.

"Wito wangu kwa wazalishaji wa bidhaa kote nchini, wawasiliane na WMA kabla ya kuanza na baada ya kuanza uzalishaji kwa sababu vipimo vikiwa sahihi, itatangaza biashara zao," alisema. Kuhusu maonyesho hayo yaliyoanza jana, meneja huyo alisema yatasaidia wazalishaji na umma kwa ujumla kupata elimu zaidi na kutambua kazi zinazofanywa na WMA ili kuzuia upimaji mbaya na hasara.

Mushi alisema WMA iko mbioni kuanza kupima mita za umeme ambazo awali hawakuzipima kutokana na kutokuwa na vifaa vya kufanya kazi hiyo.

## Tahadhari mvua ya kimbunga mikoa 17

INATOKA UK. 3

Alisema hali ya maeneo ya makazi kuzungukwa na maji pia inatarajiwa kwa mikoa mingine iliyotajwa, hivyo shughuli za kiuchumi huenda zikasimama.

Mbuya, alisema kwa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani, vipindi vya mvua kubwa vinatarajiwa zaidi kutokana na kuwapo kwa dalili ya vimbunga pacha katika Bahari ya Hindi.

"Kuna mgandamizo mdogo wa hewa unaoendelea kuimarika vinavyotarajia kutengeneza vimbunga pacha magharibi mwa Bahari ya Hindi na kuathiri mifumo ya hali ya hewa," alisema Mbuya. Aliongeza kuwa vimbunga hivyo vinaonekana katika Pwani ya Somalia na Kaskazini Magharibi mwa kisiwa cha Madagascar na kusababisha ongezeko la mvua kubwa katika Pwani ya kaskazini ya nchi yetu katika siku ya jana na leo.

Kutokana na matarajio hayo, TMA imetoa tahadhari kwa wananchi na Mamlaka husika juu ya athari zinazoweza kutokea na kuwataka wananchi kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa wanazozitoa.

## Jela maisha kunajisi mtoto

INATOKA UK. 5

huyo anaendelea kumfanyia kitendo hicho, alifika dada wa mtoto huyo mwenye umri wa miaka 5 na kushuhudia, na baada kuona alikimbia kwa jirani na kuwapa taarifa.

Alisema jirani aliwaita majirani wengine na kwenda kumchukua mtoto huyo kumpeleka kituo cha Polisi Kazuramimba na walipofika walipewa fomu ya PF3 kisha kumpeleka Zahanati ya Kazuramimba na daktari alipomfanyia uchunguzi, alibaini kufanyiwa ukatili huo.

Hakimu Mushi alisema alisikiliza kesi hiyo pande zote na kugundua kuwa upande wa mshtaka umethibitisha kosa hilo pasipokuacha shaka, hivyo mshtakiwa umetiwa hatiani, na kumpa fursa mshtakiwa kujitetea. Mshtakiwa alijitetea kuwa anaomba mahakama hiyo impunguzie adhabu kwa kuwa ni kosa lake la kwanza.

Hakimu Mushi alitupilia mbali utetezi huo na kusema kitendo alichokifanya ni cha kikatili, hivyo kumhukumu kwenda gerezani maisha.

Awali akisoma hati ya Mashtaka Wakili wa Serikali, Edina Makala, alidai Julai 5, mwaka huu majira ya asubuhi katika kijiji cha Kalenge Wilaya ya Uvinza, mshtakiwa alimnajisi mtoto huyo.

HABARI KITAIFA

# Biteko aanika vishawishi kwa watumishi madini

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Madini, Doto Biteko, amesema kuna vishawishi na majaribu mengi kwa watumishi wa Wizara ya Madini na taasisi chini ya wizara kutokana na wadau wake wengi kuwa ni watu wenye fedha.

Amesema ni rahisi kuwashawishi kwa rushwa na kusababisha mtumishi kufanya uamuzi usio na maadili na kwamba wako watu wanaowachonganisha watumishi wake na viongozi kwa kumpelekea taarifa za uongo na majungu.

Biteko alisema hayo juzi kwenye ofisi za Tume ya Madini jijini Dodoma, alipokuwa akiongea na wafanyakazi wapya 160 wa Tume ya Madini walioajiriwa hivi karibuni huku akiwataka kuzingatia maadili na kuepuka rushwa.

"Wengi wenu ni vijana, mna ari ya kufanya kazi na mna ndoto zenu. Nendeni mkafanye kazi kwa bidii kwa kuzingatia maadili ya kazi na kujituma. Rushwa ni hatari sana, wapo watakaowajaribu kwa kila namna. Naomba nendeni mkayaepuke hayo majaribu," alisema.

Biteko aliipongeza Tume ya Madini kwa kazi kubwa wanayoifanya kipekee kwa uongozi wa juu na wafanyakazi kwa ujumla.

"Nakushukuru sana Prof. Manya (Mtendaji Mkuu wa Tume ya Madini), unafanya kazi nzuri sana pamoja na mwenyekiti wenu, Prof. Idris Kikula ambaye hapa hayupo. hakika mnanisaidia sana. Hata muda wenu ukiisha nitamwomba Mheshimiwa Rais awabakize kwa sababu bado mnahitajika sana katika wizara hii.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini, Prof. Simon Msanjila, aliwaambia watumishi hao wapya kuwa wana wajibu mkubwa wa kuongeza tija katika tume na wizara kwa ujumla, hivyo kila mmoja akajitume kwa taaluma aliyoajiriwa nayo.

"Sina shaka juu yenu, ni vijana, mna nguvu na mna ari. Ni imani yangu kuwa mtakuwa chachu katika utendaji nzuri wa kazi za wizara kwa ujumla. Nendeni mkawasikilize wasimamizi wenu, msisikilize watu watakaowapotosha. Kafanyeni mnachopangiwa kufanya" alisema Prof. Msanjila.

Biteko na Prof. Msanjila walimshukuru Rais John Magufuli kwa kuwapatia vitendea kazi mbalimbali yakiwamo magari, kompyuta na vifaa vingine vya kuthaminisha madini.

Walisema kupewa kwa vitendea kazi hivyo ni deni na kwamba wanatamani kadirio walilopewa la kukusanya Sh. bilioni 475 kwa mwaka 2019/20 wavuke lengo hilo ili kutoa shukran kwa Rais kwa vitendo.



Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani (katikati), akikata utepe kuzindua umeme wa REA, katika nyumba ya mwananchi wa Kata ya Igunda, Halmashauri ya Ushetu, wilayani Kahama, mkoani Shinyanga jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Mkandarasi umeme REA apewa kibano

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAZIRI wa Nishati, Dk. Merdard Kalemani, ametoa siku 30 kwa kampuni ya Angelique International Co. Ltd kuhakikisha vijiji vyote 54 viliyoko katika Halmashauri ya Ushetu wilayani kahama, vinapata nishati ya umeme ifikapo Januari 4, mwakani. Dk. Kalemani alitoa agizo hilo juzi akiwa na ziara ya siku moja ya kutembelea na kukagua mradi wa umeme unaotekelezwa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) mkoani Shinyanga katika Halmashauri za Msalala na Ushetu.

Kutokana na kusuasua kwa utekelezaji wa miradi hiyo, alisema mpaka sasa wahandisi watatu kati ya wanne wa kampuni hiyo, ameshawanyan'ganya hati za kusafiria.

Waziri alisema kampuni hiyo ilitakiwa kupeleka umeme kwenye vijiji 54 vya Halmashauri ya Ushetu tangu mwaka 2017 lakini mpaka sasa imepeleka kwenye vijiji 14 tu. "Mkuu wa wilaya, wahandisi wa kampuni hii wako wanne na kati yao watatu nimeshawanyang'anya hati za kusafiria mpaka watakapokamilisha mradi wa REA ambao wanautekeleza katika Mkoa wa Shinyanga. Hawatarejea nchini kwao India mpaka wakamilishe kazi," alisema.

Pia aliwataka makandarasi hao kutoruka vijiji na kubagua nyumba za wananchi wakati wa ufungaji wa umeme na kuongeza kuwa nyumba za tembe, nyasi, ghorofa, tope na nyumba za malumalu zote zina hadhi sawa ya kupata umeme.

Alisema serikali imetoa Sh. bilioni 16.8 fedha za Watanzania kwa ajili ya kupeleka umeme katika vijiji vyote vilivyoko mkoani Shinyanga, lakini bado mkandarasi yuko nyuma ya muda.

Kalemani pia alimtaka mkandarasi kuhakikisha anaongeza kasi ya utendaji kazi na kuhakikisha kabla ya sikukuu ya Krismasi, vijiji sita vilivyoko katika kata ya Igunda vinapata umeme na kuhakikisha taasisi zote za umma zinalipia Sh. 27,000 na kuunganishiwa umeme.

Naye Diwani wa Kinamapula, Sharif Samweli, alisema kuna miradi ya maji ya visima virefu imerukwa na mkandarasi ambavyo vinaendeshwa kwa gharama kubwa kulinganisha na vingekuwa na umeme.

Alisema kuwa visima hivyo viko katika kata ya Chambo, makao makuu ya Halmashauri ya Ushetu Nyamilangano, Igunda na Bulungwa. Kutokana na kukosekana kwa umeme, alisema wananchi wanatumia gharama kubwa kuviendesha kwa kutumia umeme wa jenereta.

## Waanzisha dawati la watoto shuleni

**Na Mwandishi Wetu,** SUMBAWANGA

WIZARA ya Afya, Maendeo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kupitia Idara Kuu Maendeleo ya Jamii, imefungua madawati ya watoto kwa baadhi ya shule za Msingi na sekondari katika Manispaa ya Sumbawanga kwa lengo la kupambana na ukatili dhidi ya watoto ikiwemo mimba za utotoni.

Mkurugenzi Msaidizi anayeshughulikia masuala ya watoto kutoka Idara Kuu Maendeleo ya Jamii, Sebastian Kitiku, akizungumza juzi na wanafunzi wa shule za msingi Chemchem na Lukewile zote Manispaa ya Sumbawanga, aliutaja Mkoa wa Rukwa kuwa na changamoto kubwa ya mimba za utotoni.

Kitiku aliwataka watoto shuleni hapo kulitumia dawati hilo ipasavyo ili kuwa masaada mkubwa kwa wanafunzi wanaokumbana na vitendo vya ukatili na kuwataka kutokuwa waoga wa kutoa taarifa ili kuwawezesha walimu wa malezi kuangalia namna bora ya kulifanyia kazi tatizo hilo.

Alisema watoto wanatakiwa kupewa haki zote kama ilivyo kwa watu wazima huku akizitaja haki hizo kuwa haki ya kulindwa, kuendelezwa, afya, kutobaguliwa na kushirikishwa kama ilivyobainishwa katika Sera ya Taifa ya Mtoto ya Mwaka 2008.

Mkurugenzi huyo pia aliwataka watoto hao kutoa taarifa katika Dawati la Jinsia la Jeshi la Polisi lakini pia kutumia mtandao wa simu ya bure ya 116 ili kupewa msaada wa haraka pindi watakapobaini kuwa wanafanyiwa vitendo vya ukatili.

Alivitaja vitendo hiyo kuwa ni ulawiti na ubakaji, kazi ngumu kwa watoto na utumikishwaji watoto nyumbani kwa maana ya ukatili wa kingono na kimwili.

Dawati la watoto katika shule hizo limefanyika kwa wanafunzi husika kuchagua wawakilishi wao ndani lakini pia wanafunzi hao baada ya kuelimishwa pia wamewachagua walimu ambao wanawaamini kuwa walezi wao ambao kimsingi watafanya kazi kwa karibu sana na dawati la jinisia shuleni hapo.

Uanzishwaji wa dawati la watoto shuleni pia limefanyika katika Shule ya Sekondari Kilimani Maweni iliyoko nje kidogo ya mji wa Sumbawanga.

Katika ufunguzi wa dawati hilo, wizara kwa kushirikiana na uongozi wa shule na mkoa waliongoza wanafunzi kuchagua wawakilishi wao lakini pia walichagua walimu wawili kuwa walimu wa malezi shuleni hapo.

Wataalam wa Wizara kutoka Afya Idara Kuu Maendeleo ya Jamii, wako mkoani Rukwa kushirikiana na mkoa huo kuendeleza juhudi zake za kutokomeza vitendo vya ukatili dhidi ya watoto.

# Jamii yatakiwa kuwashirikisha wenye ulemavu

**Na Mwandishi Wetu**

WATANZANIA wametakiwa kuimarisha utamaduni wa kuwashirikisha watu wenye ulemavu katika kazi mbalimbali kwani wanao uwezo iwapo watapewa fursa.

Wito huo ulitolewa na Mkurugenzi wa Shirika lisilo la Kiserikali la Tanzania Youth Coalition (TYC), Lenin Kazoba, katika kongamano linalofanyika Weruweru, wilayani Hai, Kilimanjaro likishirikisha vijana 60 kutoka nchi tano za Afrika Mashariki za Tanzania, Rwanda, Kenya, Uganda na Burundi.

Kongamano hilo linalenga kuwajengea uwezo vijana katika maeneo mbalimbali ili waweze kuwa washiriki wenye tija katika kufikia maendeleo endelevu ya nchi zao na eneo la Afrika Mashariki.

TYC ni mwamvuli wa mashirika yasiyo ya kiserikali na vyama vya kijamii zaidi ya 120, vinavyohusika na maendeleo ya vijana katika nyanja mbalimbali Tanzania Bara na Visiwani.

"Ni muhimu tuangalie namna ya kuwapa fursa zaidi, kuwatia moyo na kuwajengea uwezo watu wenye ulemavu," alisema Kazoba wakati wa kutambua Siku ya Walemavu Duniani inayoadhimishwa kila mwaka Desemba 3.

Mmoja wa washiriki, Lilian Munuo 23, alisema bado juhudi zinatakiwa kwa jamii kutambua mahitaji ya wenye ulemavu.

"Wakati mwingine watu hufikiria kuwa huwezi kufanya jambo fulani kwa kutotaka tu, huku ikiwa ni kweli una changamoto ya ulemavu. Hili huumiza," alisema Lilian mwenye tatizo linalofahamika kitaalamu kama `muscular dystrophy` linalosababisha matatizo katika misuli na kuathiri utendaji kazi wa viungo.

Lilian ambaye ni mbunifu na mchoraji pia ametoa wito kwa serikali na mashirika binafsi kuendelea kuwafikiria walemavu wakati wote wa miradi ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali hapa nchini ili kuwa na mazingira rafiki kwao.

Naye Colman Ndetembea, alisema ni muhimu kuongeza juhudi kuwapatia watu wenye ulemavu vifaa saidizi, fursa na matibabu yanayotakiwa.

Colman alibuni kiti mwendo kinachoweza kusaidia walemavu au wagonjwa mbalimbali wa viungo kama waliovunjika uti wa mgongo na wenye matatizo ya misuli miongoni mwa wengine. Chombo hicho kinaweza kikatumika kama kiti, kitanda au kumsaidia ambaye hawezi kusimama kufanya hivyo kama sehemu ya mazoezi.

Katibu Tawala Msaidizi (Utawala na Rasilimali Watu), Mkoa wa Kilimanjaro, Bwai Biseko, aliwataka vijana wanaoshiriki kongamano hilo kutumia maarifa watakayopata kuleta tija zaidi katika sekta za uzalishaji kama uvuvi, ufugaji wa wanyama, nyuki, samaki na misitu katika nchi zao.

"Hizi ndizo sekta zinazoweza kuwa na soko kubwa katika nchi zetu ni muhimu kwa vijana kufanya kazi kimkakati na jumuiya za ushirikiano wa kikanda Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Soko la pamoja la Mashariki, Kati na na Kusini mwa Afrika (COMESA),"alisema.

# NHIF yashushia rungu wadanganyifu

**Na Innocent Ng'oko,**
MBEYA

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) mkoani Mbeya umewaonya wenye maduka ya dawa, vituo vya afya na hospitali zilizoingia mkataba na mfuko huo kutoa matibabu kwa wagonjwa ambazo zitabainika kujihusisha na udanganyifu.

Kwa mujibu wa onyo hilo, watakaobainika kufanya hivyo mfuko utavunja mkataba, kutoza faini au kuchukua hatua kali za kisheria.

Meneja wa NHIF Mkoa wa Mbeya, Mbala Shitindi, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusiana na mikakati na jitihada zilizowekwa na ofisi hiyo katika kuwahudumia wateja.

Alisema mfuko umejipanga kuhakikisha kila Mtanzania anapata matibabu kwa bei nafuu na kuwa hivi karibuni mfuko huo umeanzisha bima ya afya kwa mfumo wa vifurushi na kuwa mpaka sasa kuna mwitikio mkubwa wa wananchi kujisajili.

Shitindi alitoa angalizo kwa wananchi wote wanaojiunga na mfuko huo kutosubiri mpaka wakaugua na kuwa kadi zote zinazotolewa huanza kufanya kazi baada ya siku 30. Alibainisha kuwa ni vyema wananchi wote wakajisajili kwa wakati ili kuepuka usumbufu usio wa lazima pindi wanapopata ugonjwa.

Aidha, Shitindi alisema kwa sasa kuna mitambo ya kisasa ngazi ya mkoa kwa ajili ya kuchapisha kadi za bima ya afya ambayo imetolewa tangu mwaka jana na serikali, hali ambayo imesaidia kupunguza ucheleweshaji wa kadi hizo kwa wanachama.

Meneja huyo alisema kwa sasa Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) uliokuwa ukihudumia katika ngazi ya wilaya, una uwezo wa kuhudumia hadi katika hospitali ngazi ya mikoa na kuwa wanachama wa NHIF wanaweza kuhudumiwa hadi nje ya nchi kwa ushirikiano na taasisi zinazotoa huduma hiyo.

Mpaka sasa NHIF inatoa huduma za matibabu za vifurushi vya Umoja Afya, Timiza Afya na Ushirika Afya kwa wakulima.



Mkurugenzi wa Taasisi ya Wanawake katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI) Kituo cha Maarifa Makumbusho, jijini Dar es Salaam, Janeth Mawinza, akitoa mada juzi, katika semina ya jinsia na maendeleo, ambayo hufanywa kila Jumatano na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) na kushirikisha wakazi mbalimbali wa jiji hilo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Kanyasu awapa somo wenye hoteli

**Na Mwandishi Wetu,**
MOROGORO

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, amewataka wamiliki wa hoteli na sehemu za biashara za malazi kuacha kuajiri vibarua na badala yake waajiri wafanyakazi wenye sifa za kuhudumia wateja, wakiwamo watalii. Pia amewataka wawekezaji hao wasijikite kujenga majengo mazuri ya hoteli badala yake waajiri wafanyakazi waliosomea fani za utalii na ukarimu.

Akizungumza katika mkutano wa mashauriano kati ya serikali, wafanyabiashara na wawekezaji uliofanyika juzi katika ukumbi wa hoteli ya Glonency mkoani Morogoro, Kanyasu amesema Hoteli nyingi mkoani hapo zina majengo mazuri yenye nakshi za kila aina lakini zimekosa weledi wa huduma kwa wateja.

"Mtalii anahitaji vitu viwili pekee, moja ni ukarimu na pili usalama wake. Hoteli zilizo nyingi wahudumu hawana ukarimu," alisema. Kanyasu alisema baadhi ya wahudumu hawana lugha nzuri na hawajui hata namna ya kupokea wageni wakiwamo watalii wanapofika katika hoteli hizo.

Alisema wamiliki wa hoteli wamekuwa wakiajiri vibarua kwa ajili ya kuwalipa ujira mdogo hali inayosababisha kukosa wateja kwa vile hakuna mtalii anayefikia katika hoteli yenye huduma mbaya. Mkutano huo ulihudhiriwa na wafanyabiashara na wawekezaji takribani 500 na mawaziri 12 na uliandaliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji) kwa lengo la kusikiliza changamoto wanazokabiliana nazo.

Alisema mtalii akipata huduma nzuri katika hoteli anakuwa balozi mazuri kwa watalii wenzake na akipata huduma mbaya anakuwa balozi mbaya pia.

# Chuo cha Uhasibu kuwaunganisha wananchi EAC

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Chuo cha Uhasibu (IAA), Prof. Eliamani Sedoyeki, amesema chuo hicho, kimejipanga kutumia sekta ya elimu kuwa kiungo cha kuwaunganisha wananchi wa nchi za ukanda wa Afrika Mashariki.

Hayo aliyasema jana wakati wa mkusanyiko wa wanafunzi waliosoma chuoni hapo, kujadili mada mbalimbali, kuunda umoja wa wanachuo waliowahi kusoma chuoni hapo, na kutoa zawadi kwa wanafunzi waliofanya vizuri.

Alisema ni muda muafaka kwa taasisi za elimu nchini, kuangalia wapi walipotoka na wanapoelekea kwa kujenga uhusiano mzuri kazini.

Hata hivyo, alisema chuo hicho, kama sehemu ya kitivo cha diplomasia mkoani hapo, wamejipanga kutumia mafunzo ya elimu kuwaunganisha wananchi kutoka ukanda wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kuwa kitu kimoja.

"Chuo chetu kipo Arusha sehemu ya kitivo cha kidiplomasia na Makao Makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki tumejipanga kutumia sekta ya elimu kuwaunganisha wananchi kutoka nchi za Afrika Mashariki kuwa kitu kimoja," alisema Sedoyeki.

Alisema chuo hicho, kimeweka mpango mkakati wa kuboresha mazingira ya wanafunzi kusomea kwa kujenga miundombinu ya madarasa ya kisasa, kuongeza kozi mbalimbali na kuboresha mazingira ya watumishi kufanya kazi.

Alisema chuo hicho, kimefanya mazungumzo na Chuo Kikuu cha Bujumbura (Burundi), ili wakafundishe kozi mbalimbali zinazofundishwa IAA.

Alifafanua kuwa wakipata fursa ya kufundisha kozi hizo nchini Burundi itaisaidia nchi hiyo kuwa na bodi makini na yenye kujitegemea. Pia, wamefanya mazungumzo na uongozi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki chuo cha IAA, kipate fursa ya kwenda nchi ya Sudan Kusini kufundisha kozi mbalimbali kwa kuwa nchi hiyo bado ni changa kielimu.

Alisema endapo watapata fursa hiyo, lengo la chuo hicho ni kutoa mafunzo bora ambayo yatazalisha wataalamu kwenye nchi hizo.

"Sisi kama taasisi bora Afrika tunatoa kozi za fedha, biashara na Tehama, hivyo tumeanza kuangalia fursa zilizopo kwenye nchi hizo kwa ajili ya kuwapatia ujuzi na maarifa," alisema Sedoyeki.

Vile vile chuo hicho kimeanza utaratibu wa kuboresha miundombinu ya madarasa na mfumo wa Tehama na hadi sasa wameshanunua kompyuta 100 na kuagiza nyingine 300.

"Miezi sita ijayo tumepanga kuongeza madarasa 24, kumbi za mikutano za kutosha ili wanafunzi wasome katika maeneo yenye hadhi ya kimataifa.

Rais wa Umoja wa Wanafunzi waliowahi kusoma chuoni hapo, Dk. Edson Lugua, alisema baada ya kuchaguliwa kuwa kiongozi atawaunganisha wasomi waliosoma chuo hicho, kuwa kitu kimoja na kujadili mambo muhimu kwa maslahi ya taasisi hiyo na taifa kwa ujumla.

"Lengo la mkusanyiko huu ni kuwaleta wasomi waliosoma chuoni hapa, pamoja na wafanyakazi kuweka mpango mkakati wa kuendeleza taasisi hii kupiga hatua ya kimaendeleo," alisema.



Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Ikulu, Dk. Moses Kusiluka (katikati), akikabidhiwa zawadi ya mbuzi na baadhi ya wanufaika wa mpango wa kunusuru kaya maskini (Tasaf), wa kijiji cha Khusumay wilayani Karatu, mkoani Arusha juzi, kama ishara ya kushukuru serikali kwa kuwaondoa katika lindi la umaskini kupitia mpango huo uliowainigiza kwenye ufugaji wa wanyama mbalimbali. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# Viongozi wa dini, serikali, siasa wapewa neno

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

VIONGOZI wa kisiasa, kidini na serikali nchini, wametakiwa kuacha tamaa ya mali, fedha na madaraka badala yake watumikie wananchi ipasavyo.

Kiongozi wa Kanisa la Roho Mtakatifu, Kadinali Daudi Angolo, aliyasema hayo juzi katika mji mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, wakati akimsimika Askofu wa Kanda ya Kaskazini, Boaz Ambonya.

Kadinali Angolo, alisema viongozi wa serikali, dini na kisiasa wanatakiwa kuwatumikia wananchi na kuweka kando matamanio yao ili wafanikiwe kutimiza wajibu wao kikamilifu.

"Tusiweke mbele maslahi binafsi katika kutimiza wajibu wetu, kwa kuwa siku ya mwisho tutaulizwa tulifanya nini katika uongozi wetu na tutashindwa kuwa na majibu ya kujitosheleza hivyo tumtangulize Mungu kwa kila jambo," alisema Angolo.

Askofu Ambonya alisema kazi aliyopewa ya kuwatumikia waumini ni kubwa tofauti na awali alipokuwa mchungaji, hivyo atahakikisha anatimiza wajibu wake kikamilifu.

Alitoa wito kwa jamii kuachana na matendo maovu na kumrudia Mungu ili dunia iwe sehemu salama ya kuishi endapo kila binadamu ataacha kutenda dhambi na kumtegemea Mungu.

Aliwashukuru viongozi wa serikali na wa madhehebu mbalimbali ya dini walioshiriki katika hafla ya kusimikwa kwake kuwa askofu na kwamba kushiriki katika hafla hiyo kumeonyesha umoja na mshikamano.

"Mimi ni Mwenyekiti wa Umoja wa Viongozi wa dini kwenye eneo hili la Tarafa ya Moipo, nimeshukuru viongozi wenzangu mbalimbali walioshiriki katika tukio hili la mimi kusimikwa kuwa askofu wa Kanda ya Kaskazini," alisema askofu Ambonya.

Ofisa Mtendaji wa Mamlaka ya Mji mdogo wa Mirerani, Evence Mbogo, alisema serikali itaendelea kushirikiana na viongozi wa dini ili jamii iendelee kupata mahitaji ya huduma ya kiroho.

"Askofu Ambonya amesimikwa kutumikia Kanda ya Kaskazini tutaendelea kushirikiana na viongozi wa dini, mimi ni Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Manyara uliopo kwenye mamlaka ya mji mdogo wa Mirerani," alisema Mbogo.

Mwenyekiti wa Mara Group, Elia Wilson, alimpongeza Ambonya kwa kusimikwa kuwa Askofu wa kanda hiyo inayojumuisha mikoa ya Manyara, Arusha, Kilimanjaro na Tanga.

"Tunamuombea kwa Mungu kuitumikia nafasi hiyo vizuri na sisi watoto wake wa kiroho atuombe tuendelee kuwa na Mungu karibu kwa wakati wote ili tuache kutenda dhambi na kufuata amri zake," alisema Wilson.

# Gambo aanzisha mkakati kuongeza ufaulu

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MKOA wa Arusha umebuni mpango mkakati wa elimu wa kuongeza ufaulu kwa shule za msingi kwa kuanzisha utaratibu wa shule hizo kuwa na mtihani wa pamoja ukijumuisha shule binafsi zenye mchepuo wa Kiingereza ili kutambua shule ambazo hazifanyi vizuri .

Kauli hiyo ilitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, katika mahafali ya 15, kwa wanafunzi wa darasa la saba na ya 17, kwa wanafunzi wa darasa la awali yaliyofanyika katika shule ya mchepuo wa Kiingereza ya Green Valley ya jijini Arusha.

Katika mahafali hayo, jumla ya wanafanzi 120 wa darasa la saba walihitimu na kutunukiwa vyeti.

Gambo alisema utaratibu huo, utafanyika kila mara kwa wanafunzi kupewa majaribio ya mtihani ambao utatungwa na kuchapishwa mkoani hapa na hawatalipa fedha katika mashapisho ya mitihani hiyo.

Alisema lengo la kutungwa kwa mitihani hiyo, ni kuleta mwamko wa kielimu Mkoa wa Arusha ili kubaini uwezo wa shule za msingi zinazofanya vizuri na ambazo hazifanyi vizuri.

Hata hivyo, alisema kamati maalumu imeundwa kwa ajili ya kufuatilia na kubaini chanzo cha kutofanya vizuri kwa shule hizo na hatua zitachukuliwa.

"Tumeanzisha mpango mpya wa mtihani wa pamoja na utafanywa na shule zote za msingi za serikali na binafsi lengo ni kushindanisha uwezo wa shule zetu ili kubaini zinazofanya vizuri na zisizofanya vizuri, tumeunda na kamati itakayochunguza sababu za kutokufanya vizuri kwa shule hizo," alisema Gambo.

Hata hivyo, alionyesha kuchukizwa na hatua ya wanafunzi wa kike kubebeshwa mimba huku wahusika wa mimba hizo na wazazi wakiyamaliza nyumbani na kuwaonya wazazi kutokukubali watoto wao kukatishwa ndoto zao za elimu.

Mkurugenzi wa shule hiyo, Yahaya Ndarita, alisema shule binafsi zenye mchepuo wa Kiingereza zimechangia kuboresha elimu nchini na wanafunzi wanapomaliza elimu ya msingi wanakwenda kuchangamsha shule za sekondari za kata na kuleta ushindani wenye tija kwa taifa.

Aliwataka wazazi kutokuhofia kuwapatia watoto elimu bora kwa kuogopa gharama kwa kuwa zinachagiza ubora wa elimu na itasaidia kulikomboa taifa kielimu.

# Mapya yaibuka watoto yatima

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

WATOTO wengi ambao wanadaiwa kuwa ni yatima na kuchukuliwa na maofisa ustawi wa jamii katika Wilaya ya Hai, na kupelekwa kwenye vituo binafsi vya kuwalea, baadhi yao wamegundulika kupelekwa humo kimakosa.

Hiyo inatokana na kuwa na ndugu na jamaa wenye uwezo wa kuwahudumia.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa kituo cha kutunza watoto cha Kao la Amani, Elizebert Tarmo, amefichua ujanja unaofanywa na baadhi ya watu, kudanganya maofisa ustawi kwamba watoto hao hawana ndugu.

Tarmo alikuwa akizungumza na ujumbe wa viongozi wa tawi la Klabu ya Yanga lililopo katika Mji mdogo wa Bomang'ombe, Wilaya ya Hai ambao walikwenda kukabidhi misaada mbalimbali kwenye kituo hicho cha kulelea watoto yatima.

"Katika kituo hiki, kinalelea watoto yatima wapatao 48 na mwaka jana tulipokea watoto 24 kutoka Idara ya Ustawi wa Jamii, ila baadaye idara hiyo ilifanya utafiti na kugundua kwamba baadhi ya watoto hao wana ndugu na jamaa ambao wana uwezo wa kuwalea, isipokuwa wasichana wawili ambao wamekosa ndugu.

"Tumepokea watoto sita kutoka idara hiyo na wamebaki wawili baada ya ndugu na jamaa zao kuja kuwachukua ili kwenda kuwalea. Wengi wa watoto hao walikuwa wametoroka majumbani kutokana na mazingira magumu ukiwamo unyanyasaji wa kijinsia," alisema.

Kabla ya makabidhiano hayo ya misaada ya kibinadamu kama mchele, sabuni na daftari vinavyofikia kiasi cha Sh. 400,000, Mwenyekiti wa tawi hilo, Samweli Gataya alisema nafsi zao zimesukuma kutoa msaada huo ili kuendelea kuikumbusha jamii kuwa bado inawajibu wa kusaidia jamii, hasa yatima na wanaoishi katika mazingira magumu.

"Iko haja kwa wananchi wenzetu hasa wenye uwezo kiuchumi, mashirika ya kiraia na taasisi za umma, kujitokeza kuwasaidia watoto yatima na wale wanaoishi katika mazingira magumu ili kupunguza changamoto zinazowakabili kwa sasa," alisisitiza Gataya.

Aidha, alisema pia tawi hilo limetembelea Hospitali ya Wilaya ya Hai kuona wagonjwa na kutoa zawadi mbali mbali kama njia mojawapo ya kutafuta heri, ukiachana na masuala ya burudani.




Mkuu wa Wilaya ya Rombo mkoani Kilimanjaro, Agness Hokororo (kulia), akiongoza maandamano ya Jukwaa la Vuguvugu la Ukombozi wa Mwanamke Kimapinduzi (Tapo), wakati wa maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia yaliyofanyika katika Kata ya Nanjara, wilayani humo, juzi. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Udhibiti VVU shuleni waigusa serikali

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

SERIKALI imeeleza kuridhishwa kwake na mkakati wa kudhibiti maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) kwa wanafunzi wa shule 12 za msingi mkoani Kilimanjaro.

Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kippi Warioba, alisema utaratibu uliotumiwa na wadau wa maendeleo kutoka Shirika la Tanzania Women Research Foundation (Tawref), kupambana kuwalinda watoto dhidi ya maambukizi hayo, yanaipa imani serikali kuhusu kazi za kijamii zinazotekelezwa wilayani humo.

Katika hotuba yake iliyosomwa na Ofisa Tawala wa Wilaya ya Moshi, Khamisuu Uledi, imeeleza kuwa serikali itaendelea kuliunga mkono shirika hilo katika kutekeleza miradi yake ndani ya jamii.

Tawref inatekeleza mradi huo katika shule sita za Manispaa ya Moshi, shule na sita za Halmashauri ya Wilaya ya Moshi.

"Sisi kama serikali naomba niwamegee siri kwamba tunaridhishwa sana na NGO za Moshi (mashirika ya kiraia) yanavyofanya kazi na jamii kwa ushirikiano na serikali. Hamjatuangusha katika malengo yenu mliyoyatoa wakati wa usajili wenu," alieleza Warioba.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Tawref, Dafrosa Itemba, akizungumza katika mkutano wa tisa wa shirika hilo jana uliofanyika mjini hapa, alisema watoto 720 hutumia nyenzo kuchochea badiliko la tabia.

"Tumewapa elimu kupitia aina tofauti za ujifunzaji kama stadi za maisha, mashua salama, mahakama bandia na mabunge ya watoto. Mchango wa Tawtef katika kutoa huduma hizi ni kutoa huduma ya upimaji virusi vya Ukimwi na uunganishwaji wa dawa kwenye kata 11 za Manispaa ya Moshi na kata 31 za Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, kata sita za Wilaya ya Hai, Kata 13 za Jiji la Arusha na kata 13 za Halmashauri ya Wilaya ya Arusha," alieleza Itemba.

Tawref imekuwa ikichangia katika malengo ya Umoja wa Mataifa yanayolenga kupima asilimia 95 ya watu wenye virusi vya ukimwi ili asilimia 95 ya watu hao wapatiwe dawa na asilimia 95 ya waliopata dawa wawe wamefubaza makali ya VVU.

Kwa mujibu wa Itemba, malengo hayo yanalenga kutokomeza maambukizi mapya ya Ukimwi ifikapo mwaka 2030.

Kwa mwaka huu, taarifa ya Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (Tacaids), Watanzania waliopima wamefikia asilimia 78 ya makadirio ya watu wenye VVU ambao hawajapima.

# Kesi ubakaji watoto zaongoza Rombo

**Na Godfrey Mushi,** ROMBO

HAKIMU Mkazi wa Wilaya ya Rombo, Regina Futakamba, amesema kesi nyingi zinazofikishwa katika mahakama hiyo kwa sasa zinahusu zaidi matukio ya ubakaji wa watoto wenye umri chini ya miaka 12.

Akizungumza jana na wananchi wa Tarakea katika Kata ya Nanjara, Wilaya ya Rombo, hakimu huyo alisema ushahidi wa kitabibu unaotolewa na mashahidi wa upande wa mashtaka, unaonyesha kuwa watoto hao hubainika wamebakwa zaidi ya mara moja.

Alikuwa akitoa mada kuhusu matendo ya ukatili wa kijinsia na miongozo ya sheria, wakati wa kongamano la siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia yaliyoandaliwa na Jukwaa la Vuguvugu la Ukombozi wa Mwanamke Kimapinduzi (Tapo). "Hakuna mtoto aliyefika mahakamani kutoa ushahidi akawa amebakwa mara moja, wote wanaoletwa wameingiliwa zaidi ya mara moja. Sasa madaktari wanaokuja kutoa ushahidi baada ya kuwafanyia vipimo watoto hao wanaodaiwa kubakwa, huthibitisha kwamba watoto hao huwa wamebakwa zaidi ya mara moja.

Zaidi Hakimu Futakamba aliongeza: "Kina mama kabla ya kujitokeza kupinga ukatili huu, turudi kwanza katika jukumu letu la msingi la malezi bora, tufuatilie watoto wetu. Tumejikita zaidi katika kutafuta pesa (fedha) badala ya kuhudumia familia. Kilimanjaro nimeona karibu kila mwanamke anachakarika kwenye biashara kuanzia tarehe moja hadi mwisho wa mwezi, hii haifai." Katika kongamano hilo, Mratibu wa mradi wa ujenzi wa nguvu ya pamoja ya kutetea wanawake na watoto kupambana na ukatili wa kijinsia kutoka Shirika la Kwieco, Veronika Ullomi, alisema malengo mahususi ya kuanzishwa kwa vuguvugu hilo (Tapo) ni kukuza uelewa na utambuzi wa ushiriki wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwenye maamuzi na masuala ya uongozi.

"Nia yetu ni kujenga uelewa wa pamoja wa dhana muhimu za kijinsia zikihusishwa na maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa, lakini kuhamasisha jamii na kukuza uelewa wao juu ya dhana na itikadi ya ufeministi kama dhana ya kufikia usawa wa kijinsia," alieleza Ullomi.

Awali, akiwasilisha mawazo chanya ya wanaharakati hao kutoka Wilaya ya Rombo, Mwanaidi Mkumbo alisema moja ya mambo wanayoisihi serikali wilayani humo kuyapa mkazo niuanzishwaji wa kituo jumuishi cha pamoja," alieleza Mkumbo.

Pia wameitaka serikali kuzisukuma Halmashauri za wilaya mkoani Kilimanjaro kutenga walao ruzuku kwa ajili ya kuwawezesha watoa huduma kuwafikia waathirika wa ukatili wa kijinsia vijijini.



MAJALIWA ATIMIZA AHADI...
Hasunga aiweka rasmi tumbaku yote nchini sasa imenasa soko

Ukurasa 19

# BUFE

Ijumaa Desemba 6, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

UCHUMI



BODI MPYA & BOSI MPYA...
Kariakoo ya 'Hapa Kazi' ilivyofyeka deni la kutisha, yageuka rafiki TRA

Ukurasa 14



KUTOKA MGETA - MVOMERO

## Warudia kilimo kahawa baada ya nyanya na kabichi kuwatelekeza

Ukurasa 16

UCHUMI Ukurasa 18

Biashara katika picha Ukurasa 17

BIASHARA

BODI MPYA & BOSI MPYA...

# Kariakoo ya 'Hapa Kaz deni la kutisha, yageul

• Miaka 45, soko jipya, mageuzi makubwa yaja




SOKO kuu la Kariakoo, katika siku zake za mwanzo.

**Na Maneno Selanyika**

UNAPOTAJA Kariakoo kwa Kiswahili cha mitaani 'ni jina kubwa mjini'. Hicho ni kitovu cha Jiji la Dar es Salaam ambacho kimeteka biashara si kitaifa tu, bali Afrika Mashariki na Kati.

Hapo unataja wateja wa bidhaa zaidi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), kwa uchache unawataja watu kutoka Malawi, Zimbambwe, Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Umaarufu wa Kariakoo kibiashara si wa jana wala juzi, bali unaenda sambamba au hata zaidi ya uhuru wa nchi unaotarajiwa kusheherekewa Jumatatu ijayo.

Hilo ndilo chimbuko la aliyekuwa Rais wakati huyo, Hayati Mwalimu Julius Nyerere kuchukua hatua za makusudi katikati ya Kariakoo yenyewe, akaipa kandarasi Kampuni ya Ujenzi ya Mwananchi (MECCO) kujenga soko la kisasa ambalo kwa wakati huo halikuwa na mpinzani.

Jengo la aina yake ambalo halina kingo za kawaida zilizozoeleka katika majengo yaliyotapakaa kila mahali, chini yake kukiwa na eneo lililobuniwa, maarufu kwa jina la 'shimoni' ambako ndiko kulikuwa soko kuu la jumla.

Mfumo mzima wa soko hilo linalopambwa na masoko madogo nje yake, mwaka 1974 baada ya kukamilika, serikali ililiundia taasisi inayodumu hadi leo inayoitwa Shirika la Masoko Kariakoo.

**MENEJA MKUU**

Hetson Msalale, Meneja Mkuu wa Shirika la Masoko Kariakoo, anasema shirika hilo lenye miaka 45 hivi sasa lina historia ndefu ya kupitia vipindi mbalimbali vya uhai wake, tangu lilipozinduliwa rasmi na Rais Nyerere Desemba 8, 1975.

Baada ya kuwa kioo cha biashara kilichotamba kwa miaka mingi ndani ya jiji na kimataifa, pia limekutana na milima na mabonde ya kibiashara, ikiwamo mageuzi makubwa ya kiuchumi nchini mwaka 1985 yaliyofungua mlango huria na kasi kubwa ya ukuaji wa Jiji la Dar es Salaam.

Leo hii, shirika hilo lililobahatika kupitia mikono ya awamu zote za uongozi wa nchi, isipokuwa miaka 13 ya kwanza ya uhuru, liko chini ya uongozi wa Rais John Magufuli.

Meneja huyo anataja mambo kadhaa yanayohusu mafanikio ya shirika, ikiwamo kupata safu na muundo kamili wa uongozi kisheria baada ya kulegalega kwa miaka 16, kati ya mwaka 1999 hadi 2015.

Msalale anafafanua muundo huo ni kuundwa kwa Bodi ya Wakurugenzi yenye mwenyekiti, pia kumteua mtendaji mkuu, ambaye ni meneja mkuu, ikiwa ni kati ya uamuzi mkubwa wa awali uliofanywa na Rais Magufuli akiwa na wastani wa mwezi mmoja madarakani.

Anataja sehemu ya madhara yaliyotokana na kukosekana kwa uongozi kamili wa shirika na kuyumba kiutendaji, hali iliyochangia deni kubwa lililofikia Sh. bilioni 1.3, kutokana na madai kama ya kodi za mishahara na ardhi.

> **"Anataja sehemu ya madhara yaliyotokana na kukosekana kwa uongozi kamili wa shirika na kuyumba kiutendaji, hali iliyochangia deni kubwa lililofikia Sh. bilioni 1.3, kutokana na madai kama ya kodi za mishahara na ardhi.**

**BIASHARA IKOJE?**

Msalale anasema shirika hadi sasa limefanikiwa kuongeza wigo wa mapato yake, kupitia kuongezwa kwa maduka mapya madogo 99, maarufu 'Vigoli' kuzunguka jengo kuu la soko.

Anaainisha mustakabali wa bajeti ya Shirika la Masoko Kariakoo, likiwa na ongezeko la asilimia 32.4, akimaanisha ni kutoka Sh. bilioni 2.5 mwaka 2015/2016 ilipoundwa bodi hadi bajeti iliyoko sasa ya Sh. bilioni 3.7. Ni ongezeko la mara moja na nusu.

"Ukuaji huu wa bajeti ya shirika umekuwa ni kwa wastani wa asilimia 8.1 kila mwaka," Msalale anasema na kufafanua kwamba, mradi wa maduka umeongeza wastani wa mapato kutoka Sh. milioni 48.263 kwa mwezi.

Kuhusu madeni, meneja huyo

> **"Ukuaji huu wa bajeti ya shirika umekuwa ni kwa wastani wa asilimia 8.1 kila mwaka," Msalale anasema na kufafanua kwamba, mradi wa maduka umeongeza wastani wa mapato kutoka Sh. milioni 48.263...**

anasema hamasa na mwongozo unaoanzia kwenye bodi mpya, imewezesha kukombolewa deni la Sh. milioni 800, ambayo ni wastani wa theluthi mbili ya deni iliyolikuta (asilimia 61.5).

Sambamba na kukombolewa deni, anasema shirika hivi sasa 'halilazi' madeni stahiki ya kisheria kwa Mamlaka ya Mapato (TRA), akitaja mfano mojawapo wa makato ya kodi ya mshahara ya Lipa Kadri Unavyopata (PAYE).

"Haya ni mafanikio makubwa ndani ya shirika chini ya uongozi wa Rais John Pombe Joseph Magufuli, tangu alipoingia madarakani," anasifu.

**MIRADI MIKUBWA**

Msalale anasema kwa sasa, shirika lina mpango mkakati wa kuboresha jengo la soko lake dogo,

# zi' ilivyofyeka ka rafiki TRA



Lango la kuingia shimoni, katika soko kuu Kariakoo. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

kuligeuza katika mhimili mkubwa na wa kisasa, likikadiria kutumia zaidi ya Sh. bilioni 23.

Vilevile, meneja huyo anataja mpango mwingine ni upembuzi unaoendelea wa kujenga soko lingine la kisasa nje ya Jiji la Dar es Salaam, katika Manispaa ya Kinondoni unaokadiriwa kugharamu zaidi ya Sh. milioni 500 na uwekezaji kama huo katika eneo lake lingine la Tabata katika Manispaa ya Ilala.

Kwa mujibu wa meneja huyo, ndani ya miaka hiyo minne, limetoa ajira 27 na kuanzisha maeneo mapya maeneo mapya ya biashara kwa wajasiriamali 300.

**KUPANUKA MTAJI**

Msalale anasema tathmini ya shirika hadi Juni mwaka huu, inaonyesha kwa sasa linamiliki mali zenye thamani ya Sh. bilioni 56 kutoka Sh. bilioni 53.2 za miaka mitano iliyopita. Ni ongezeko la Sh. bilioni 2.8 na linajiendesha kwa kutumia mapato yake.

Anafafanua wigo wa mafanikio yake kwamba, kwa mwaka wa fedha uliopita, Shirika la Masoko Kariakoo ni miongoni mwa asasi za umma zilizowasilisha mchango wake serikalini, akitaja kiwango cha Sh. milioni 50.

Meneja Mkuu anaendeleza wigo wa majivuno yake, akitaja kuwapo maslahi bora kwa watumishi wa asasi hiyo kwa kutumia mapato ya ndani ambayo kwa sasa hayayumbi.



Hali ilivyo sasa sokoni Kariakoo.



Viongozi wa Nato katika picha ya pamoja. **PICHA: MTANDAO.**

## 'Songombingo' mabosi Nato sherehe miaka 70

SIKU ya kwanza ya mkutano wa wakuu wa nchi za Umoja wa Kujihami wa Nato, wiki hii ilishuhudia kubadilishana maneno makali kati ya marais Donald Trump na Emmanuel Macron, wa Ufaransa, na matakwa ya Uturuki yanayotishia kusababisha mkwamo.

Ilikuwa katika hafla ya kuadhimisha miaka 70 tangu kuundwa kwa jumuiya hiyo ya ushirikiano wa kijeshi kati ya Ulaya na Amerika Kaskazini.

Walianzia katika makao makuu ya Malkia wa Uingereza Elizabeth na kisha kuendelea nyumbani kwa Waziri Mkuu Boris Johnson, katika mtaa wa Downing.

Yalikuwa mapokezi ambayo viongozi hao walikarimiwa kwa glasi za vinywaji.

Matukio makubwa kwa siku hiyo yalikuwa ubadilishanaji maneno makali kati ya marais Trump na mwenzake wa Macron.

Kwanza Trump alimshambulia Macron, kwa kusema kauli yake ya awali kwamba Nato ilikuwa 'imekufa' kimawazo ilikuwa chafu na yenye dharau na akaongeza kuwa Ufaransa ni nchi inayohitaji ulinzi wa Nato kuliko nyingine yoyote.

Lakini, viongozi hao wawili walipokaa pamoja, Trump alipunguza makali ya lugha, badala yake alizungumza kwa utani, akimuuliza Macron ikiwa Ufaransa ingependelea kuwapokea magaidi wote waliokamatwa nchini Syria.

Rais Macron hakufurahia utani huo na kwa ukali alisema, "hebu tuache mambo ya mzaha".

Chanzo kingine cha mvutano katika mkutano huo, ni hatua za Uturuki za kununua mfumo wa ulinzi wa makombora kutoka Urusi na sharti la kutaka Nato iliweke kundi la Wakurdi kwenye orodha yake ya magaidi.

Ni sharti ambalo baadhi ya wanachama kama Ufaransa hawalikubali, ikizingatiwa kundi hilo lilikuwa mshirika mkubwa wa Nato katika vita dhidi ya kundi linalojiita Dola la Kiislamu, IS au Islamic State.

Katibu Mkuu Nato

Katibu Mkuu wa Nato, Jens Stoltenberg, anabainisha kwa mara ya kwanza, Nato imeizungumzia China katika tangazo la pamoja la viongozi, ikiitambua kama taifa kubwa ambalo ushawishi wake unaozidi kupanuka unaambatana na fursa pamoja na changamoto kwa wanachama wote wa jumuiya hiyo.

Hili nalo huenda lisipate muafaka wa wanachama wote, kwani nchi muhimu kama Ujerumani zinapendelea kuwa na sera binafsi kuhusu mahusiano yake na China.

Shinikizo la Rais Trump, kuzitamka nchi nyingine zitoe fedha zaidi kugharimia uendeshaji wa shughuli za Nato halikuepukika, ingawa halikupata muda wa kutosha katika mkutano wa saa tatu tu.

Katika hali hii ya mvutano, Katibu Mkuu wa Nato,Jens Stoltenberg na Kansela wa Ujerumani, Angela Merkel, wanatazamiwa kutumia maarifa yao ya kidiplomasia, kutafuta suluhu.

• **HABARI HII KWA MUIJIBU WA MTANDAO.**

BIASHARA

KUTOKA MGETA - MVOMERO

# Warudia kilimo kahawa baada ya nyanya na kabichi kuwatelekeza

• Waliacha kwa mbwembwe za kung'oa miche • Wapiga 'magoti' na kurejeshwa kundini

**Na Ashton Balaigwa, Morogoro**

ZAO la Kahawa limekuwa juu katika kuongoza kwa kipato na kuleta maendeleo ya haraka kwa jamii ya wakulima.

Hapo unataja maeneo kama mkoa Kilimanjaro na Kagera. Pia, kuna wilaya za Mbinga, Ruvuma na Rungwe mkoani Mbeya, kwa kiasi kidogo tarafa za Mgeta wilayani Mvomero, mkoa Morogoro.

Mgeta kunalimwa kahawa tangu miaka ya 1970, na kukaibadilisha maisha ya wananchi wakapata maendeleo ya haraka, lakini ghafla ilikufa katika miaka ya 2,000 wakulima wengi kukimbilia kilimo cha nyanya, matunda na kabichi.

Inadaiwa, wakulima wengi walirubuniwa na vijana waliowahadaa kahawa inawachelewesha kujikwamua kimaisha, kwa kusubiri muda mrefu kupata fedha zake, wakakubali na kuanza kung'oa miti ya kahawa shambani.

**WAKULIMA WAELEZA**

Anatheti Kambaya, ni mkazi wa tarafa ya Mgeta, anasimulia miaka ya nyuma kahawa lilikuwa maarufu na wasomi wengi walienda shule kwa ada za kahawa, kwa sababu kuu uhakika wa soko na kuwa na bei nzuri, ikilinganishwa na mazao mengine kama mahindi mtama,mpunga na mbogamboga.

"Zamani Tarafa ya Mgeta ilikuwa chini ya Halmshauri ya Wilaya ya Morogoro Vijijini, kabla ya kugawanya kuwa chini ya wilaya ya Mvomero" anasema Anatheti na kuongeza:

"Hivi sasa sisi wakazi wa tarafa ya Mgeta ndio tulikuwa tunachangia mapato makubwa kutokana na kahawa, pia ndio eneo la kwanza kujengwa nyumba bora na kutoa wasomi ukilinganisha na maeneo mengine ya wilaya kutokana na zao hili,"

" Huku Mgeta hali ya hewa yake ni kama Kilimanjaro, hivyo zao letu kuu lililotutoa lilikuwa kahawa, watu wamesoma huku na kupata maendeleo kwa ajili ya kahawa lakini miaka ya 2000 lililopoingia zao la nyanya tu, vijana wenye tamaa wakaanza kung'oa miti yake ili kupanda nyanya na kabichi," anafafanua.

Abdul Kalindo, ni mkulima wa kahawa katika miaka 1970, anayesema: "Mimi binafsi unavyoniona hapa niliweza kusomesha watoto wangu mpaka chuo kikuu na leo wana kazi nzuri wananitunza.

"Kwa kuwa kipindi kile nilikuwa nalima kahawa na napata pesa nyingi.Mimi ni mmoja wa watu hapa Mgeta niliyojenga nyuma bora, wakati huo na imedumu mpaka sasa hivi hii yote ilikuwa ni kahawa."

Anataja ushawishi wa vijana baada ya kuona wenzao katika maeneo ya vijiji vingine kama Mlali na Doma, katika barabara kuu ya Morogoro -Mikum, kuelekea Iringa kulima nyanya.

Mkulima Albert Senga, anasema baada ya kuingia kilimo cha nyanya, kabichi na matunda, walikuwamo katika walioshawishiwa kung'oa miti ya kahawa na kuanza kupanda mazao mengine.

Anakiri sura ya pili, nyanya na kabichi ziliwapatia fedha za haraka



Shughuli za upandaji kahawa zikiendelea.

Wakulima wakivuna kahawa zao. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

kutokana na soko kubwa, wateja wao wengi walitoka mikoa kama Dar es Salaam na Dodoma

"Soko la Dodoma lilianza kupotea kwa kuwa vijiji vilivyopo barabara kuu ya Dodoma - Morogoro eneo la Dumila, nao wanalima nyanya na barabara vijiji vya barabara kuu ya Dar es Salaam - Morogoro na wanalima nyama. Sasa tumejikuta hatuna soko na wakati mwingine tunalazimika kuzitupa nyanya au kuwapa mifugo," anaeleza.

**"Tulifanya utafiti nchi nzima na maeneo mengine ni mapya hayajalimwa, mikoa inayolima kahawa ni Kilimanjaro, Mbeya, Ruvuma na Kagera," anasema Kilambo.**

**WARUDIA KAHAWA.**

Kutokana na hiko, wakulima wa Mgeta, sasa wameanza kufufua tena kilimo cha kahawa, ikiwa ndio zao pekee la biashara kama ilivyokuwa huko nyuma.

Ni uamuzi uliohamasishwa na Taasisi ya Utafiti wa kahawa nchini (TacRi) kwa kushirikina na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tanzania (CDTF), zilizotoa mbegu, mafunzo na vifaa vya kilimo kwa vikundi mbalimbali vinavyojishughulisha.

Mwenyekiti wa kikundi cha ujasiriamali wa kilimo cha Tugendelele, Stephen Msimbe, anasema baada ya kupatiwa mbegu na vifaa, tayari wameshazalisha vitalu vyenye miche 60,000.

Anasema miche hiyo ya kahawa wataigawanya kwa wakulima wa tarafa ya Mgeta, wapande shambani na mingine kugaiwa katika taasisi mbalimbali za serikali kama shule za msingi na sekondari, ili waipande katika mashamba yao.



Nyanya wilayani Mvomero, zao lililowafanya wakulima kuacha kahawa, lakini wamierudia tena kahawa, baada ya nyanya hizo kukosa soko.

Msimbe anataja matatizo yao kwa sasa ni kuikosa mbolea ya ruzuku na mashine za kisasa za kukoboa kahawa, kukausha ,kupukucha na kuziweka katika madaraja.

Anaiomba serikali, iwasaidie nyavu za kutunzia vitalu vya miche ya kahawa, maturubai na kuwaongezea watalaamu wa kuwapa elimu ya kilimo cha kisasa.

Ni kauli inayoungwa mkono na Diwani wa Kata ya Bunduki, Prosper Mkunule, anayesema tayari wameshapanda miche 30,000 aina za Arabica na Robusta, katika mashamba ya kata hizo mbili, ikiwa ni mkakati wa kufanya zao hilo kuwa la biashara.

Anasema, kuwa kabla ya kupanda miche hiyo, taasisi ya CDTF iliwapelekea watalaam wa kilimo na kuvifundisha vikundi 35 kutoka kata za Bunduki na Mgeta, walime kwa kuzingatia kanuni bora shambani.

Diwani, anasema kilimo hicho cha kahawa kilikuwa kikisaidia kuhifadhi mazingira na vyanzo vya maji katika tarafa nzima ya Mgeta akini uharibifu na mabadiliko ya tabianchi wameamua kukirudisha tena.

**MGETA YASAIDIWA**

Mkurugenzi wa CDTF, Henry Mgingi, amesema Taasisi hiyo yenye makao makuu jijini Dar es Salaam, imekuwa ikisaidia tarafa ya Mgeta katika kilimo na mwaka elimu na mpango mkakati uliopo ni kurudisha kilimo cha kahawa kuwa mkombozi wa wananchi kibiashara.

" Sisi Kama CDTF tumeona wananchi wa Tarafa ya Mgeta kutokana na hali yao ya hewa wanaweza kuendelea tena na kulima zao la kahawa ambalo bado lina umuhimu hapa nchini kutokana na kuwa na soko la uhakika, tofauti na zao la nyanya na kabichi ambao wateja wake ni wa kubembeleza," anasema.

Anasema baada ya kupanda vitalu vya miche hiyo ya kahawa CDTF ilimua sasa kugharamia mafunzo kwa vikundi 35 vya kata ya mgeta na bunduki ili kujua mbinu za kilimo hicho na shughuli za ujasiliamali zilizotolewa na watalaamu mbalimbali kwa gharama ya Sh. milioni sita.

Mgingi anasema malengo yao ni kuhakikisha wakulima wa tarafa ya Mgeta wanafanya kilimo endelevu cha kutunza mazingira na kuhifadhi vyanzo vya maji, pia kupunguza kasi ya uchomaji moto unaosababisha uharibifu wa mazingira.

Mwenyekiti wa Bodi ya CDTF, Leon Msimbe, anasema: "Hivi sasa nchi inakwenda katika uchumi wa viwanda na mahitaji makubwa ni malighafi zinazotokana na kilimo, ikiwamo hili zao la kahawa ambalo lina soko kubwa ndani na nje ya nchi sasa.

"Sisi kama CDTF tumeona tukirudishe tena kilimo hiki cha zao la kahawa katika Tarafa ya Mgeta ili kuunga mkono jitihada za Serikali."

Mhandisi Msimbe, anavitaka vikundi kutumia kilimo kurejesha hali ya zamani, iliyochafuliwa na kuathiri mazingira, ikiwamo Mto Mgeta ambao ndio sehemu ya Mto Ruvu.

**MIKAKATI TaCRI**

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kahawa (TaCRI), Dk. Deusdedit Kilambo, anataja mkakati wake kuendeleza zao hilo, tayari wameainisha maeneo mapya ya kupanda, akiitaja ni Wilaya ya Tanganyika mkoani Katavi na maeneo ya milima ya Uluguru, iliyopo wilaya Mvomero wakibaini yana uwezo mkubwa kuzalisha zao hilo.

Mkurugenzi huyo anasema kuwa katika Wilaya ya Tanganyika, baada ya kufanyiwa utafiti wameanza uzalishaji wa miche bora ya kahawa, kazi inayofanyiwa na TaCRI

Dk. Kilambo anasema, hivi sasa wana aina mpya za kahawa 23 watakazozipanda katika maeneo mapya na zamani.

"Tulifanya utafiti nchi nzima na maeneo mengine ni mapya hayajalimwa, mikoa inayolima kahawa ni Kilimanjaro, Mbeya, Ruvuma na Kagera," anasema Kilambo.

Waziri wa Kilimo, Jafeth Hasunga, anasema hivi sasa serikali imejipanga kutafuta wanunuzi wa bei nzuri ya kahawa katika soko la dunia na tayari wameshapatikana wanne na walishafika nchini na wameonyesha nia ya kununua kahawa ya Tanzania.

## BIASHARA KATIKA PICHA



Mkulima wa Kijiji cha Tandala, Wilaya ya Chemba, mkoani Dodoma, Ally Abdalah, akikagua mazao katika bustani yake kijijini hapo, juzi. Mkulima huyo, amekuwa akitumia kilimo cha umwagiliaji ili kujipatia mazao bora kwa ajili ya biashara na chakula. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Vijana wakikokota maguta yaliyosheheni vipande vya magodoro katika Barabara ya Shekilango, jijini Dar es Salaam juzi. Vipande hutumika kutengenezea viti vya makochi kwa ajili ya biashara. **PICHA: SABATO KASIKA**



Mfanyabiashara wa makoti ya mtumba (kulia), akiwashawishi wateja kununua bidhaa zake katika Mtaa wa Sokoine, jijini Arusha hivi karibuni. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

UCHUMI



Muhabe Marwa akionyesha baadhi ya kazi zake za ujasiriamali. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA.**

# Yalivyo maisha mapya kwa ngariba mstaafu 'ngangari'

- Ya leo; vitisho, marufuku kilimo, kutengwa
- Asimamia uamuzi, mkufunzi wa waliokataa

**Na Sabato Kasika, aliyekuwa Serengeti**

***SEHEMU ya kwanza jana, ilikuwa na simulizi ya ngaruba aliyeacha, alichofanya huko na mkasa uliomuondoa katika kazi hiyo ya ukatili wa kijinsia na haki za binadamu. Endelea kujua anachokifanya sasa, katika ajira mpya.***

MUHABE Marwa, alistaafu kazi ya ungariba mwaka 2016 akiwa amekeketa mara moja tu, lakini alipopata elimu dhidi ya vitendo vya ukeketaji, aliamua kuweka zana zake chini na kuhamia ajira kinzani.

Haukua mtihani rahisi kuacha kazi hiyo. kijijini alitengwa, wakamzuia kulima katika mashamba ya familia na vitisho lukuki. Kamwe hakubadilika, badala yake akatoka 'kivingine'anashika chaki kuelimisha vita dhidi ya mila huyo potofu.

Katika mazungumzo yake na Nipashe, elimu iliyombadilisha inatoka kwa Rhobi Samwelly, Mkurugenzi wa taasisi ya Hope for Girls and Women Tanzania, iliyopo mjini Mugumu, Serengeti mkoani Mara.

Ngariba huyo mstaafu, sasa amepewa jukumu la kuwa 'mhadhiri' anayetoa elimu kuhusu mila na desturi za kabila la jamii yao waachane nambo yaliyopitwa na wakati, zikiwamo za ukeketaji.

Muhabe mwenye umri wa miaka 47, anasema ingawa uamuzi wake huo umesababisha akumbane na matatizo mengi, ikiwamo vitisho, msimano wake hatarajii kurudia kazi hiyo.

"Mimi kwa sasa ninaishi mjini Mugumu. Mara tu baada ya kuachana na kazi ya ukeketaji, niliifanya kwa msimu mmoja wakati huo nikiishi katika kijiji cha Matare, wilayani Serengeti," anasema Muhabe.

Mama huyo anasema amelazimika kwenda kuishi mjini Mugumu katika nyumba za kupanga, kwa vile hakuona sababu ya kuendelea kuishi kijijini, wakati hakuwa na sehemu ya kulima, baada ya kunyang'anywa mashamba na ndugu zake.

"Kwa kweli hali bado haijawa nzuri, hasa baada ya kukosa sehemu ya kulima. Ila ninamshukuru Dada Rhobi Samwelly, ambaye amenileta hapa nyumba salama ya Hope for Girls and Women Tanzania," anasema.

Anasema jukumu lake katika nyumba hiyo, ni kufundisha mila na desturi za kabila lake na anapewa posho kidogo, inayomuwezesha aendelee kuishi mjini, wakati akitafuta njia za ziada

"Pamoja na matatizo yote ninayokumbana nayo baada kuacha ukeketaji, siwezi kurudia kazi hiyo. Badala yake ninayageuza matatizo hayo kuwa fursa ya kupiga hatua kwenda mbele," anasema.

Muhabe anaanza kusimulia kwamba, amezaliwa katika familia ya watoto 14, yeye akiwa wa tatu. Pia, wapo wengine 10 waliozaliwa na mke wa pili wa baba yao.

Anasema, alisoma Shule ya Msingi Kibeyo na kuhitimu mwaka 1987. Mwaka uliofuata alikeketwa na kisha mwaka 1990 akaolewa na kubahatika kupata watoto saba wote wa kiume, lakini walio hai sasa ni watatu.

> **"Lakini nilishaachika baada ya kukumbana na manyanyaso katika ndoa yangu.Kwa sasa ninaishi mwenyewe nikiendesha maisha yangu, ingawa kama nilivyosema yana changamoto nyingi," anasema.**



"Lakini nilishaachika baada ya kukumbana na manyanyaso katika ndoa yangu.Kwa sasa ninaishi mwenyewe nikiendesha maisha yangu, ingawa kama nilivyosema yana changamoto nyingi," anasema.

Aidha, anasema jina la Muhabe alilopewa ni la bibi yake mzaa baba, ambaye alikuwa anafanya kazi ya ukeketaji, hivyo naye alipewa jukumu hilo, ambalo alilifanya mara moja tu na kuliacha kabisa.

**ALIANZAJE UNGARIBA?**

Muhabe anasema, alianza kazi ya kukeketa mwaka 2016 na kisha akaacha kazi hiyo na kukumbana na vitisho kutoka kwa familia na wazee wa mila, vikiwamo kwamba atakutwa na mambo mabaya kwa kukiuka mila ya kikurya.

Ngariba huyo mstaafu anasema, aliamua kuziba masikio na kumtegemea Mungu na ameweza kuvuka vikwazo hivyo ingawa kinachomsumbua sasa kukosa sehemu ya kulima ili aendeshe maisha yake kwa uhakika.

"Dada Rhobi wa Hope for Girls and Women Tanzania ananisaidia, lakini pia ni muhimu kuwa na kitu changu mwenyewe cha kuniwezesha kuendesha maisha yangu ya kila siku," anasema.

Ngariba hiyo anasema, vitisho haviko kwake tu bali hata wale wanaotoa elimu ya kupinga ukeketaji nao wanakumbana navyo, kwa vile wanagusa maslahi ya wanaofaidika na ukatili huo.

**OMBI LAKE**

Anasema, jambo la kwanza ni kuwataka ngariba wengine wanaoendelea kazi hiyo waache mara moja na kuungana nayo katika vita ya kupinga ukeketaji kwa ajili ya kunusuru maisha ya watoto wa kike.

"Ninasema hivyo kwa sababu uhai wa binadamu ni muhimu kuliko fedha, na pia wazee wa kimila waache kutisha watu wanaokataa kukeketa au kukeketwa kwamba kuna madhara watapata, huo ni uongo," anasema.

Mubabe anawaomba wadau wote wanaojishughulisha na kupinga vitendo vya ukeketaji, wawasaidie ngariba wote walioachana na ukeketaji kwa hali na mali, ili waweze kujikimu kimaisha.

"Binafsi ningesaidiwa kupata mtaji ili niweze kufanya biashara ndogo hapa mjini Mugumu, huku nikiendelea kuelimisha jamii kuhusu madhara ya mila potofu zikiwamo za ukeketaji," anasema.

Anasema, anamhurumia Rhobi Samwelly, ambaye amekuwa akimpa posho inayomsaidia kuendesha maisha, lakini akipata msaada zaidi kutoka kwa wadau wengine, atakuwa na uhakika kumudu gharama za maisha.

"Ninasikia kuna mashirika huwa yanawasaidia fedha za biashara, ngariba wanaoacha kazi hii, niwaombe kama wapo wanione hata mimi ambaye niko hapa nyumba salama ya Hope for Girls and Women Tanzania," anasema.

Muhabe anasema, ameamua kutokuwa miongoni mwa watu wanaosababisha madhara kwa watoto wa kike, kwa vile ameshaelimishwa na kutambua kile ambacho kinawakuta watoto wanaokeketwa.

"Bahati nzuri mimi nilipokeketa, hakuna binti aliyepoteza maisha kwa kutokwa na damu nyingine bali wote walisalimika, hivyo ninashukuru nimeacha kazi hiyo mikono yangu ikiwa salama," anasema.

"Ninajua kuna vitisho ambavyo umekuwa ukikutana navyo, katika vita hii, wewe endelea usikate tamaa, serikali inaunga mkono juhudi zako na inataka vitendo vya ukeketaji vikomeshwe kwenye jamii," anasema.

BIASHARA

## MAJALIWA ATIMIZA AHADI...

# Hasunga aiweka rasmi tumbaku yote nchini sasa imenasa soko

- Ni ziada ya walichopangiwa kuzalisha
- Walivuka lengo la mikataba yao 121%
- Soko jipya 'jeupe' kwa Wachina na ...

**Na Beatrice Moses**

WAKULIMA wa zao la tumbaku chini ya usimamizi wa Wizara ya Kilimo nchini, wanajipanga kujitanua na kuliteka soko la kimataifa la zao hilo la kibiashara.

Miongoni mwa soko jipya linalonyemelewa na wakulima hao ni China na barani Asia kwa jumla. Hivi sasa juhudi hizo zimeanza kwa utafiti wa mbegu za tumbaku kutoka nchi hizo, ili kuweza kuwavutia wanunuzi waliopo kwenye huko.

"Jitihada hizo zinaendelea vizuri, mpaka sasa mbegu tatu kati ya tano zinaonekana kufanya vizuri, hivyo matokeo ya utafiti huo yatatuwezesha kuingia katika soko kubwa la China ambalo linatajwa kuwa na idadi ya watu wengi," anasema Waziri wa Kilimo Japhet Hasunga.

Anasema katika msimu wa kilimo 2019/2020 ambao masoko yake yataanza mwezi Mei 2020. Kampuni za ununuzi zilizopo nchini ambazo ni Alliance One Tanzania, Premium Active Tanzania na Japan Tobacco International zimetoa mikataba ya kilo 42,225,985.

"Tayari wakulima wapatao 33,000 wameomba kusajiliwa na Bodi ya Tumbaku kutokana na uzalishaji huo," anasema Hasunga na kuongeza: "Uzalishaji huo ni mdogo na hivyo unaacha wakulima takribani 16,000 bila kulima tumbaku msimu huu."

Waziri anasema kampuni nne mpya tayari zimeonyesha nia ya kununua tumbaku nchini katika msimu ujao, wakati kampuni nyingine ya Tanzania Leaf Tobacco imekuwa kimya kutoa makisio ya uzalishaji msimu wa sasa.

Anataja jumla ya kampuni nne, zitanunua tani kilo milioni 15 na laki tatu ya tani 15,300, kati yake moja itawakilishwa na kampuni ya kizawa Grand Tobacco Growers, itakayonunua kilo milioni tisa sawa na tani 9,000 ambayo ni asilimia 58.8 ya makadirio hayo ya ununuzi.

Hasunga alizitaja kampuni hizo na makadirio yake kwa uzani wa kilo ni Magefa Growers (5,500,000) Transafricque inayowakilishwa na wazawa (9,000,000), Petrobena (300,000), na Pachtec (500,000).

Anabainisha, kutokana na hali hiyo wizara kupitia Bodi ya Tumbaku imefanikiwa kutafuta masoko mengine kuziba pengo la kampuni ya Tanzania Leaf Tobacco TLTC ambayo haijatoa makisio ya uzalishaji msimu huu.




Tangazo la ufunguzi wa soko la tumbaku lilivyokuwa. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

> **"Tayari wakulima wapatao 33,000 wameomba kusajiliwa na Bodi ya Tumbaku kutokana na uzalishaji huo," anasema Hasunga na kuongeza: "Uzalishaji huo ni mdogo na hivyo unaacha wakulima takribani 16,000 bila kulima tumbaku msimu huu."**

"Hivyo, pamoja na asilimia 10 kwa mujibu wa mkataba, jumla ya kilo kwa msimu ujao zitakuwa 63, 278,583.5. kwa muktadha huo, wakulima waliokuwa chini ya kampuni ya TLTC wanahamasishwa waendelee kulima na kutunza tumbaku yao ili kukidhi soko hilo," anasema.

### KISHINDO MSIMU

Waziri Hasunga anasema, wakulima wa tumbaku tayari wameonyesha juhudi zenye hamasa, baada ya kuzingatia maelezo ya wataalam na kufanikiwa kuzalisha kilo 69,757,425 ambayo ni asilimia 121.7 ya malengo katika msimu uliopita, ambayo kwa mujibu wa mikataba, lilikuwa kilo 57,305,127 na serikali ikapata kazi kuhakikisha inawasaidia wakulima kupata soko la kilo 12,452,298 za ziada ya malengo ya mikataba.

Waziri anasema tumbaku iliyonunuliwa mpaka mwisho wa msimu huo wa mwaka 2018/2019 ndani ya mikataba ni kilo 60,691,972.21 zenye thamani ya dola za Kimarekani 92,927,331.79 sawa na asilimia 105.9 ya lengo.

Anabainisha, wizara hiyo kwa kushirikiana na Bodi ya Tumbaku zilifanikiwa kushawishi kampuni ya Alliance One na Premium Active kununua tumbaku kilo 6,305,000, yaani kutoka kilo 4,200,000 hadi 7,400,000.

" Mpaka sasa ununuzi wa tumbaku hiyo iliyozidi malengo ya uzalishaji umefikia kilo 8,107,221 zenye thamani ya Dola za Kimarekani 6,330,174.

Anasema tumbaku iliyobaki kwa wakulima bila mnunuzi ni kilo 3,345,077 zilizozo katika mikoa ya Tabora na kiasi kidogo Ushetu mkoani Shinyanga.

Hasunga anasema ununuzi umekamilika kwa asilimia 100 katika mikoa ya Mbeya, Songwe, Kigoma, Singida, Iringa, Ruvuma na Katavi.

### SOKO JIPYA

Pia, anafafanua wizara yake imefanikisha tumbaku iliyobaki kupata mteja kutoka kampuni mbili za nchini Zambia; Copper Leaf na Tombwe Processing, ambazo tarehe 11 mwezi uliopita zilikubali kununua tumbaku iliyobaki na wahusika wake walio nchini kukamilisha mchakato wa ununuzi unaostahili, kupitia mikataba ya vyama vya msingi vya ushirika.

"Kwa hatua hiyo, tatizo la uwapo wa tumbaku iliyozalishwa nje ya mkataba msimu huu kwa wakulima wa tumbaku litakuwa limekwisha kabisa. Wananchi waendelee kulima mashamba kwa msimu unaokuja," anasema.

Huku akiitaja ilianza kuzalishwa nchini katika zama za ukoloni, Waziri Hasunga anaendelea: "Limekuwa na mchango mkubwa kwa taifa kiuchumi na kijamii, kwani linatoa ajira nyingi na fedha za kigeni."

Hadi sasa mikoa inayolima tumbaku nchini ni: Tabora, Kigoma, Shinyanga, Geita, Kagera, Katavi, Mbeya, Songwe, Singida, Iringa, Ruvuma. Mikoa Morogoro na Mara haina wanunuzi kwa sasa.

Anataja taratibu muhimu za ununuzi ni kwamba, kila mkulima nisharti aingizwe kwenye daftari ya wakulima wa tumbaku, ili asajiliwe na kuondolewa dosari ya kukataliwa tumbaku yake.

Julai mwaka huu, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alipozungumza na wadau wa tumbaku, kutoka mikoa mbalimbali katika mkutano uliofanyika mkoani Tabora, aliahidi serikali ingeendelea kutafuta masoko ya zao hilo.

Alikaririwa kwamba, serikali imeshafanya mazungumzo na nchi mbalimbali hatua ambayo itawawezesha wakulima kuzalisha kwa wingi tumbaku na kuwaongezea kipato.

Waziri Mkuu anabainisha kuwa wakulima wa tumbaku wanakwamishwa mikataba inayowabania kiwango cha uzalishaji, licha ya kuwa na uwezo mkubwa katika uzalishaji.



Mlima tumbaku akiwajibika shambani.

UCHUMI

# Mawaziri SADC waibua maswali utapiamlo chini ya miaka mitano

**Na Michael Eneza**

SUALA la utapiamlo uliokithiri lilikuwa sehemu ya kilichojiri katika mikutano ya wataalamu kando ya mkutano wa wakuu wa nchi wanachama wa Jumuia ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) mwezi Agosti.

Takwimu zilizoibuliwa katika vyombo vya habari na majarida ya uchumi barani Afrika, zilisema kati ya asilimia 35 na 40 ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano, wana utapiamlo sugu unaokaribia kusababisha mtindio wa ubongo wakati wa kuanza shule. Siyo takwimu njema kuainisha mafanikio katika kufikia maendeleo eneo hili.

Suala hili ni muhimu hasa kutokana na mwelekeo wa taasisi za Umoja wa Mataifa za kupima maendeleo halisi katika nchi zinazoendelea, jitihada iliyoanza kama harakati miaka ya 1960 halafu ikapewa kipaumbele miaka ya 1970.

Mwaka 1977 mchumi bingwa wa Pakistan, Mahbubul Akifundisha nchini Marekani, alibuni kielelezo tofauti cha maendeleo akakiita 'Human Development Index,' (HDI) yaani kielelezo cha kupima maendeleo ya watu. Ni tofauti na GDP (Gross Domestic Product) ambayo inaangalia thamani ya uzalishaji bidhaa kwa jumla nchini.

Kielelezo kingine kilionekana kinatosheleza mahitaji ya ziada kuacha GDP, wastani wa pato kwa kila mwananchi, lakini wanaharakati hawakuridhika na kipimo hicho.

Ndipo mchumi huyo akishirikiana na wengine akaunda HDI iliyoanza kuwa muhimu katika takwimu za UN na kila shirika likaanza kubuni takwimu maalum kuainisha nini kinatokea katika eneo hili au lile la ustawi wa jamii na hata ustawi wa uchumi, wakaacha hali ya kutegemea takwimu za jumla kuonyesha ubora au umakini wa maendeleo nchi yoyote.

Ndiyo maana takwimu maalum ya kiwango cha utapiamlo ni tatizo kwa nchi za SADC kwa vile zimekuwa na malengo ya pamoja na mkutano wa kujadili maendeleo kwa jumla, hasa kwa vile SADC iliundwa katika mwelekeo wa kijamii, siyo kibiashara zaidi kama Jumuia ya Afrika Mashariki.

Isitoshe nchi za SADC zina aina fulani ya mshikamano wa jadi unaotokana na historia ya pamoja ya kupigania uhuru na kufikia utawala wa walio wengi. Ilikuwa harakati ya muda mrefu iliyowaleta pamoja ukilinganisha na EAC ambako 'walikutana ukubwani.'

Nchi 16 wanachama wa SADC na Burundi, ndizo zilikuwa zinataka uanachama. Mtawanyiko huo unapunguza hisia ya kulengwa nchi hii au ile katika mijadala ya kiitikadi au kuainisha hali halisi kama ilivyo kwa suala la utapiamlo uliokithiri.

Ndiyo maana suala hili linaweza kuibuliwa na kujadiliwa SADC lakini siyo rahisi kulileta mezani EAC kutokana na hisia kali zaidi za utabaka katika kupima maendeleo, wakati katika SADC kuna hali ya uwazi zaidi. Kwa hiyo hali ya kuthubutu kuangalia takwimu ilijionyesha.




Kikao kimojawapo cha mawaziri wa Jumuiya ya Maendeleio Kusini mwa Afrika (SADC). **PICHA: MTANDAO.**

> **"Suala hilo likishapenya katika hisia za jamii, mjadala ni wazi utaelekea katika suala hilo, jinsi ya kuzuia magonjwa nyemelezi kwa watoto wadogo, kuwa maziwa ya mama ni kinga muhimu, na lile suala pana zaidi la utapiamlo uliokithiri .**

Jitihada hiyo ilileta mchango maalum wa kamati hiyo ya mawaziri wa afya wa kanda, kuangalia mazingira ya ziada ya utapiamlo uliokithiri. Mchango uliotolewa na kamati hiyo ya mawaziri, haukugusa utapiamlo moja kwa moja.

Bali linahusika na watoto katika umri mchanga, hili la kukosa kinga ya kutosha na kuambukizwa kwa urahisi magonjwa nyemelezi. Waliainisha kwa msisitizo unaohitajiwa kuwa watoto wachanga wanakosa lishe ya maziwa ya mama kama kianzio hasa katika miezi sita ya kwanza na inapokuwa kuna udhaifu wa wazi katika kipindi hicho, ya baadaye yanakuwaje?

Ndiyo hapo ikaonekana kuwa kikao cha mawaziri wa afya kimetoa majibu kuhusu takwimu hasi ya utapiamlo wa kutisha miongoni mwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano, kuwa udhaifu huo wa malezi ni chanzo cha matatizo ya jumla ya watoto, hasa wakiwa wachanga.

Wanaoendelea kusikiliza maeneo tofauti ya vyombo vya habari hasa mijadala ya asubuhi wakati watu wanaanza shughuli muhimu za siku, na mara nyingine maofisa waandamizi serikalini wakiwa barabarani wanasikiliza mijadala inasemaje watakuwa wamehisi jambo fulani. Baadhi ya wafuatiliaji na washiriki harakati wameendelea kujiuliza kama jibu hlo linatosheleza.

Kitaaluma au kisaikolojia unaweza kusema kuwa maelezo kuhusu kutumia maziwa ya mama na siyo ya kopo katika kipindi cha uchanga wenyewe ni kama 'kuzima moto' wa takwimu hasi ya utapiamlo uliokithiri.

Ni kuonyesha tatizo la ziada ambalo siyo dogo, na kama lingefanyiwa kazi, kwa kinamama na hasa ambao ni wasomi wa taaluma tofauti na si rahisi kwao kukaa nyumbani bila kazi ya kufanya.

Suala hilo likishapenya katika hisia za jamii, mjadala ni wazi utaelekea katika suala hilo, jinsi ya kuzuia magonjwa nyemelezi kwa watoto wadogo, kuwa maziwa ya mama ni kinga muhimu, na lile suala pana zaidi la utapiamlo uliokithiri lingojeshwe.


Katika chombo cha habari kimoja kilichojadili kwa kina suala hilo, suala la msingi lililoainishwa ni tatizo la utapiamlo siyo la vichanga kabisa, yaani wenye siku chache hadi miezi sita, kipindi ambacho mtoto anategemea maziwa ya mama tu.

Utapiamlo hasa linaanza baada ya miezi sita ambako mtoto anahitaji chakula cha ziada kuacha maziwa ya mama, na hapo ndipo kuna chimbuko la tatizo kuwa mfumo wa jamii wa nini kinapatikana na kinatumikaje kinawaacha watoto wakiwa taabani.

Suala ni uzembe wa kundi la baba katika jamii, kuwa ukiangalia kiasi cha pato la kawaida kinachotumika katika anasa, ni picha ya kutosha ya kuelezea utapiamlo wa watoto, kuwa ni wa mwisho katika matumizi yao.

Siyo rahisi kusema kuwa kamati ya mawaziri wa afya wa SADC ilikuwa na nia ya kuzuia kusutwa kwa wanaume kuwa hawana mpangilio makini katika matumizi yao, kwani anasa ziko katika kila ngazi ya jamii, na mshikamano kuangalia hali ya watoto wadogo ni duni kabisa.

Wakati ambapo si jambo la kushangaza kusikia kuwa hakuna mshikamano kati ya watu ndugu wenye familia tofauti kusaidiana kimaisha, udhaifu wa mshikamano katika familia, na hata kutupa watoto baada ya kuzaliwa, ni matatizo yanayoendana. Kwa vile idadi ya watoto walio katika mazingira hasi ya lishe ni zaidi ya asilimia 30, haielekei kuwa ni wale walioachwa moja kwa moja na baba zao, kuwaacha kina mama wabangaize.



## HABARI MBEYA



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (katikati), akiwa na baadhi ya maofisa wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, wakikagua maeneo ya Ngombe Kusini, katika Kata ya Itezi, juzi, yanayodaiwa kuwa yalitengwa kwa ajili ya viwanda, lakini yamevamiwa na watu waliojenga nyumba za makazi. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Waliovamia viwanda waamriwa kubomoa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amewataka wananchi wote wanaodaiwa kuvamia eneo la viwanda na kujenga makazi yao katika Mtaa wa Gombe Kusini Kata ya Itezi jijini Mbeya kuvunja nyumba zao kabla hawajachukuliwa hatua.

Chalamila alitoa agizo hilo juzi alipotembelea eneo hilo pamoja na baadhi ya viwanda vilivyopo katika eneo hilo ambapo aliambiwa na maofisa ardhi na mipango miji wa Jiji hilo kuwa baadhi ya wananchi hao ni wavamizi na wamejenga makazi ya kudumu.

Alisema baadhi ya maeneo hayo yameanza kuendelezwa na wenye viwanda, lakini wengine wanashindwa kwa sababu ya uwepo wa nyumba hizo.

Alisema baadhi ya watu hao wanatumia njia za kijanja kwenda mahakamani kwa ajili ya kuikwamisha serikali kutekeleza mipango yake na kwa kutumia baadhi ya wanasheria, hivyo akawatahadharisha kuacha tabia hiyo mara moja.

"Hatuko tayari kuingilia mahakama ila tuko tayari kuendelea na kazi zetu kama ambavyo mihimili mingine inaendelea na kazi zao, kwa hiyo wale wote waliovamia eneo lenye hati miliki kwa ajili ya viwanda, waanze kutupisha wenyewe kuanzia leo," alisema Chalamila.

Alisema eneo hilo haliwezi kutolewa hati kutokana na kuwapo kwa hati nyingine ambayo ni maalumu kwa ajili ya viwanda, hivyo alisema watu hao hawana haki ya kukaa mahali hapo.

Akitoa taarifa ya eneo hilo, Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi na Mipango Miji wa Jiji la Mbeya, Peter Msilanga, alisema eneo hilo lilipimwa miaka ya 1980 na lilitengwa kwa ajili ya viwanda lakini limevamiwa.

Alisema eneo hilo lipa katika Kitalu namba BB Uyole, na kwamba wananchi waliojenga nyumba zao kwenye eneo hilo hawana vibali vilivyotolewa na serikali na hivyo ni wavamizi.

Alisema idadi ya nyumba hizo ni kubwa, na baadhi zipo kwenye maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kupitisha barabara na hivyo kulifanya eneo hilo kutokuwa rafiki kwa wawekezaji wa viwanda ambao wanataka kuwekeza.

"Watu hao wanawazuia wawekezaji kuendeleza maeneo yao kitu ambacho sasa hata sisi tunapata shida, idadi kamili ya nyumba hizo bado mpaka tutakapozihesabu," alisema Msilanga.

Hata hivyo baadhi ya wananchi waliojenga nyuma zao kwenye eneo hilo walidai wana vibali vilivyotolewa na Idara ya Ardhi ya Jiji la Mbeya na hivyo wanashangaa kuambiwa kuwa ni wavamizi.

Mmoja wa wananchi hao ambaye hakutaka kutaja jina lake, alisema walinunua maeneo hayo kutoka kwa wenyeji waliokuwa wanayamiliki kama mashamba na wakalipia asilimia za mapato serikalini.

Alisema pamoja na kwamba wanadaiwa kuwa ni wavamizi, lakini wanalipa kodi za nyumba ambazo zinakusanywa kila mwaka na Mamlaka ya Mapato (TRA).

# Wapuuza sheria kuwabana wanaopata mimba shuleni

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATETEZI wa Haki za Binadamu mkoani Mbeya, wamesema hakuna sababu ya serikali kutunga sheria ya kuwaadhibu wanafunzi wa kike wanaowashawishi wanaume kuwatia mimba kwa madai kuwa kundi hilo linapitia katika madhira mengi.

Walitoa kauli hiyo juzi kwenye maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia yaliyoandaliwa na Mtandao wa Mashirika yasiyokuwa ya kiserikali yanayotoa msaada wa kisheria nchini (Tanlap) yaliyoambatana na utoaji wa elimu ya ukatili wa kijinsia. Mmoja wa watetezi hao, Leticia Petro, alisema mtoto wa kike anapopata mimba anapoteza haki yake ya kuendelea na masomo na hivyo kutunga sheria ya kumwadhibu ni kumwongezea maumivu.

Alisema kwa sasa serikali inatakiwa kuendelea kutumia sheria zilizopo ambazo zinawabana wanaume mpaka pale itakapojiridhisha kuwa watoto wa kike wamelelewa katika maadili mema lakini bado wanayakiuka.

Leticia alikiri kuna uwezekano mkubwa wa mtoto wa kike kumshawishi mwanaume kumtia mimba, lakini akaeleza kuwa yawezekana matukio hayo yanatoke kutokana na kutokuwa na maadili mema.

"Bunge letu pamoja na jamii yetu tutakapoona kuwa kuna umuhimu wa kutungwa kwa sheria hiyo itatunga, lakini sio kwa wakati huu sio muda mwafaka mtoto wa kike aliyepata mimba kufungwa gerezani kama ilivyo kwa mtoto wa kiume," alisema Leticia.

Ofisa Mradi wa Mashirika yanayotoa huduma ya msaada wa kisheria nchini, Msheleri Machumbana, alisema, Tanzania haina chombo maalumu cha kushughulikia ukatili wa kijinsia hali ambayo inasababisha vitendo hivyo kuendelea kushamiri kwenye jamii.

Alisema kila mdau anafanya jukumu hilo kwa nafasi yake ikiwamo Jeshi la Polisi, Wizara ya Afya na wadau wengine hali ambayo alidai inaleta changamoto wakati mwingine katika kushughulikia suala hilo.

Alisema chombo hicho kinaweza kikaundwa kama ilivyo kwa vyombo vingine kama, Tume ya Kupambana na Dawa za Kulevya, Tume ya Kupambana na Maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (Tacaids), pamoja na vyombo vingine.

Hata hivyo, baadhi ya wadau waliikosoa Sheria inayowahukumu wanaume pekee kwenye makosa ya ukatili wa kijinsia wakidai kuwa inasababisha matatizo mengine ikiwamo kujenga uhasama miongoni mwa familia zinazohusika.

# Waomba barabara ya Mbeya-Songwe

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATUMIAJI wa barabara inayounganisha Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na Wilaya ya Songwe, wameiomba serikali kuiboresha barabara hiyo kwa madai ni hatari kwa maisha yao pamoja na vyombo vya moto.

Wanadai barabara hiyo imeharibika kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha, hali ambayo inawafanya watumie muda mrefu kutoka Mkwajuni yalipo Makao Makuu ya Wilaya ya Songwe mpaka Mji wa Mbalizi.

Walipaza kilio chao walipokuwa wanazungumza na Nipashe katika eneo la Ndiwi Kata ya Mshewe ambapo mabasi yote yalishindwa kupita kutokana na lori lililokuwa limebeba shehena ya mbole kukwama.

Mmoja wa madereva wa mabasi hayo, Steven Manyama maarufu kwa jina la 'Ngosha', alisema maeneo yenye changamoto kubwa ni kuanzia Garula mpaka Utengule ambapo alisema kuna makorongo mengi.

Alisema wakati mwingine kuwa wanalazimika kuwashusha abiria ili kupunguza uzito na kwalazimu abiria kuanza kusukuma magari hayo ili kuyakwamua kutoka kwenye matope.

"Kwa mfano hapa Ndiwi hatuwezi kupita kwa sababu hakuna njia nyingine mbadala ya kupita, ni lazima tushirikiane wote kuliondoa hili lililokwama ili tupite, ukitaka kupita pembeni kuna tope ambalo linaweza likasababisha matatizo zaidi," alisema Ngosha.

Alidai kuna mabasi mengine yalikuwa yamekwama katika eneo la Garula ambapo moja ya mabasi hayo lilikuwa limekwama kwenye tope hivyo akaiomba serikali kuchukua hatua haraka kabla wenye magari hawajaamua kuziondoa gari zao.

Naye mmoja wa abiria wa magari hao, Fredrick Vungwa, alisema barabara hiyo ni muhimu kwa sababu inaunganisha wilaya mbili ambazo ni muhimu kwenye uzalishaji wa mazao mbalimbali ikiwamo tumbaku na mahindi.

Alisema hata watumishi wa Halmashauri hiyo wanatumia barabara hiyo wanapoenda katika Mji wa Vwawa yalipo Makao Makuu ya Mkoa wa Songwe na hivyo bila kuiboresha itakuwa inakwamisha baadhi ya huduma.

Vungwa alisema hata huduma nyingi za matibabu hasa hospitali za rufani zinapatikana Mbeya na Mbozi hivyo endapo mtu akapatiwa rufani ya kuelekea huko kutoka Mkwajuni inaweza ikawa shida.





# Waliokwamisha maelfu ya leseni madini kuhamishwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imemwagiza Meneja wa Utawala na Rasilimali Watu Tume ya Madini, Gifti Kilimwomeshi, kuhakikisha watumishi watano wa Idara ya Leseni na Tehama makao makuu wanahamishiwa mkoani Tabora ndani ya siku tano kutokana na kufanya mgomo uliosababisha maombi ya leseni 3,410 kukwama.

Hayo yaliainishwa na Waziri wa Madini, Dotto Biteko, jijini hapa wakati akizungumza na waajiriwa wapya 116 wa tume hiyo ambao wameripoti na kupewa mafunzo kwa ajili ya kupangiwa vituo vya kazi .

Tukio hilo lililambatana na uzinduzi wa magari 10 yaliyotolewa na serikali kwa ajili ya kazi mbalimbali.

Alisema, watumishi hao waliweka mgomo baridi na kusababisha mapato ya mwezi Oktoba na Novemba kushuka kutokana na mgomo huo uliosababisha leseni 3,410 kukwama huku wananchi wakibaki kulalamika.

Waziri alisema tume ilichukua watumishi wanne kutoka Tabora na kuwaleta jijini Dodoma kuja kufanya kazi wakati makao makuu kuna watumishi katika Idara hiyo ya leseni kisha wameweka mgomo baridi.

“Kwa serikali ya sasa hilo haliwezekani na halikubariki kila mmoja anapaswa kufanya kazi alipopangiwa,” alisema Biteko.

“Wananchi wanalia kuna watu wanaweka mgomo baridi na kuacha kufanya kazi, sasa naagiza wahamishwe wapeleke Tabora na wale wa Tabora waje hapa makao makuu wapige kazi kwa kuwa mliwaleta na wakapiga kazi na tija ikaonekana, msitaka tuonekane ni wizara ya kushughulikiana, nanyi msitushughulikie,” alisema Biteko.

Aidha, aliitaka tume kujiangalia maana wamepata ugonjwa mpya wa kutaka kufanya kazi mpaka walipwe posho, utaratibu wanaoutumia kudai haufai na wakitaka kuutumia wakautafutie mahali pengine na si Wizara ya Madini.

Biteko aliagiza mchakato wa kuhamisha watumishi hao wanne ambao wanastahili kuhamishiwa makao makuu ya tume Dodoma kuwa umekamilika ifikapo Desemba 9, mwaka huu mchakato huo uwe umekamilika. Pia alimwagiza Katibu Mtendaji wa Tume, Prof. Shukrani Manya, kufanya upya mapitio ya wakuu wa idara kwa lengo la kuimarisha utendaji wa tume hiyo.

Biteko aliwataka waajiriwa wapya kufanya kazi kwa kuzingatia kanuni, sheria, taratibu na kutenda haki kwa kuepuka vitendo vya rushwa ukizingatia kuwa watu wanaokwenda kuwahudumia wanamaneno mengi na majungu hivyo wasipokuwa makini watawaharibia kazi.

Aliwataka kujifunza kupitia sheria ya madini kuisoma kwa makini na kuifahamu vyema.

Biteko alitoa onyo kwa maofisa wa madini wa kanda wenye tabia ya kutegesheana kusaini madokezo jambo ambalo linachelewesha, ambapo amemwagiza katibu mkuu kufikisha taarifa kwa RMO wa aina hiyo ambaye hakutaka kumtaja jina lake, kwamba hiyo ni nafasi ya mwisho asirudie.

Prof. Manyama alisema, wamepokea watumishi wapya 116, ambao watapangiwa vituo vya kazi baada ya mafunzo hayo.



Mwendesha bodaboda akivunja sheria za usalama barabarani, kwa kupakia abiria watatu maarufu kama mshikaki, huku wote wakiwa hawajavaa kofia ngumu kichwani, katika kijiji cha Mondo, Wilaya ya Chemba, mkoani Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mahenge awaagiza maofisa ustawi jamii

**Na Peter Mkwavila,** KONDOA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, amewaagiza maofisa ustawi wa jamii kutochelewesha mikopo itokanayo na mapato ya ndani ya halmashauri inayoombwa na makundi maalumu ya watu wenye ulemavu.

Agizo hilo lilitolewa na Mkuu wa Wilaya ya Kondoa, Sezeria Makota, alipokuwa akizungumza na wananchi kwa niaba ya mkuu wa mkoa kwenye Maadhimisho ya Siku ya Watu wenye Ulemavu Duniani yaliyofanyika kimkoa wilayani Kondoa.

Dk. Mahenge alisema hayo kutokana na kilio cha Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Mkoa wa Dodoma (SHIVYAWATA) kudai kukwamishwa na maofisa ustawi ya jamii wa halmashauri za wilaya na jiji mikopo hiyo na maombi yao kutopatiwa kwa wakati.

Alisema kutokana na madai hayo ya makundi ya watu wenye ulemavu amewaagiza maofisa hao kuhakikisha wanatatua changamoto hiyo ili kuwawezesha kupata mikopo ili kutekeleza miradi yao na kuondokana na kuwa ombaomba.

“Napenda niwaagize maofisa ustawi wa jamii wote katika mkoa, waache kukwamisha mikopo hiyo ya asilimia mbili inayotolewa na halmashauri kwa ajili yao ili kuwawezesha kufanya shughuli za maendeleo na watu waache kuwaondoa kama vile kazi zao ni ombaomba tu,” alisema.

Awali akisoma mapendekezo yao kwa kupitia risala yao kwenye maadhimisho hayo Katibu wa Shivyawata Mkoa wa Dodoma, Justus Ng'wanmtalima, alimwomba mkuu wa mkoa kuwatumia watendaji wa serikali waliopo vijijini na mitaa ili kupata takwimu sahihi za watu wenye ulemavu.

Alisema kuwa hali hiyo itarahisisha upatikanaji wa mipango itakayoakisi mahitaji halisi ya watu wenye ulemavu wa aina yote.

Aidha, mapendekezo mengine pamoja na kuziomba taasisi zinazotoa huduma kwa umma ziwasomeshe wafanyakazi wao lugha ya alama ili watoe huduma ya mawasiliano kwa viziwi.

Mapendekezo mengine ni serikali za mitaa kuanzia ngazi ya vijiji, mitaa hadi halmashauri zizingatie ushiriki wa watu wenye ulemavu katika kuandaa bajeti ikiwa pamoja na kuhakikisha makundi hayo yanajumuishwa kwenye kamati za ushauri za wilaya.

# Sokoni wafundwa uchaguzi viongozi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

OFISA Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna, amewataka wafanyabiashara wa soko la samaki wabichi, matunda na mboga la Bonanza, kuchagua viongozi wabunifu wa miradi itakayowaongezea mitaji yao.

Alisema wafanyabiashara wanatakiwa kutowachagua viongozi wao kwa ushabiki ambao wanaweza kuleta matokeo ya kuchochea migogoro na kusababisha mgawanyiko kati yao na uongozi wa jiji.

Tahadhari hiyo ilitolewa na ofisa huyo alipokuwa akizungumza kwenye mkutano wa wafanyabiashara hao ulioitishwa kwa ajili ya maandalizi ya kuwachagua viongozi.

Akizungumza kwenye mkutano huo wa wafanyabiashara, aliwataka kuchagua pia viongozi wenye kutumia hekima na busara kwa lengo la kulisaidia soko hilo na wao wenyewe kiutendaji.

“Wengi watajitokeza kutaka wachaguliwe kwenye soko hili, kinachotakiwa kwenu nyinyi wafanyabiashara muwachague wenye kubuni miradi ili muongeze mitaji yenu na siyo kwa kuwachagua kwa ushabiki unaoweza kuhatarisha maisha yenu na biashara zenu,” alisema.

Hata hivyo aliwataka wafanyabiashara wanao jishughulisha na uuzaji wa samaki wabichi kuweka mazingira safi kwenye maeneo yao wanayofanyia biashara, ili kuepukana na magonjwa ya mlipuko ambayo yatatokea katika kipindi hiki cha mvua za masika.

Mwenyekiti wa soko hilo anayemaliza muda wake, Goya Magwai, alisema pamoja na changamoto nyingi zilizopo, lakini bado wanayo sababu ya kuishukuru serikali kutokana na juhudi zake ambazo hivi sasa zimeanza kuonekana.

Alisema changamoto ambazo zimeanza kutatuliwa ni pamoja na miundombinu ya mitaro, vyoo na ujenzi mkubwa unaoendelea wa eneo la kuuzia samaki wabichi ambalo litakuwa na uwezo wa kuhifadhi pindi watakapobaki.

Naye Diwani wa Chamwino, Jumanne Ngende, alisema atashirikiana na jiji kuhakikisha kero zilizobaki zinatatuliwa ili kuendana na hali halisi ya makao makuu ya serikali.

Aidha, aliwataka viongozi watakao chaguliwa moja ya majukumu wanayotakiwa kuyafanya ni kuunga mkono juhudi za serikali zinazotekelezwa sokoni hapo pamoja na kuhakikisha kujiepusha na migogoro.



# Ofisa vibali mbaroni kwa madai ya rushwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SIKU chache baada ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA), kumnasa daktari wa hospitali ya serikali kwa madai ya kuomba rushwa ya ngono kwa mgonjwa, mamlaka hiyo jana imemnasa ofisa mwenye dhamana ya utoaji vibali vya kazi kwa wafanyakazi wa nje ya nchi kwa tuhuma za kuomba rushwa ya Sh. milioni moja.

Ofisa huyo aliyetambuliwa kwa jina la Khamis Ali Omar, ni mfanyakazi wa Serikali ya Zanzibar.

Akizungumza na waandishi wa habari, Ofisa Uchunguzi wa ZAECA, Moza Mtumwa Faki, alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa majira ya saa sita za mchana juzi ofisini kwake Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Mwanakwerekwe Mjini Unguja.

Alisema mamlaka ilipokea malalamiko kutoka kwa mmoja wa waajiri sekta binafsi ambaye hakumtaja jina akieleza kufika ofisini kwa mtuhumiwa huyo kwa ajili ya kuomba vibali vya kazi ili aweze kuajiri wafanyakazi wa kigeni katika kampuni yake, lakini alitakiwa kutoa rushwa ili kupatiwa vibali hivyo.

Moza alisema baada ya mamlaka kupokea taarifa hiyo walipanga na mlalamikaji akubali kutoa fedha hizo ili kumnasa mtuhumiwa huyo.

"Baada ya kukubaliana na mlalamikaji tulimkabidhi fedha hizo Sh. milioni moja ambazo tayari tumeziwekea alama ya mtego, alizichukua na kwenda kumkabidhi mtuhumiwa huyo baada ya kumkabidhi nasi tulifika na kumtia hatiani kwa tuhuma za kupokea rushwa," alisema.

Alisema mtuhumiwa huyo hivi sasa yupo chini ya mamlaka hiyo kwa ajili ya mahojiano maalum ya kiuchunguzi, ili aweze kufikishwa katika vyombo vya sheria kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria.

"Sisi ZAECA tupo macho muda wote na tupo tayari kutoa ushirikiano wetu wakati wowote, kubwa tunawaomba wananchi nao kuwa tayari kuwafichua waombwa rushwa wote, lengo ni kuona haki inapatikana bila ya kutoa rushwa kama ilivyo sheria ya nchi," alisema.

# Wanaovuna asali kwa kuchoma nyuki waonywa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAFUGAJI wa nyuki visiwani Zanzibar wamepigwa marufuku kuvuna asali kwa njia ya kizamani ya kuchoma moto ambayo huwateketeza.

Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Dk. Makame Ali Ussi, alipiga marufuku hiyo wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Ziwani Pemba, Suleiman Ali Makame, aliyetaka kujua hatua zinazochukuliwa na serikali kukabiliana na watu wanaovuna asali kwa kuteketeza nyuki.

Dk. Ussi alisema kitendo hicho ni uharibifu wa mazingira kwa wavunaji asali kuchoma moto nyuki wakati wakiwa katika harakati za kugema (kuvuna) asali. Alisema matukio kama hayo athari zake kubwa zimeonekana ikiwamo baadhi ya misitu kuteketea kutokana na tabia ya wafugaji kuchoma moto wakati wakigema asali.

"Haikubaliki ni kitendo cha uharibifu wa mazingira wakati nyuki akiwa anahitajika kwa ajili ya kuzalisha asali watu wanawateketeza kwa kuwachoma moto," alisema.

Alisema wameanza kutoa mafunzo kwa wafugaji kuhusu njia sahihi za kuvuna asali bila ya kusababisha madhara ya kuua nyuki.

Alisema jumla ya wafugaji nyuki 700 wamepatiwa elimu ambayo itawawezesha kuvuna asali kwa njia za kisasa bila ya kuharibu mazingira.

Pia alisema jumla ya vikundi 250 vimepatiwa mizinga ya kibiashara kwa ajili ya ufugaji.

"Vikundi vya wafugaji asali vingi tumevipatia mafunzo juu ya kuvuna asali kwa kuzingatia mazingira na uhifadhi wake... sioni sababu ya kuchoma nyuki wakati wa kuvuna asali," alisema.

Dk. Ussi aliwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba shughuli za kufuga kwa ajili ya kuzalisha asali imeanza kuleta matunda mazuri kwa wananchi wa Unguja na Pemba ikiwamo kujitokeza vikundi vingi kwa ajili ya kazi hizo.



Mwakilishi wa Jimbo la Mkwajuni, Ussi Yahya (kushoto), akisikiliza kwa makini taarifa mbalimbali wakati wa kikao cha Baraza la Wawakilishi, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Zanzibar haijapata vifaa vya usikivu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Afya ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, imesema hadi sasa hakuna vifaa vya huduma za upandikizaji wa usikivu ambavyo hutumiwa na watu wenye matatizo ya kutosikia vizuri.

Naibu Waziri wa Afya, Harusi Said Suleiman, alisema hayo wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Konde, Omar Seif Abeid, aliyetaka kujua kuhusu matibabu ya upandikizaji wa vifaa vya usikivu kama huduma hizo zinapatikana katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Alisema wizara inaendelea na mazungumzo na baadhi ya taasisi za afya ziliopo China kuanza kutoa huduma kama hizo.

Alisema huduma hizo ni muhimu kwa sababu baadhi ya nchi jirani ikiwamo Tanzania Bara, zimeanza kupatikana kwa wagonjwa wanaohitaji matibabu hayo. "Wizara inaendelea na mazungumzo na baadhi ya taasisi ziliopo China juu ya uwezekano wa kuanzisha huduma za upandikizaji vifaa vya matibabu ya usikivu kwa wananchi wa Unguja na Pemba," alisema.

Hata hivyo, alisema katika Hospitali ya Mnazi Mmoja zipo huduma mbalimbali zinazotolewa katika kitengo cha masikio, pua na macho. Alisema wagonjwa wenye matatizo ya usikivu hupatiwa matibabu na hatua ya awali katika Hospitali ya Mnazi Mmoja iliyopo Unguja pamoja na Abdalla Mzee ya Pemba.

# Wenye ulemavu bado wakosa taarifa za afya

**Na Mary Geofrey**

WAKATI dunia ikiadhimisha siku ya watu wenye ulemavu Disemba 3 kila mwaka, nchini watu hao bado wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo ya kupata taarifa za afya.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Peace Life For People With Disability (PLPDF), Sophia Mbeyella, aliyasema hayo wakati akizungumza na Nipashe katika ofisi za Kampuni ya The Guardian, juzi jijini Dar es Salaam, alipokuwa katika ziara ya kuelezea maadhimisho ya siku hiyo.

Alisema licha ya Serikali kutekeleza sera ya elimu jumuishi, bado sekta ya afya haijazingatia kuwa na wataalam wenye uelewa wa kuwasilisha taarifa muhimu kwa kundi la watu wenye ulemavu.

"Tumekuwa tukiona taarifa muhimu kama za afya ya uzazi, Ukimwi na magonjwa mbalimbali zinatolewa bila kuzingatia kundi hili, kwa sababu watoa taarifa au watoa huduma za afya hawana uelewa kuhusu namna ya kuwasilisha taarifa hizo kwa watu wenye ulemavu hasa wa kusikia," alisema Sophia.

Alisema kutokana na changamoto hiyo baadhi ya walemavu hupata ujauzito katika umri mdogo, kutochukua tahadhari za magonjwa mbalimbali.

Aidha, alisema sekta ya elimu kundi la walemavu linakabiliwa na changamoto ya miundombinu rafiki ikiwamo ya vyoo na vitabu nundu kwa walemavu wa macho.

"Serikali imesaidia elimu inatolewa shuleni bila kubagua wenye ulemavu lakini changamoto kubwa ni miundombinu rafiki kwa wenye ulemavu na vifaa vya kufundishia," alisema Sophia.

Alisema mbali na changamoto hizo, pia vifaa kama miguu bandia na visaidizi vya kutembelea vinauzwa kati ya Sh. milioni nne hadi sita fedha ambazo walemavu hawawezi kumudu.

Sophia anatumia fursa hiyo kuitaka Serikali kupunguza kodi za vifaa hivyo vinavyotoka nje ya nchi ili kuwapunguzia mzigo watu wenye ulemavu.

"Tunaiomba Serikali ikiwezekana kuondoa kabisa kodi ya vifaa hivi kama siyo kupunguza kodi. Kutokana na vifaa hivyo kuuzwa bei ya juu, walemavu wamekuwa wakikaa barabarani kuomba fedha za kujikimu badala ya kufanya kazi," alisema Sophia.

Kuhusu maadhimisho hayo, alisema wanayatumia kutoa elimu kwa jamii, wazazi na walezi kutobagua kundi hilo na jamii kwa ujumla kuwapa kipaumbele katika shughuli mbalimbali za maendeleo nchini.

Sophia pia aliwataka watu wenye ulemavu kujiamini na kujikubali ili waweze kushiriki katika shughuli mbalimbali za kuwaletea maendeleo badala ya kulalamika.

Alisema kauli mbio katika maadhimisho hayo inasema 'Kuhamasisha ushirikishaji kwa watu wenye ulemavu katika uongozi chukua hatua kuelekea maendeleo endelevu ya dunia 2020/30.

"Kauli mbiu hii inahamasisha jamii kuwakubali watu wenye ulemavu hasa wakati wa kuelekea uchaguzi mkuu wa 2020, wamepewa nafasi wanaweza," alisema Sophia.



With Disability (PLPDF), Sophia Mbeyella, akifafanua jambo, katika mahojiano na gazeti hili, jijini Dar es Salaam, mapema wiki hii. **PICHA: JOHN BADI**

# Ufaransa kutoa fursa ya elimu Afrika

**Na Beatrice Shayo**

BALOZI wa Ufaransa nchini Tanzania, Frederic Clavier, amesema Serikali ya Ufaransa inalenga kuwapa elimu wanafunzi wengi zaidi wa kimataifa hasa kutoka Afrika kwa zaidi ya 200 za Kiingereza.

Balozi Clavier alisema hayo juzi jijini Dar es Salaam katika hafla ya 'Chagua Ufaransa' kuadhimisha mtandao wa Alumni wa Ufaransa nchini Tanzania baada ya kuzinduliwa rasmi Juni, mwaka huu.

"Tunataka kudumisha taalumu yetu kama nchi kubwa ya mwenyeji na uwezo wake wa kuvutia wanafunzi bora katika taasisi zake, iwe ni kutoka Afrika, Asia au Amerika. Ufaransa inafahamu taaluma zote za kiwango cha juu za Kitanzania ambazo zitaleta baraka katika mitaala ya kimataifa ya vyuo vikuu vingi mashuhuri na shule," alisema.

Alisema Serikali ya Ufaransa mwaka huu imefadhili wanafunzi 30 kufuata masomo katika vyuo vikuu tofauti vya Ufaransa na inatoa asilimia 20 (Euro 10,000) ya bajeti yake ya kitaifa kila mwaka ili kusaidia elimu.

Pia, alisema watu walichagua kusoma nchini Ufaransa kutokana na sababu kadhaa ikiwamo utamaduni na lugha ya Kifaransa.

Alisema Ufaransa imechaguliwa kuwa lugha rasmi ya watu milioni 200 wanaozungumza katika mabara matano.

Kuzungumza Kifaransa kunatoa fursa nzuri ya kufikia zaidi ya nchi 47 ulimwenguni.

Alisema Rais Emmanuel Macron, ameweka lengo la kufikia wanafunzi wa kimataifa wa 500,000 kila mwaka kuanzia mwaka 2017. Hivi sasa, kuna wanafunzi 7,000 wa kigeni wanaosoma nchini Ufaransa.

"Ufaransa ndiyo nchi ya nne kubwa mwenyeji wa wanafunzi wa kimataifa ulimwenguni baada ya Amerika, Uingereza na Australia," alisema Balozi.

Vile vile, alisema wameandaa halfa ya kwanza ya elimu ya juu ya Ufaransa na Tanzania itakayofanyika Dar es salaam wiki ijayo kwa vyuo vikuu 10 vya Ufaransa na vyuo vikuu vya Tanzania vitashiriki.

Alumni na wanachama wa sekta binafsi watakutana na wawakilishi tofauti wa vyuo vikuu vya Ufaransa na Tanzania kupata fursa za kitaaluma na udhamini wa masomo.

Mwakilishi wa wanafunzi, Salvius Duwe, alisema yeye alipata ufadhili na kwenda kusoma nchini Ufaransa na elimu yao ni nzuri, hivyo anaamini taaluma aliyoipata itaitumia ipasavyo pamoja na kuwaelimisha wengine.

Alisema wanafunzi wa Kitanzania wakienda nchini Ufaransa watajifunza mambo mbalimbali kwa kuwa nchi hiyo imeendelea na ina viwanda vingi, watapata ujuzi na kuisaidia Serikali ya Tanzania kuinua uchumi hususani kilimo, uhandisi na utamaduni.

Mhadhiri Mwandamizi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Colman Msoka, alisema wana uhusiano na chuo kikuu cha Ufaransa tangu mwaka jana na wamepata fursa ya wanafunzi wao kupata taaluma nchini huko.

Alisema wazazi na wafadhili wanaopenda kuwapeleka watoto kusoma nje ya nchi ni vizuri wakaangalia nchi ya Ufaransa ili waweze kujifunza lugha hiyo ambayo ni muhimu.

# Wakulima watakiwa kubadilika kifikra

**Na Gurian Adolf,** KALAMBO

WAKULIMA mkoani Rukwa wametakiwa kubadilika na kuacha mazoea ya kununua pembejeo za kilimo wakati wa kuanza msimu wa kilimo ili kupunguza malalamiko ya uhaba wa bidhaa hiyo.

Ofisa Kilimo wa Mkoa huo, Okram Chengula, aliyasema hayo juzi wakati Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo, akizindua kilimo katika mashamba ya wakulima wa Kijiji cha Kalalasi wilayani hapa.

Alisema wakulima wengi wamekuwa hawana utaratibu wa kuandaa pembejeo mapema na kutafuta taarifa za maeneo yanayopatikana pembejeo ndiyo maana wanalalamikia kuwapo kwa uhaba wa pembejeo.

Chengula alisema kuwa pembejeo za kilimo zipo za kutosha mkoani Rukwa na zinauzwa kwa bei elekezi ya serikali, lakini wengi wao hawajui na badala yake wamekuwa wakilalamika kuwa hazipatikani.

"Naomba niwashauri wakulima kuwa na utaratibu wa kununua pembejeo za kilimo mapema kabla ya msimu wa kilimo au kutafuta taarifa za upatikanaji wake. Kinyume cha hapo mtaendelea kulalamikia uhaba wa pembejeo," alisema.

Ofisa huyo alisema serikali ya Mkoa wa Rukwa imehakikisha pembejeo za kilimo ambazo ni mbegu bora, mbolea na dawa za kilimo, zinapatikana katika kipindi chote cha mwaka ili mkulima anunue kila anapohitaji na si kusubiria mpaka msimu wa kilimo uanze.

Kwa upande wake, Angabo aliwataka wakulima kufuata taratibu za kilimo bora ili kupata mavuno ya kutosha kwa kuwa mvua zimeanza kunyesha na ni za kutosha.

Alisema katika msimu uliopita mavuno kwa mazao yote yalikuwa 8,000,094 lakini mwaka huu malengo ni kuzalisha tani 700,000 za mahindi peke yake.

Naye mmoja wa wakulima, Maria Maeka, alisema msimu huu wa kilimo unaonekana utakuwa na neema kwa kuwa mvua zinanyesha vizuri, hivyo ni jukumu lao wakulima kuongeza juhudi ili wapate mavuno ya kutosha na wafikie malengo ya serikali.

# Marekani yafufua uhusiano na Sudan

**KHARTOUM, Sudan**

MAREKANI imefufua uhusiano na Sudan kwa kumuunga mkono Waziri Mkuu wa mpito, Abdallah Hamdok, anaendelea na ziara nchini humo kuomba vikwazo dhidi ya nchi yake visitishwe kwa kuunga mkono ugaidi.

Ziara hiyo ya Waziri Mkuu wa mpito wa Sudani nchini Marekani ni ziara ya kihistoria.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo, alisema Marekani na Sudan zimeamua kuanza mchakato wa kubadilishana mabalozi baada ya kuvunjika kwa uhusiano kati ya nchi hizo mbili kwa muda wa miaka 23.

Hivi karibuni balozi wa Marekani atateuliwa huko Khartoum.

"Uamuzi huu ni hatua muhimu katika kuimarisha uhusiano wa nchi hizi mbili, Sudan na Marekani, haswa wakati huu ambapo serikali ya mpito inayoongozwa na raia inafanya mageuzi makubwa," alisema Mike Pompeo.

Uhusiano kati ya nchi hizo mbili ulikuwa umedorora kabisa kwa kipindi cha miaka 30 ya utawala wa Omar al-Bashir, aliyepinduliwa madarakani kufuatia kutokea kwa maandamano makubwa.

Tangu mwaka 1993, wakati Rais Bashir alipompokea kiongozi wa mtandao wa Al-Qaeda, Osama bin Laden, Sudan iliwekwa kwenye orodha nyeusi ya mataifa yanayounga mkono ugaidi.

Mwaka 1998, baada ya mashambulizi makubwa ya Al-Qaeda dhidi ya balozi za Marekani nchini Kenya na Tanzania, Washington iliendesha mashambulizi ya anga nchini Sudan.

Tangazo la kufufua uhusiano kati ya Sudan na Marekani linakuja wakati Waziri Mkuu wa mpito anaendelea na ziara yake Washington.

Ni mara ya kwanza tangu mwaka 1985 kiongozi wa Sudan kupokelewa na maofisa wa serikali ya Marekani katika mji mkuu wa Marekani.

Juzi, Abdallah Hamdok alikutana kwa mazungumzo na Waziri wa Fedha wa Marekani, Steven Mnuchin, ambaye alikaribisha nia yake ya mageuzi na akasisitiza kuhusu vita dhidi ya utakatishaji fedha na ufadhili wa ugaidi.

**RFI**

# Mahari yaondolewa baada ya wanaume kususa kuoa

**LAGOS, Nigeria**

MAMLAKA nchini Nigeria imesitisha uamuzi wa kuwakata kodi wananchi wanaoishi Kaskazini mwa nchi hiyo pindi wanapooa, baada ya wanaume wa maeneo hayo kususa kuoa.

Uamuzi huo ulianza baada ya Ado Sa'id, ambaye ni chifu wa kijiji cha Kera kaskazini magharibi mwa Nigeria, kutangaza kuwa kila mwanaume atakayetaka kuoa atapaswa kulipa kodi ya kiasi cha dola 375 za Kimarekani.

Hii ikiwa ni mbadala wa utamaduni ambao uliopo wa kulipa samani, vyombo vya jikoni na vitu vingine vya thamani kwa ajili ya kutoa kwa familia ya bibi harusi watakapofunga ndoa.

Kiongozi huyo alisema kuwa kulipa kodi ni rahisi zaidi kuliko kulipa mahari na itawafanya watu wengi kufunga ndoa kirahisi.

Amri hiyo iliwafanya wanaume wa eneo hilo kushindwa kufunga ndoa, huku wengi wao wakisusia kuoa.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kano, Maigida Adamu, alisema kuwa chifu alifanya makosa kwa kuanzisha kodi hiyo.

"Hakutuuliza kabla ya kutangaza kuanzisha kodi hiyo. Hivyo kuanzia sasa nimesitisha utaratibu huo na kuunda kamati ya watu saba kuangalia hatua ambayo chifu atachukua," alisema Adamu.

Isah Yusuf, ambaye ni mkazi wa kijiji hicho alifurahia uamuzi uliotolewa na kusema kuwa jamii ilipinga kabisa jambo la kulipia kodi ndoa.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa hakuna mtu ambaye ameoa katika kijiji hicho na sasa miezi minne imepita tangu chifu Ado Sa'id, alipoweka malipo ya kufunga ndoa na kusitisha watu kupeleka vitu vya samani.

Chifu huyo alisema kuwa kulipa kodi ni rahisi zaidi na itawarahisishia watu wengi kufunga ndoa.

Mwanakijiji mwingine, Isah Kera alisema kuwa sheria ile iliwalazimisha baadhi ya wapenzi kuhama na kwenda kufunga ndoa sehemu nyingine.

Mwanakijiji mwingine, Sani Kera alisema kuwa ana watoto watano ambao wako tayari kuoa, lakini mipango yao imebidi ihairishwe.

Mahari ni nini?

Utamaduni wa kutoa mahari upo katika nchi nyingi ulimwenguni zikiwamo barani, Asia, Mashariki ya Kati, sehemu kadhaa za Afrika na pia katika baadhi ya visiwa vya pasifiki.

Kiwango kinachotolewa hutofautiana kuanzia zawadi ndogo tu za kuendeleza utamaduni huo hadi maelfu ya dola za Marekani kwa mfano kama inavyoshuhudiwa katika ndoa za baadhi ya jamii.

Tangu jadi, utoaji mahari umekuwa ni utamaduni unaoheshimiwa na kuenziwa pakubwa hata miongoni mwa jamii za watu waliosoma na kuishi maisha ya kisasa.

Kwa kawaida mahari huwa ni kama mkataba wa makubaliano kabla ya ndoa ambapo mali kama ng'ombe, ngamia, mbuzi au hata pesa taslimu hulipwa na bwana harusi kwa familia ya bibi harusi ili apewe mke.

Iwapo mume hatotimiza mahari iliyokubaliwa kwa muda uliotolewa, kuna jamii ambao humrudisha mke nyumbani mpaka mume akamilishe kulipa mahari.

***BBC***



Nyumba zikiwa zimezingirwa na maji baada ya mvua kubwa kunyesha mlimani na kusababisha maporomoko ya mawe nchini Burundi. **PICHA AFP**

# Watu 23 wafariki kwa maporomoko

**BUJUMBURA, Burundi**

ZAIDI ya watu 23 wameripotiwa kufariki kutokana na maporomoko ya mlima yaliyoangukia nyumba za wakazi katika kijiji cha Nyabundu, Tarafa ya Mugina mkoani Cibitoke Magharibi mwa Burundi.

Taarifa kutoka eneo hilo zinaeleza kuwa mvua nyingi zilizonyesha usiku wa kuamkia juzi zimesababisha mlima ulio katika eneo hilo kukabiliwa na mmomonyoko wa ardhi na maporomoko ya tope zilizosababisha mafuriko katika nyumba zilizo katika eneo hilo.

Leonard Habonimana mkazi wa eneo hilo alieleza kuwa mvua ni nyingi katika eneo na kwamba hadi saa mbili asubuhi maiti za watu sita zilikuwa tayari zimeondolewa chini ya udongo ambao uliifunika kwenye eneo la Mugina.

Alisema tayari milima mitatu imemomonyoka katika eneo hilo la Mugina.

Mkuu wa Tarafa ya Mugina alibaini kuwa tayari miili ya watu 23 imeondolewa eneo hilo na kwamba shughuli za uokozi bado zinaendelea.

Hata hivyo, eneo kulikotokea mafuriko hayo na maporomoko ya ardhi limetajwa kuwa umbali wa kilometa tano na makao makuu ya tarafa ya Mugina.

Mvua nyingi zimekuwa zikinyesha siku za hivi karibuni nchini humu na kusababisha mafuriko makubwa.

Oktoba, mwaka huu watu wengine wa sita walipoteza maisha katika mtaa wa Carama Kaskazini mwa Jiji la Bujumbura.

Burundi imekuwa ikikabiliwa na athari za tabia nchi ambapo jua kali limekuwa likiharibu mimea mashambani na kusababisha njaa hususani katika mkoa ya kaskazini mwa nchi pamoja na mvua zilizosababisha mafuriko na maafa.

***DW***

# Heche ajitetea kauli ya wizi wa serikali

**Na Hellen Mwango**

SHAHIDI wa tisa, John Heche amedai mahakamani kuwa mtu anaposema kuna wizi unaofanywa na serikali ya awamu ya tano, ni wazi kuwa wizi huo unafanyika katika taasisi mbalimbali za serikali.

Alidai kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali wa zamani (CAG), Profesa Mussa Assad, aliwahi kuwasilisha bungeni taarifa iliyoonesha kuwa kuna wizi umefanyika serikalini wa kiasi cha Sh. trilioni 1.5.

Heche alidai mbali na CAG hata Rais Dk. John Magufuli, alishawahi kusema kuna wizi unafanyika serikalini na ndiyo maana anatumbua majibu.

Akiongozwa na Wakli wa utetezi, Peter Kibatala, Heche alidai kuwa Rais Magufuli ni wa serikali ya awamu ya tano.

Kuhusu kifo cha aliyekuwa mwanafunzi wa Chuo cha Usafirishaji (NIT) Akwilina Akwilini, shahidi huyo alidai kuwa anakumbuka Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini (IGP), Simon Sirro, wakati akiongea na makamanda wa Polisi Tanzania, alieleza kuwa kifo cha mwanafunzi huyo kilitokea kwa sababu polisi walishindwa kutimiza wajibu wao vizuri.

Alidai kuwa hata Kamanda wa Kanda Maalum Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, alimsikia akisema kuwa kifo cha Akwilina kilisababishwa na askari na tayari wameshawakamata watu wawili.

Vile vile, Heche alidai kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani aliyepita, Mwigulu Nchemba, akiwa bungeni alitoa taarifa ya kupotea kwa watu mbalimbali wakati akijibu swali la kuhusu kupotea kwa Ben Saanane.



Mkurugenzi wa Tigo Kanda ya Pwani, Joseph Mutalemwa (kulia), akimkabidhi funguo ya gari mkazi wa Zanzibar, Shaban Khamis Ali, baada ya kuibuka mshindi wa shindano la Tigo Chemsha Bongo, jijini Dar es Salaam jana. Shindano hilo lilienda sambamba na msimu wa Tigo Fiesta 2019 unaotarajia kumalizika kesho Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wataalamu afya watakiwa kwenda kidijitali

**Na Beatrice Shayo**

WATAALAMU wa afya wametakiwa kukuza ujuzi wao ili kukidhi huduma za kisasa za kidijitali kuendana na kasi inayokua duniani.

Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Ellen Mkondya, alitoa rai hiyo wakati akizindua kongamano la tatu la wanasayansi jijini Dar es Salaam, jana.

Alisema teknolojia haiwezi kukimbiwa, hivyo wataalamu wajiandae kiujuzi zaidi ili kuitumia.

"Kukua kwa teknolojia kunaweza kumpunguzia kazi daktari kwa kuona wagonjwa, hivi sasa watu wana vifaa vya kujipima wenyewe mtu anaweza kujua namna mapigo yake ya moyo yanavyoenda anaona hakuna haja ya kumuona mtaalamu, lakini ni lazima tubaki kuwa ni watu tunaohitaji kutoa utaalamu, tujitahidi kukua zaidi na sio kuiogopa teknolojia," alisema Dk. Mkondya.

Aliitaka hospitali hiyo iendelee kuwa kituo cha umahiri na ubora, tofauti na hospitali nyingine na kuzijengea uwezo hospitali za rufani na maendeleo ya matibabu kidijitali yamewezesha tiba za kibingwa ikiwamo kuhifadhi takwimu za wagonjwa.

"Kumekuwa na wasiwasi kwamba teknolojia hiyo inaweza kuondoa ukaribu kati ya mtoa huduma na mpokeaji, hususani matumizi ya kompyuta wakati wa kufanya majadiliano na mgonjwa. Inafaa kujua matumizi sahihi ya teknolojia ili isisababishe matokeo hasi, pia mifumo mingi inahitaji uwapo wa rasilimali fedha za kutosha ili kuiweka," alisema Dk. Mkondya.

Kaimu Mkurugenzi MNH, Dk. Hedwiga Swai, alisema kongamano hilo lilitanguliwa na mafunzo kwenye maeneo mbalimbali ya utafiti ambayo ni mojawapo ya mikakati waliyojiwekea ili kuongeza uwezo wa kufanya utafiti hasa zenye malengo ya kuboresha utoaji wa huduma.

Alisema kaulimbiu ya kongamano hilo ni 'huduma za afya katika zama za kidijitali' yaendane na mwelekeo wa serikali na dunia kwa kutumia teknolojia ili kurahisisha na kuboresha utoaji wa huduma.

# Watanzania washauriwa matumizi bidhaa za rangi

**Na Mwandishi Wetu**

WATANZANIA wameshauriwa kutumia bidhaa bora ya rangi ya Jk Wall Putty ambayo inaweza kupendezesha kuta za nyumba pamoja na kupata rangi inayoweza kudumu kwa muda mrefu.

Ushauri huo ulitolewa jijini Dar es Salaam jana na Mkurugenzi Mkuu wa Jk Cement, Amint Kothari, katika hafla ya kutangaza kuunganisha kampuni mbili za Jk White Cement (Afrika) ambayo ni sehemu ya Kampuni ya Jk Cement ya India na kampuni ya uzalishaji wa rangi ya Goldstar ya Tanzania ili kuingiza sokoni bidhaa mpya ya Jk Wall Putty.

Mkurugenzi huyo akizungumza na waandishi wa habari aliwaomba kutumia bidhaa zao hizo kwa sababu rangi ya Jk Wall Putty ni suluhisho kwa kuwa inastahimili kwa muda mrefu huku ikihakikisha mwonekano ang'avu na nyororo kwenye kuta.

Pia alisema rangi hiyo inaondoa uhitaji wa kutumia gypsum plaster ambayo ni njia inayozoeleka nchini na kwamba Kampuni ya Goldstar Paints ikiwa na mzalishaji wa bidhaa bora sokoni, itatoa nafasi kwa Jk Wall Putty kuingiza sokoni kwa haraka zaidi na Jk Wall Putty itapatikana kwenye maduka yote ya Goldstar Paints na mawakala wake.

Kuhusu ushirikiano huo Mkurugenzi Kothari alisema: "Sisi kama Jk White Cement, siku zote tumekuwa na azma ya kuzalisha bidhaa zenye ubora na huduma nzuri kwa wateja wetu, ikiwa tumefanikiwa kufika maeneo mengi ulimwenguni kwa kuwa na nembo na mikakati imara ya kukuza soko la bidhaa zetu," alisema Kothari.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Goldstar Paints K Srinivasan, alisema kampuni yao imekuwa mstari wa mbele kwenye soko katika kuhakikisha kwamba inaleta bidhaa zenye viwango vya juu.

**Kuhusu ushirikiano huo Mkurugenzi Kothari alisema: "Sisi kama Jk White Cement, siku zote tumekuwa na azma ya kuzalisha bidhaa zenye ubora na huduma nzuri kwa wateja wetu, ikiwa tumefanikiwa kufika maeneo mengi ulimwenguni kwa kuwa na nembo na mikakati imara ya kukuza soko la bidhaa zetu," alisema Kothari.**

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### KAZI /AJIRA

**Nafasi za kazi** ualimu masomo ya sst/diploma 0656490706/0784142792


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**au piga simu: 0782253676**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA – MWANZA**

**SHAURI NA. 423 LA 2016**

**WINIFRIDA EZEKIEL.......................................MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

1. **DIAMOND TRUST BANK LTD**
2. **BONIPHACE K. MALIJA**
3. **MAJEMBE AUCTION MART**
4. **JABIL M. MWAMBASHA**
5. **MARTHA CHARLES**

**...................... WADAIWA**

**WITO WA KUITWA MAHAKAMANI**

**KWA: BONIPHACE K. MALIJA**
**MARTHA CHARLES**

Mnafahamishwa kwamba Mleta maombi hapo juu amefungua Shauri/Ombi dhidi yako katika Baraza la Ardhi na Nyumba Mkoa wa Mwanza, ombi hili limepangwa kutajwa tarehe 11/12/2019 katika Chumba cha Baraza, Barabara ya Posta Jengo liko Mkabala na Mahakama Kuu ya Biashara, Tanzania.

Kwa hivyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza siku hiyo wewe mwenyewe, wakili wako au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria.

KAA – Mkijua kwamba kushindwa kufika, Baraza litasikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila nyinyi kuwepo.

Imetolewa name kwa Amri na Chapa ya Baraza leo tarehe 22/10/2019.

115546502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika Mahakama ya Mwanzo: **DODOMA MJINI**

Usimamizi wa Mirathi No. 88/2019
Ombi la **ATHUMAN HUSSEIN** kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya Marehemu **HUSSEIN HASAN MLELWA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe ……………..kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 02/12/2019

115545901


***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa***

***Kutangaza Nasi***

***Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie 0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI MICHEZO



# LAMPARD
## AVUTIWA KIWANGO CHELSEA

**LONDON, England**

FRANK Lampard amewasifia wachezaji wake wa Chelsea kwa kusahau kipigo walichokipata kwa West Ham na kuonyesha kiwango cha kuvutia wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Aston Villa, juzi Jumatano.

Mabao kutoka kwa mchezaji wa zamani wa Villa, Tammy Abraham na Mount yalitosha kuipa ushindi huo Chelsea katika mechi ya Ligi Kuu England.

Ingawa Chelsea walishindwa kupata bao la tatu, kocha huyo alionyesha kuridhika na kiwango cha kikosi chake hasa baada ya kutoka kufungwa na West Ham Jumamosi iliyopita.

Akiwa ameendelea kushika nafasi ya nne katika msimamo wa ligi hiyo, Lampard alisema: “Nafikiri tulikuwa bora. Kwa uhakika kilikuwa kiwango cha kuvutia zaidi.

“Tulicheza mchezo wetu na kwa uhakika kabisa nimeridhika na kiwango. Ilikuwa ni sisi tena. Tulicheza kwa kiwango kibaya dhidi ya West Ham.

“Lakini wachezaji wangu wanacheza kwa kiwango kizuri, kwani hata kama tukipoteza hatufungwi mabao mengi na huwa tunatengeneza nafasi za kutosha.”

## SOLSKJAER: UNITED ILIONYESHA KIWANGO BORA

**MANCHESTER, England**

OLE Gunnar Solskjaer amesifia utawala wa kiwango cha Manchester United kilichoonekana katika mechi dhidi ya Tottenham, akielezea kwamba walicheza kwa kiwango bora kwa “muda mrefu”.

United walikuwa hawajashinda mechi tatu katika mashindano yote na walikutana kwa mara ya kwanza na Jose Mourinho tangu alipofukuzwa kama kocha pale Old Trafford Desemba mwaka jana.

Lakini vijana hao wa Solskjaer walimaliza mwanzo wa ushindi wa Mourinho akiwa na Spurs kwa kushinda 2-1, huku mabao yote yakifungwa na Marcus Rashford.

Dele Alli alifunga bao la kuvutia la kusawazisha dakika sita kabla ya mapumziko, kitu ambacho Solskjaer amekielezea kwamba ulikuwa wakati mgumu kuutawala mchezo huo.

“Hasa katika kipindi cha kwanza, pengine tulicheza kwa ubora zaidi kwa muda mrefu,” alisema akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

“Tulitawala mchezo na tungeweza kumaliza mchezo mapema tu wakati wowote.

“Golikipa aliokoa hatari nyingi, lakini walipata bao kabla ya mapumziko na unafikiri tulikabiliwa na wakati mgumu.”




## LJUNGBERG AMWEKEA MIPANGO PEPE

**LONDON, England**

FREDDIE Ljungberg anapanga kupata mambo mazuri zaidi kutoka kwa Nicolas Pepe aliyesajiliwa kwa ada iliyoweka rekodi baada ya kutokuwa na mwanzo mzuri zaidi Arsenal.

Pepe alihamia pale kwenye dimba la Emirates akitokea Lille kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 72, Agosti, mwaka huu, lakini winga huyo mwenye umri wa miaka 24 amefunga bao moja tu katika mechi 12 za Ligi Kuu England alizocheza.

Wakati wa mchezo wa kwanza wa Ljungberg akiwa kama kocha wa muda Jumapili wakitoka sare ya 2-2 dhidi ya Norwich City, Pepe alikuwa benchi na hakutumika na mara ya mwisho alianza kwenye mchezo dhidi ya Crystal Palace mwishoni mwa Oktoba.




Na Ljungberg sasa anataka kumsaidia mchezaji huyo wa Ivory Coast kuwa kwenye kiwango bora zaidi pale kwa washikabunduki.

“Nico ni mchezaji mzuri zaidi. Wakati mwingine unapokuja kutoka kwenye ligi tofauti inachukua muda kuzoea mazingira kwenye ligi mpya – ndani ya uwanja na nje ya uwanja,” amesema mchezaji huyo wa zamani wa Arsenal akiwaambia waandishi wa habari.

“Nina mpango wa kuzungumza naye kujua namna anavyojisikia. Yeye ni mchezaji muhimu, lakini majadiliano yetu yatabakia ya mimi na yeye.

“Nafikiri ni nchi mpya kwake, sehemu ambayo kuna aina mpya ya kucheza. Nitazungumza naye kwa ufundi kuhusu nini nitachokitarajia na namna gani nataka yeye acheze.”

## HABARI MICHEZO




# MANE

## ALISTAHILI KUWA 3 BORA BALLON D'OR - GUEYE

**LIVERPOOL, England**

NYOTA wa Liverpool, Sadio Mane alistahili angalau kumaliza kwenye tatu bora ya tuzo za Ballon d'Or, kwa mujibu wa mchezaji mwenzake wa Timu ya Taifa ya Senegal, Idrissa Gueye.

Huku Lionel Messi akitwaa Ballon d'Or kwa mara ya sita na kuweka rekodi Jumatatu, Mane alimaliza akiwa nafasi za nyuma ya nyota huyo wa Barcelona, mchezaji mwenzake wa Liverpool, Virgil van Dijk na nyota wa Juventus, Cristiano Ronaldo.

Kiungo huyo wa Paris Saint-Germain, Gueye anaamini Mane alistahili zaidi baada ya kuwa na mwaka wenye mafanikio kwake.

"Alistahili kuwa jukwaani," alisema Gueye baada ya PSG kushinda 2-0 dhidi ya Nantes katika Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, juzi Jumatano.

"Kwa upande wangu, alistahili angalau kuwa kwenye jukwaa la tuzo za Ballon d'Or. Kwa bahati mbaya kamaliza nafasi ya nne na hiyo ni aibu. Najisikia huzuni kwa ajili yake.

"Yeye ndio chanzo cha ufahari wa Wasenegal wote. Kwa kile alichokifanya msimu uliopita, kwa uhakika alistahili kupata kilichopo bora kabisa."

Mane kwa mara nyingine alionyesha kiwango chake Jumatano kwa kufunga mabao mawili wakati Liverpool wakiibuka na ushindi wa magoli 5-2 dhidi ya Everton pale kwenye Uwanja wa Anfield.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 sasa amefikisha mabao 13 na kutoa pasi za mwisho 21 kwenye mashindano yote msimu huu.

# Klopp asifia kiwango cha Origi

**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp amemsifia Divock Origi kwa "kiwango cha kuvutia" wakati Liverpool wakiibuka na ushindi wa mabao 5-2 dhidi ya Everton, juzi Jumatano.

Origi alianza mchezo wake wa kwanza wa Ligi Kuu tangu Oktoba mwaka huu na alitumia nafasi nzuri pale Anfield, akifunga mabao mawili kwenye ushindi huo wa Liverpool.

Bao la pili la mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji alilifunga kwa stadi akiunganisha pasi nzuri ya Dejan Lovren na kocha akamsifia kwa kiwango chake.

"Kiwango cha kuvutia. Alicheza mchezo wa kuvutia. Sio tu mabao aliyofunga, lakini namna yalivyokuwa ya aina yake," alisema Klopp akiwaambia waandishi wa habari.

"Bao lake la kwanza lilikuwa bora zaidi kwa ujumla, akipata mpira kupitia kwa Adam (Lallana) pasi ikaenda kwa Sadio (Mane), Sadio na mpira ulipomfikia akaugusa mara moja na kupata bao."

Klopp alifanya mabadiliko matano kwenye kikosi cha kwanza dhidi ya 'dabi' hiyo ya Everton, huku Origi, Adrian, Lallana, Shaqiri na James Milner wakianza.

Ulikuwa mchezo wa kwanza kwa Shaqiri kuanza msimu huu na Klopp alimwomba radhi mshambuliaji huyo, huku akikisifia kikosi chote cha Liverpool.

"Samahani kwa Shaq! Aliumia kwa muda mwingi," alisema Klopp.

# Tuchel azungumzia hali ya Cavani PSG

**PARIS, Ufaransa**


KOCHA Mkuu wa Paris Saint-Germain, Thomas Tuchel, amesema anahuzunishwa na hali ya Edinson Cavani kwa kukosa nafasi kwenye kikosi hicho kwa sasa.

Cavani ambaye mkataba wake na klabu hiyo unamalizika mwishoni mwa msimu huu alitokea benchi wakati PSG ikiibuka na ushindi wa 2-0 kwenye Ligue 1 dhidi ya Nantes juzi Jumatano.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, ambaye amekuwa akihusishwa na mpango wa kwenda Ligi Kuu Marekani, MLS, aliingia kwenye mchezo huo dakika ya 87.

Cavani ameanza michezo minne tu kwenye Ligue 1 msimu huu na mitano katika mashindano yote katika msimu huu wa 2019-20.

Alipoulizwa kuhusu mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay, Tuchel aliwaambia waandishi wa habari: "Nimezungumza nae. Wote tunajua kwamba ni wakati



mgumu zaidi kwa upande wake. Na sio tu maamuzi magumu kwa upande wangu, inahuzunisha pia.

"Tumecheza mechi nyingi kwa kuwatumia washambuliaji watatu, mmoja namba tisa. Cavani alikuwa ameumia mwanzoni mwa msimu, sio kosa lake. Mauro (Icardi) alicheza vizuri zaidi kwa kipindi hicho, alifunga mabao mengi.

"Kama tukicheza mfumo wa 4-3-3, tunakuwa na wachezaji watatu wanaocheza mbele na mmoja namba tisa, Kylian (Mbappe), Mauro na yeye. Nina huzuni kwa sababu sina namna ya kumjumuisha kwenye kikosi cha kuanza kwa sasa.

"Hastahili hilo, ni mchezaji mwenye kiwango cha juu na ana njaa ya mafanikio, ni muhimu kwa timu. Lakini kwa wakati huu sina nafasi ya kumpa acheze zaidi."

Cavani, ambaye aliwasili hapo akitokea Napoli mwaka 2013-14, amefunga mabao mawili kwa kikosi hicho cha Tuchel msimu huu.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MOURINHO AKIRI SPURS ILIZIDIWA

Aeleza United ilistahili ushindi kwa sababu wachezaji wake walishindwa...

**MANCHESTER, England**

JOSE Mourinho amekubali Manchester United ilistahili kuifunga Tottenham wakati akirudi Old Trafford kwa mara ya kwanza tangu afukuzwe hapo.

Mabao ya Marcus Rashford na lile la kufutia machozi la Dele Alli ilimaanisha kwamba Mourinho na Tottenham yake walipoteza kwa magoli 2-1 katika mchezo wa Ligi Kuu England uliochezwa juzi usiku, na akimaliza rekodi yake ya mwanzo nzuri wa asilimia 100 tangu alipochukua mikoba ya kuinoa Spurs kutoka Mauricio Pochettino.

Spurs ilikosa nguvu, lakini Mourinho alikataa kama mchezo huo ulistahili penalti iliyotolewa kwa faulo ya Moussa Sissoko na ikafungwa na Rashford na kuifanya United kupata bao la pili na la ushindi mapema kipindi cha pili.

"Nafikiri wao (United) walistahili ushindi katika kipindi cha kwanza, hatukuanza vizuri kabisa," alisema Mourinho akiwaambia waandishi wa habari.

"Nafikiri dakika 30 za kwanza zilikuwa bora kwa timu yao kwa sababu ya hilo, dakika 30 za mwanzo tulionekana hatukuwa kabisa mchezoni.

"Pia namna tulivyoruhusu bao la pili, nafikiri walistahili kushinda.

"Kama nikiangalia mechi tatu zilizopita ambazo tulishinda, hatukuanza vizuri. Timu haianzi mechi vizuri, inakuwa ngumu kufutata nguvu yetu katika mchezo.

"Niliwaambia wao kuhusu Old Trafford, kuhusu baadhi ya wachezaji kama vile (Scott) McTominay ambaye alionyesha ubora wake haraka kwenye mchezo, Rashford alikwenda kumjaribu golikipa, aina hii ya ari inayoonyeshwa mapema ilitufanya sisi tuonekane kama vile hatupo mchezoni.

"Baada ya hapo tukapata mpira, tulicheza na kufunga na tungeweza kutengeneza nafasi zaidi, halafu katika kipindi cha pili nilifikiri kabisa kwamba tutakuwa kwenye utawala wa mchezo kama tulivyomaliza kipindi cha kwanza.

"Tuliruhusu bao ambao haiwezekani kuliruhusu kama tunatakiwa kushinda, tulilala, hatukuwa na utawala. Halafu kile kilichotokea ndani ya "box" ni matokeo ya kulala kwetu."

Spurs watarudi tena katika Ligi Kuu England kwa kucheza dhidi ya Burnley hapo kesho Jumamosi na sasa wamepitwa na United kwenye msimamo wa ligi hiyo, wako katika nafasi ya sita.

"Nahitaji kufanya kazi kwa sababu hadi sasa ni kama sijafanya kazi yoyote, ndani ya wiki mbili tunakuwa na mechi," alisema Mourinho, ambaye alifukuzwa United mwaka mmoja uliopita.

## KWA UFUPI

**SOUTHGATE ATAJWA UNITED**

MANCHESTER United inaweza kurejesha mchakato wa kumwajiri Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya England, Gareth Southgate, kama itafikia uamuzi wa kuachana na Ole Gunnar Solskjaer, utakapofika mwisho wa msimu huu. ***(Sun)***

**UNITED YAHITAJI WAKALI**

KOCHA Msaidizi wa Manchester United, Mike Phelan, amesema kuwa klabu hiyo bado inahitaji kusajili "wachezaji nyota" ili kuboresha kikosi chake. ***(Evening Standard)***

**SANCHO KUIKAMUA CHELSEA**

CHELSEA imesema kuwa iko tayari kuvunja rekodi yake kwa kutumia kiasi kikubwa cha fedha ili kunasa saini ya mshambuliaji wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho, ambaye ana umri wa miaka 19. ***(Goal)***

**VIEIRA AKARIBIA ARSENAL**

KIUNGO wa zamani wa Arsenal, Patrick Vieira, ambaye sasa anaifundisha Nice ya Ufaransa, anatajwa kuongoza katika orodha ya kuwa kocha mpya wa Gunners kufuatia klabu hiyo kumtimua Mhispania Unai Emery. ***(Nice-Matin, via Mail)***

**ZIDANE AMGANDA POGBA**

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, bado anataka kuona kiungo wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Paul Pogba (26), anatua Bernabeu. ***(Marca)***

**MATIC SAFARI IMEIVA**

MANCHESTER United inatarajia kumjumlisha kiungo wake Mserbia, Nemanja Matic (31), kama sehemu ya kumnasa kiungo mchezeshaji wa Timu ya Taifa ya Denmark, Christian Eriksen (27) anayeichezea Tottenham. ***(The Athletic - subscription required)***

**SANCHO KUBAKIA DORTMUND**

IMEELEZWA kuwa mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho, ambaye aliwahi kuitumikia Manchester City, hana nia ya kuondoka katika klabu hiyo inayoshiriki Bundesliga katika dirisha dogo la usajili la Januari. ***(Bild, via Mirror)***

**CITY: STERLING WETU**

MABOSI wa Manchester City, wanaamini kuwa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya England, Raheem Sterling (24), atasaini mkataba mpya ambao utamfanya kuwa mchezaji anayelipwa kiasi kikubwa ambacho hakijawahi kutokea katika klabu hiyo. ***(Metro)***

**ADEYEMI AGOMBEWA ULAYA**

LIVERPOOL na Arsenal zimeungana na Barcelona katika vita ya kuwania saini ya straika Mjerumani, Karim Adeyemi (17), ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo katika klabu inayoshiriki Ligi Daraja la Pili nchini Austria, Liefering akitokea RB Salzburg. ***(Sport via Mirror)***

**SIMEONE KUONDOKA ATLETICO**

KOCHA wa Atletico Madrid, Diego Simeone, ambaye aliwahi kuwindwa na Everton, anakaribia kuondoka katika klabu hiyo ya Hispania. ***(Marca via Sport Witness)***

**DIGNE, EVERTON SAFI**

EVERTON inajiandaa kumpa mkataba mpya na wa muda mrefu beki wa kushoto wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Lucas Digne, ambaye ana umri wa miaka 26. ***(Mail)***

**KESSIE AKARIBIA WEST**

WEST Ham inatajwa kuwa katika nafasi nzuri dhidi ya Wolves katika vita ya kuwania saini ya kiungo wa AC Milan na Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Franck Kessie (22). ***(Milan Live)***

HABARI MICHEZO

# BAYI AWATAKA WACHEZAJI WAJITUME, WASILALAMIKE

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

WANAMICHEZO wa hapa nchini wametakiwa kuacha kuilaumu serikali kwa wawakilishi wake kufanya vibaya katika mashindano mbalimbali wanayoshiriki na badala yake wametakiwa kujituma na kuongeza bidii ili kufikia malengo waliyojiwekea.

Ushauri huo umetolewa jana na Katibu Mkuu wa Kamati ya Olimpiki Tanzania (TOC), Filbert Bayi, katika ufunguzi wa mkutano mkuu wa mwaka wa kamati hiyo na pia amewakumbusha wanamichezo wote kutambua kuwa michezo ni ajira na biashara.

Bayi alisema kuwa vyama vya michezo vinapaswa kuweka mazingira bora kwa wanamichezo ili waweze kufikia malengo na viwango vinavyotambulika kimataifa.

Alisema kuwa idadi ya wanamichezo wanaoshiriki Michezo ya Olimpiki kutoka Tanzania imekuwa ikipungua kwa sababu ya kukosekana kwa jitihada za mchezaji mmoja mmoja au vyama wanavyotoka.

"Sio kwamba Tanzania inashindwa kushiriki katika mashindano hayo ya Olimpiki, lakini tunaendelea kupambana kuhakikisha tunaongeza kiwango cha ushiriki, kwa miaka miwili iliyopita tumeweka namba sawa sawa ya watu saba lakini inawezekana mwaka huu ikapungua tena kutokana na wachezaji wawili tu ndio walifikia viwango,"alisema Bayi.

Kiongozi huyo alisema kuwa bado anaimani idadi ya wanamichezo watakaofikia viwango vya kushiriki Michezo ya Olimpiki itaongezeka kwa kipindi cha kuanzia Januari hadi Juni mwakani.

Hata hivyo, Bayi, alisema wameendelea kuwashawishi na kuwashauri vijana ambao wanaibukia kuwa na uzalendo katika michezo wanayoshiriki na sio kufikiria zaidi fedha na kuwaeleza kwamba kupata medali kunaipa pia nchi sifa nzuri.

Naye mwanariadha, Alphonce Simbu, alisema kuwa ni vema maandalizi ya kushiriki michezo hiyo yakaanza mapema ili kuwaweka tayari kwenda kushindana.

Mwenyekiti wa Wanawake wa Michezo Kanda ya Tano, Irene Jackson, alisema kuwa wanamichezo sasa hivi wamekosa uzalendo tofauti na waliokuwa zamani kwa sababu ya kuangalia maslahi binafsi.

"Wanamichezo wa sasa ukiwaita kushiriki mashindano, kwanza anaanza kukuuliza atalipwa kiasi gani cha fedha, wakati anatambua michezo hiyo ni ya riadhaa," Irene alisema. Kiongozi huyo aliwataka wanamichezo wastaafu kuendelea kutoa ushauri na kuwajenga chipukizi ili wawe tayari kuiletea nchi heshima kupitia Michezo ya Olimpiki inayokuja.



Wanariadha, Damas Emmanuel (kulia) na Jeremia Baruti, wakiwa katika mazoezi ya kujiandaa na mashindano ya mbio za JICA kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam jana. Mashindano hayo yanatarajiwa kufanyika kesho kwenye uwanja huo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Zanzibar Heroes yapata msaada

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KATIKA kuhakikisha inakwenda kufanya vizuri kwenye mashindano ya Kombe la Chalenji mwaka huu, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), imetoa kiasi cha Sh. milioni tano kwa Timu ya Soka ya Zanzibar (Zanzibar Heroes), imeelezwa.

**Mashindano ya Kombe la Chalenji kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati yataanza kesho jijini Kampala na Zanzibar Heroes itaanza kampeni ya kuwania ubingwa huo Jumapili kwa kuwavaa Sudan.**

Afisa Uhusiano wa ZSSF, Juma Mmanga, alisema kuwa mchango huo ni kwa ajili ya kuisadia Zanzibar Heroes katika mahitaji yake muhimu wakati wakiwa Uganda katika michuano hiyo.

Rais wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Seif Kombo Pandu, alisema kuwa timu hiyo inahitaji hamasa zaidi kutoka kwa Wazanzibar ili ifanye vizuri katika michuano hiyo ambayo mwaka huu inashirikisha timu tisa.

Pandu alisema kuwa wanaishukuru ZSSF kwa mchango huo na kuongeza kwamba utakwenda kusaidia mahitaji ya wachezaji wao, ambao tayari wapo Uganda kwa lengo la kuwania kikombe hicho.

# Sanaa yawapaisha wanafunzi Dodoma

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

WANAFUNZI 20 kati ya 500 wa Shule za Msingi wa jijini Dodoma, wameibuka washindi katika tamasha maalumu la kuibua na kukuza vipaji mbalimbali "Mavunde Talent Search 2019", imefahamika.

Tamasha hilo limefanyika chini ya ufadhili wa Mbunge wa Jimbo la Dodoma Mjini, ambaye pia ni Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Anthony Mavunde, na malengo yake ni kuibua vipaji vya watoto kupitia sanaa mbalimbali ikiwamo uimbaji, kupiga piano, gitaa, ngoma, mpira wa miguu na netiboli.

Mmoja wa washindi ni mwanafunzi wa Shule ya Msingi ya Chadulu, Nuru Kwangaya (10), ambaye aliibuka mshindi katika kipengele cha uimbaji baada ya kufanya vema na kutoa burudani safi kwa wageni waliohudhuria tamasha hilo.

Akimtangaza mshindi huyo jana, Mratibu wa shindano hilo, Samwel Marwa, alisema wanafunzi hao wamepata ufadhili wa kusomeshwa bure katika shule ya Ellen White English Medium.

"Tuna kila sababu ya kumshukuru mbunge wetu, ametoa Sh. milioni 36 kwa ajili ya kuwalipia ada wanafunzi hawa, ikiwamo usafiri, chakula, vifaa vya kusomea na Ipad," alisema Marwa.

Mgeni katika shindano hilo, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini, Patrobas Katambi, aliagiza idara ya elimu kuhakikisha inakamilisha mchakato wa uhamisho wa wanafunzi hao mapema ili ifikapo Januari, mwakani wahamie katika shule hiyo.

Katambi aliwataka wazazi wote nchini kutowakatisha tamaa watoto wao pindi wanapoonyesha kuwa na vipaji, bali watakiwa kuwasaidia ili kuviendeleza.

# AZAM YATAMBA KUTETEA FA CUP

**Na Shufaa Lyimo**

MABINGWA watetezi wa mashindano ya Kombe la FA (Tanzania), Azam FC, wamesema kuwa wanaendelea "kujinoa" kwa ajili ya kuhakikisha wanafanya vizuri katika mashindano hayo ambayo bingwa wake anapata tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa mwakani.

Kocha Msaidizi wa Azam FC, Idd Cheche, alisema kuwa wamejipanga kuongeza umakini katika mashindano hayo kwa sababu hawataki kutolewa mapema katika michuano hiyo.

**"Tunajipanga vizuri kuhakikisha tunaiwakilisha tena nchi yetu, tunaomba mashabiki wetu wazidi kutuombea na kutupa ushirikiano ili tutimize malengo tuliyonayo," alisema Cheche.**

Kocha huyo aliongeza kuwa wanafahamu mashindano hayo yatakuwa na ushindani na wataingia kwa tahadhari kuanzia mchezo wa kwanza kwa sababu wapinzani wao, African Lyon wana uzoefu pia na michuano hiyo.

Azam FC itaanza kampeni ya kutetea kombe hilo kwa kucheza dhidi ya African Lyon wakati Simba wataikaribisha Arusha FC huku Iringa United ikiwafuata Yanga jijini Dar es Salaam kati ya Desemba 20 na 22, mwaka huu.

# Michezo

Ijumaa Desemba 6, 2019

Nipashe




Mourinho akiri Spurs ilizidiwa

HABARI UK 30



Mshambuliaji wa Tottenham, Dele Alli (kulia), akifunga bao la kusawazisha kwa timu yake huku golikipa wa Manchester United, David De Gea, akishindwa kuzuia hatari hiyo. United ilishinda mabao 2-1. **PICHA: MTANDAO**

# KASEJA ATEMWA KILIMANJARO STARS

**Nyota 22 waondoka kwenda kusaka ubingwa wa mashindano hayo unaoshikiliwa na ...**

**Na Somoe Ng'itu**

KATIKA hali ya kushangaza, aliyekuwa kipa chaguo la kwanza wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Juma Kaseja, ameachwa katika kikosi kitakachoshiriki mashindano ya Kombe la Chalenji ambayo yanatarajiwa kufanyika kuanzia kesho Desemba 7 hadi 19, mwaka huu jijini Kampala, Uganda.

Baada ya Kaseja kuachwa, magolikipa watatu waliobakia kwenye kikosi cha Kilimanjaro Stars chenye wachezaji 22, kilichoondoka nchini jana kwenda katika mashindano hao ni pamoja na Aishi Manula wa Simba, Metacha Mnata (Yanga) na David Kisu, ambaye anaidakia Gor Mahia ya Kenya.

Kaseja alikuwa ni mmoja wa wachezaji waliokuwa kwenye kikosi hicho kinachoongozwa na Kocha, Juma Mgunda, Suleiman Matola na Zuberi Katwila, waliofanya kikamilifu hadi mazoezi ya mwisho ya kikosi hicho yaliyofanyika jana asubuhi.

"Mimi siwezi kusema ni kwa nini nimeachwa, wenye nafasi nzuri ya kulizungumzia uamuzi huo ni wakubwa (benchi la ufundi) wenyewe, ila hadi kwenye mazoezi ya mwisho leo (jana), asubuhi nilikuwepo," alisema Kaseja, ambaye alisimama langoni katika mechi zote ambazo Taifa Stars imesheza na hatimaye kukata tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

Nyota wengine walioachwa katika kikosi hicho ni pamoja na Iddi Suleiman "Nado", Salum Aboubakar "Sure Boy", Frank Domayo na Shabani Chilunda.

Mgunda alisema kuwa amelazimika kuwaacha wachezaji hao kwa sababu ni majeruhi na wanahitaji kupata muda zaidi wa kupona ili taifa na klabu zao ziwatumie hapo baadaye.

"Kubwa ambalo limetokea kwa vijana hawa ni kupata majeraha wakati wa mazoezi, Nado ameumia siku moja kabla hatujasafiri, Chilunda alikuja akiwa ameumia, mchezaji wangu mkongwe, nahodha wangu, Kaseja alipata maumivu mguu wake wa kulia, madaktari wameshauri akafanyie vipimo na matibabu yaanze haraka, tutamhatarisha tukiendelea kumtumia," alisema Mgunda.

Aliongeza kuwa kikosi chake kimejiandaa vizuri kwenda kupambana na kusaka matokeo mazuri ili kulinda heshima ya nchi.

"Ni jukumu zito ambalo tumepewa na Watanzania, tunakwenda kushindana, katika ukanda wetu ni mashindano makubwa, vijana wako tayari, yoyote tutakayekutana naye ni mshindani wetu," alisema Mgunda.

Naye beki wa timu hiyo, Bakari Mwamnyeto, amesema kuwa wachezaji wanaahidi wanakwenda kushindana ili kurejea na ubingwa.

"Hii ni mara yangu ya kwanza kushiriki mashindano haya ya Chalenji, tumejiandaa vizuri, tunaenda kusaka ushindi, tunawaahidi mambo mazuri, " alisema beki huyo anayeichezea Coastal Union.

Wachezaji wengine wa Kilimanjaro Stars waliosafiri jana ni pamoja na Juma Abdul, Nickson Kibabange, Gadiel Michael, Mwaita Gereza, Mohammed Hussein "Zimbwe Jr", Bakari Mwamnyeto, Kelvin Yondani, Baraka Majogoro, Jonas Mkude, Zawadi Mauya, Mzamiru Yassin, Hassan Dilunga, Cleofas Mkandala, Paul Nonga, Miraji Athumani, Eliuter Mpepo, Kikoti Lucas na Rashid Chambo.

Kilimanjaro Stars itaanza kampeni ya kuwania ubingwa huo keshokutwa kwa kuwavaa mabingwa watetezi Harambee Stars ya Kenya, halafu itacheza mechi yake ya pili dhidi ya Zanzibar hapo Desemba 10 na itamaliza hatua ya makundi kwa kuvaana na Sudan hapo Desemba 14, mwaka huu.

## Simba: Tulihitaji huduma ya Okwi

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya aliyekuwa Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems, kusema kuwa hakuridhia kuondoka kwa mshambuliaji Emmanuel Okwi, uongozi wa timu hiyo umeibuka na kusema Mganda huyo alihitaji kupata changamoto mpya.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, alisema kuwa Okwi aliamua kuondoka klabuni hapo baada ya kupata "ofa nono" na si kuachwa na viongozi.

**"Hakuna kiongozi wa Simba ambaye alipenda kumuacha Okwi, mwaka 2018 tulitaka kumwongeza mkataba ili umalizike mwaka 2021, lakini alikataa akasema, anahitaji amalize mwaka huu na anataka kwenda kutafuta changamoto nyingine, hivyo hivyo kwa Kotei (James) ambaye alipata "dili" la Kaizer Chiefs," alisema Manara.**

Aliongeza kuwa pia klabu hiyo ilichelewa kufanya uamuzi wa kumtimua Aussems, ambaye alikuwa amewagawa wachezaji katika makundi mawili, jambo ambalo halikuwa na "afya" kwenye timu hiyo.

Kiongozi huyo alisema pia kocha huyo alikuwa ni mtu asiyependa kupewa ushauri, na wakati mwingine akitoa kauli za kuwakatisha tamaa baadhi ya wachezaji.

"Kuna mechi wenzake walimshauri amchezeshe Dilunga (Hassan), bahati nzuri tulishinda, baada ya mechi akasema Dilunga ndio nani na mchezaji mwenyewe alisikia, akaamua kuondoka na kesho yake akasusia mazoezi," Manara alisema.

Aliongeza kuwa mbali na kutolewa mapema kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu, Aussems, ameweka rekodi mbaya ya kufungwa mabao mengi ugenini katika michuano hiyo msimu uliopita.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >